# MAUDHUI YA MABADILIKO NA UKUAJI WA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LANGU* NA *DUNIA MASHAKA MAKUU*

**ELIZABETH KERRE**

**C50/CE/28514/2013**

**TASNIFU HII IMEWASILISHWA KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**NOVEMBA, 2020**

# IKIRARI

Tasnifu hii ni kazi yangu asili na haijapata kuwasilishwa kwa madhumni ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine.

Mtahiniwa

Jina: **ELIZABETH KERRE** Sahihi ........ Tarehe 6/11/2020

**C50/CE/28514/2013**

Wasimamizi

Tasnifu hii ya utafiti imetolewa kwa idhini yetu kama wasimamizi katika Chuo Kikuu cha Kenyatta.

1. **PROF. KITULA KING'EI**

   Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

   Chuo Kikuu Cha Kenyatta.

   Sahihi................ Tarehe 10/11/2020......

2. **PROF. CATHERINE NDUNGO**

   Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika

   Chuo Kikuu cha Kenyatta.

   Sahihi................................Tarehe 10/11/2020

# TABARUKU

Naitabaruku kazi hii kwa mama yangu mpendwa Khadija Idd Mukoyani, mume wangu Pascal Njani Shikuku, wanangu Maria Resa Njani, Azariah Furaha Njani, Pio Faraji Njani na ndugu zangu wote. Maombi, ufadhili na ushauri mlionipa ulinipa ari ya kuikamilisha kazi hii.

## SHUKURANI

Kwanza namshukuru Mungu kwa kunijalia baraka, afya njema, uhai, na subira ya kutimiza malengo yangu. Kazi hii haingetimilika bila nguvu zake. Fadhili zake zimekuwepo nami tangu mwanzo hadi hatima ya kazi hii.

Shukurani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Profesa Kitula King'ei na Profesa Catherine Ndungo kwa kujitolea kuniongoza kwa busara na ukakamavu na kuhakikisha kazi yangu imekamilika. Maarifa mlionipa, fikra na mwongozo umenifaa sana kufikia kiwango hiki. Mungu awajalie afya njema na maisha marefu ili mwendelee kuwafaa wengine. Pia nawashukuru wahadhiri wote wa Idara ya Kiswahili kwa mwongozo na ushawishi mlionipa nilipohitaji msaada wenu.

Nachukua fursa hii kumshukuru mume wangu Pascal Njani kwa kunihimiza kila mara kuendelea na masomo, kunitia moyo kila wakati na zaidi ya hayo kwa kunifadhili. Mungu amjalie mema duniani. Namshukuru vilevile mamangu Khadija Mukoyani kwa kuniombea mema kila wakati na kutia moyo niendelee na masomo. Mama, umekuwa nguzo maishani mwangu. Nakuombea maisha marefu. Babangu marehemu Jackson Mukoyani Kerre aliyeitambua ndoto yangu nikiwa mdogo. Kweli nimeng'ang'ana kutimiza ndoto hiyo. Siwezi kuwasahau ndugu zangu wote kwa kunijengea msingi wa masomo yangu. Moses na Robert Kerre mlijitolea kwa hali na mali kunifadhili. Mungu awajalie mema yote duniani.

Hatimaye ningependa kuwashukuru wanafunzi wenzangu ambao tulianza nao safari ya usomi, Gladys Wachira, Harriet, Oluoch Scott, Munyoki, Atieno, Chris Khatete kwa mijadala tuliofanya pamoja iliyotufaa sana. Mungu awabariki. Bila kumsahau Stephen Mwendwa na Selly kwa ushauri wa kipekee mlionipa na kunitia moyo kila wakati.

## IKSIRI

Utafiti huu umelenga kuchunguza maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya za *Chozi Langu (*Mogambi, 2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (Omar, 2015). Mtafiti amechunguza mabadiliko ya tabia, hali, hisia na afya ya vijana baleghe kati ya umri wa miaka ya 10 - 19 na ukuaji wao. Masuala ambayo yamechunguzwa ni pamoja na malezi, umaskini, na mengineyo ambayo huwa chanzo cha mabadiliko ya tabia na ukuaji wa vijana. Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Uhalisia Lukacs (1972), imeendelezwa na Wamitila (2002), Ntaragwi (2004), Wafula na Njogu (2007) na wengine. Nadharia ya Uhalisia imeeleza kuwa kazi ya msanii inapaswa kuwasilisha ukweli kama ulivyo katika mazingira. Imetumika kuchunguza changamoto wanazopitia vijana baleghe katika jamii na suluhu zake. Pia, nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii imetumika. Nadharia hii iliasisiwa na Erickson (1950). Aliiendeleza nadharia hii katika kazi ya baadaye ikiwemo; Erickson(1982), Erickson na Erickson (1998). Waitifaki wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ni Cherry (2017), McLeod (2013) na wengine. Nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii imesisitiza jinsi ambavyo utangamano na uhusiano wa kijamii ni muhimu sana katika ukuaji wa binadamu. Imetumika kuchunguza mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe. Mbinu-kusudio imetumiwa kuteua vitabu teule. Mbinu ambayo imetumika katika ukusanyaji wa data katika utafiti huu ni usomaji wa riwaya mbili teule. Data ya utafiti huu ilipatikana maktabani ambapo vitabu teule vilisomwa kwa kina ili kupata data ya kubainisha aina ya mabadiliko na ukuaji na mambo yanayochangia maendeleo ya vijana. Pia mtafiti alisoma tasnifu na vitabu vingine vinavyojadili changamoto za vijana ili kuongeza nguvu utafiti huu. Data imechanganuliwa kulingana na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule. Mwishowe, matokeo yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Tasnifu hii ina sura tano: sura ya kwanza ina mada, maswali ya utafiti, malengo, upeo na mipaka, yaliyoandikwa kuhusu mada, sababu ya kuchagua mada na misingi ya nadharia. Sura ya pili imeshughulikia aina ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume katika riwaya teule, sura ya tatu imeshughulikia changamoto wanazopitia vijana wa kike na wa kiume katika jamii na suluhu zake, sura ya nne imeangazia mambo yanayochangia maendeleo ya wahusika vijana. Sura ya tano imejumuisha muhtasari, matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo. Utafiti huu umenuia kuwa wenye manufaa kwa wachanganuzi wa masuala ya kijamii, waandishi wa fasihi na vijana kwa sababu umeonyesha jukumu la kila mmoja katika kuleta mabadiliko chanya na kuwaendeleza vijana.

## ABSTRACT

This research intends to investigate the theme of change and development of adolescents in *Chozi Langu (*Mogambi, 2014) and *Dunia Mashaka Makuu* (Omar, 2015**).** The research has investigated the character, situation, feelings and health change and development of the adolescents between the ages of 10 to 19 years. The issues investigated are parenting, poverty among others that influence the character change in adolescents. The research is guided by the tenets of Realism theory Luckas (1972) which has been modified by Wamitila (2002), Ntaragwi (2004), Wafula and Njogu (2007) and others. It stresses on the depiction of life and society as it exists. The tenets of this theory have been used to investigate the different challenges that the adolescents face in the society and how they solve them. The research is also guided by the Psychosocial theory by Erickson (1950). He expanded and refined in later books; Erickson (1982) and Erickson and Erickson (1998). It was modified by Cherry (2017), McLeod (2013) and others. The Psychosocial theory stresses on the importance of social interaction and relationship in the development and growth of human beings. It has been used to investigate the theme of change and development of adolescents. The researcher has used purposive sampling to select the novels. Data was collected in the library through comprehensive reading of sampled novels in order to analyze the theme of change and development of adolescents. Also, thesis and other materials related to the topic were read. The collected data has been analyzed descriptively in line with the objectives and by the tenets of the theories of the study. Lastly, the results are presented by discussion method. The research project has been presented in five chapters: the first chapter covers the introduction, statement of the problem, scope, literature review and theoretical framework. Chapter two shows the types of change and development of adolescents in the texts, Chapter three investigates the challenges that the adolescents face in the society and their solutions, the fourth chapter investigates the factors that influence the progress of adolescent characters and lastly, the fifth chapter covers summary, conclusions and recommendations. The research intends to benefit social analysts, literature authors and adolescents because it has depicted the roles of each one of them in bringing positive change and development among the adolescents.

## MAELEZO YA ISTILAHI

Kijana : Mtu mwenye umri kati ya miaka kumi na minane hadi miaka thelathini na mitano. ( Kulingana na Katiba ya Kenya).

Kulingana na YALISA (2011) Kijana mdogo ni mtu mwenye umri wa miaka na miwili hadi kumi na nane.

Baleghe : Msichana au mvulana aliyefikisha umri wa miaka 10 mpaka19. Pia ni mvulana au msichana aliyeingia katika hali ya kuweza kuzaa.

Ukuaji : Ukuaji ni hali ya kuongezeka akili au kuwa na busara. Pia ni hali au namna ya kuongeza kimo.

Mabadiliko : Hali ya kuwa tofauti na ilivyokuwa mwanzo.

Komaa : Kuwa mtu mzima.

Changamoto : Ni jambo, kitu au hali inayomkabili na kumtatiza mtu.

Jamii : Viumbe wenye asili moja au wenye uhusiano.

Msongo : Uchovu pamoja na hofu apatayo mtu baada ya kusongwa na mambo mengi mazito akilini.

Saikolojia : Taaluma inayotoa mafunzo kumwezesha mtu kutoa fikra na mwenendo wa nafsi au akili ya binadamu.

Maendeleo : Hali ya kufanikiwa kijamii na kiuchumi.

## VIFUPISHO

YALISA - Young Adult Library Association

UNFP - United Nations Population Fund

**YALIYOMO**

**IKIRARI** ..... ii

**TABARUKU** ..... iii

**SHUKRANI** ..... iv

**IKSIRI** ..... v

**ABSTRACT** ..... vi

**MAELEZO YA ISTILAHI** ..... vii

**VIFUPISHO** ..... viii

**YALIYOMO** ..... ix

**SURA YA KWANZA** ..... 1

1.0 Usuli wa Mada ..... 1

1.1 Suala la Utafiti ..... 3

1.2 Malengo ya Utafiti ..... 4

1.3 Maswali ya Utafiti ..... 4

1.4 Sababu za Kuchagua Mada ..... 4

1.5 Upeo na Mipaka ..... 5

1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada ..... 6

1.7 Misingi ya Nadharia ..... 12

1.7.1 Nadharia ya Uhalisia ..... 13

1.7.2 Nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ya Erickson. ..... 15

1.8 Mbinu za Utafiti ..... 18

1.8.1 Muundo wa Utafiti ..... 18

1.8.2 Mahala pa Utafiti ..... 18

1.8.3 Sampuli Lengwa .......... 18

1.8.4 Ukusanyaji wa Data .......... 19

1.8.5 Uchanganuzi wa Data .......... 20

1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo .......... 20

1.9 Hitimisho .......... 21

**SURA YA PILI .......... 22**

**MAUDHUI YA MABADILIKO NA UKUAJI WA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LANGU* (2014) NA *DUNIA MASHAKA MAKUU* (2015) .......... 22**

2.0 Utangulizi .......... 22

2.1Muhtasari wa riwaya ya *Chozi Langu* ( Mogambi, 2014) .......... 22

2.2 Muhtasari wa riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (Omar, 2015) .......... 25

2.3 Dhana ya Mabadiliko .......... 28

2.4 Dhana ya Ukuaji .......... 29

2.5 Mabadiliko Miongoni mwa Vijana wa Kike na wa Kiume katika Riwaya teule .......... 30

2.5.1 Mabadiliko ya Hali ya Afya .......... 30

2.5.2 Mabadiliko ya Hali ya Maisha .......... 33

2.5.3 Mabadiliko ya Tabia .......... 37

2.5.4 Mabadiliko ya Hisia .......... 43

2.6 Ukuaji Miongoni mwa Vijana wa Kike na wa Kiume Katika Riwaya teule .......... 47

2.6.1 Ukuaji wa Kiakili .......... 47

2.6.2 Ukuaji wa Kimaadili .......... 52

2.6.3 Ukuaji wa Kijamii .......... 56

2.6.4 Ukuaji wa Kihisia .......... 59

2.7 Hitimisho .......... 63

**SURA YA TATU ..... 64**

**CHANGAMOTO WANAZOPITIA VIJANA KATIKA JAMII NA SULUHU ..... 64**

**ZAKE ..... 64**

3.0 Utangulizi ..... 64

3.1 Changamoto Wanazopitia Vijana wa Kike na wa Kiume katika Riwaya teule ..... 66

3.1.1 Umaskini ..... 66

3.1.2 Ukosefu wa Malezi bora ..... 70

3.1.3 Ukosefu wa Elimu bora ..... 73

3.1.4 Uhusiano wa Kimapenzi ..... 77

3.1.5 Ukosefu wa Usalama ..... 81

3.1.6 Msongo wa Mawazo ..... 85

3.1.7 Kubaguliwa Kiuana ..... 88

3.1.8 Mimba za Ujanani ..... 90

3.1.9 Dhuluma ..... 93

3.1.10 Matumizi ya Mihadarati ..... 97

3.1.11 Vifungo vya Jela na Vizuizi ..... 100

3.2 Suluhu kwa Changamoto Zinazowakumba Vijana Katika *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ..... 102

3.2.1 Umaskini ..... 102

3.2.2 Ukosefu wa malezi bora ..... 103

3.2.3 Ukosefu wa Elimu bora ..... 105

3.2.4 Uhusiano wa Kimapenzi ..... 107

3.2.5 Ukosefu wa usalama ..... 107

3.2.6 Msongo wa Mawazo ..... 108

3.2.7 Kubaguliwa Kiuana ..... 109

3.2.8 Mimba za Ujanani ........ 110

3.2.9 Dhuluma ........ 111

3.2.10 Matumizi ya Mihadarati ........ 113

3.2.11 Vifungo vya Jela na Vizuizi ........ 114

3.4 Hitimisho ........ 115

**SURA YA NNE ........ 116**

**MAMBO YANAYOCHANGIA MAENDELEO YA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LANGU* (2014) NA *DUNIA MASHAKA MAKUU* (2015) ........ 116**

4.0 Utangulizi ........ 116

4.1 Elimu ........ 116

4.2 Jitihada ........ 119

4.3 Ushauri Nasaha ........ 120

4.4 Ufadhili kwa Vijana ........ 125

4. 5 Dini ........ 127

4.6 Malezi ........ 130

4.7 Vyombo vya Habari ........ 135

4.8 Ukuzaji Vipawa ........ 137

4.9 Sheria ........ 138

4.10 Hitimisho ........ 140

**SURA YA TANO ........ 142**

**MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ........ 142**

5.0 Utangulizi ........ 142

5.1 Muhtasari wa Utafiti ........ 142

5.2 Matokeo ya Utafiti ........ 145

5.3 Changamoto za Utafiti ........ 155

5.4 Mchango wa Utafiti ........................................................................................ 155

5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ................................................................... 156

**MAREJELEO ........................................................................................................ 158**

# SURA YA KWANZA

## 1.0 Usuli wa Mada

Fasihi ni sanaa ya lugha ambayo wasanii hutumia kuwasilisha ujumbe kwa msomaji au jamii iliyonuiwa. (Ngure, 2003). Njogu na Chimerah (1999), wanasema ya kwamba fasihi ina jukumu la kuelimisha na kustarehesha. Uelimishaji wa fasihi unatokana na masimulizi yanayofungamana na tajriba halisi wala si maelezo ya kidhahania tu. Hivyo basi njia moja ya kufaulisha kazi ya fasihi ni kuteua maudhui ya mguso kwa jamii ambayo yana uhusiano mkubwa baina ya sanaa na matukio ya jamii. Maudhui ya fasihi huchochewa na hali halisi. Kwa mujibu wa King'ei na Kisovi (2010), mwanafasihi huweza kushughulikia maudhui ambayo ni muhimu kutokana na hali halisi katika jamii anamoishi.

Wamitila (2003), anaeleza kuwa kuna fasihi ya watoto, vijana na ya watu wazima. Kwa mujibu wa Crowe (1998) fasihi ya vijana ni fasihi ambayo imeandikwa kwa ajili ya vijana, na imejikita zaidi kwa masuala yanayowalenga vijana baleghe. Anasema kuwa maudhui na ploti ya hadithi ya vijana huzungumzia changamoto wanazopitia vijana na kwa wakati mwingine hurejelewa kama riwaya tatizo. Hata hivyo, anakiri kuwa ni vigumu kuweka mipaka dhahiri kati ya fasihi ya watoto, vijana na ya watu wazima. Hii ni kwa sababu muundo na matini hufanana katika fasihi zote na pia wahusika katika fasihi ya watoto na vijana huweza kuwa wahusika wazima. Anasema kuwa fasihi ya watoto na vijana hutumiwa kuufikisha ujumbe kwa hadhira iliyo chini ya miaka 18.

Naye Wamitila (2003) anaeleza kuwa fasihi ya watoto ni fasihi inayoandikwa kwa ajili ya watoto ilhali ya watu wazima inatumiwa kuufikisha ujumbe kwa watu wenye umri wa zaidi ya miaka 10.

Kulingana na Kaui (2008), wahusika katika fasihi wanaweza kuainishwa kijinsia na kiumri. Uainishaji huu unatokana na hali ilivyo katika jamii. Katika kigezo cha umri makundi matatu makuu hujitokeza; watoto, vijana na watu wazima. Jamii hukadiria ujana kwa vipimo mbalimbali. Kulingana na katiba ya Kenya (2010), kijana ni binadamu wa kiume au wa kike aliye na umri wa miaka 18 na 35. Young Adult Library Association (YALISA) (2011), wanaeleza kuwa kijana mdogo ni mtu mwenye umri wa miaka 12 mpaka 18.

Waandishi tofauti wamekuwa wakisawiri nafasi ya vijana katika kazi zao. Aidha, wameonyesha uozo na ukosefu wa maadili miongoni mwa vijana kwa ujumla. Katika riwaya teule, mtafiti amechunguza jinsi waandishi wamewapa wahusika vijana baleghe nafasi muhimu ya kuendeleza maudhui ya mabadiliko na ukuaji katika jamii husika. Vilevile, amechunguza mambo mbalimbali yanayochangia maendeleo ya wahusika vijana. Kama anavyosema Cherry (2017), katika kipindi hiki cha kubaleghe, vijana wanahitaji mwelekeo bora maishani kwani hukumbwa na changamoto si haba. Dhana ya mabadiliko na ukuaji ina maana pana. Kimsingi, mabadiliko huweza kuwa ya tabia, hali na afya. Mabadiliko ya tabia ya vijana huweza kuwa chanya au hasi. Ukuaji huweza kutokea katika maeneo yafuatayo; kihisia, kijamii, kiakili na kimaadili na hutarajiwa kwenda sambamba na ukuaji wa kimwili. Kijana anayechagua kufanya lililo sahihi badala ya lisilo sahihi katika

jamii atakuwa amekua kimaadili. (McLeod, 2013). Hivyo basi, maudhui ya mabadiliko na ukuaji yanachangiana na kukamilishana. Mabadiliko na ukuaji huweza kuchochewa na masuala kama vile malezi, umaskini, elimu na mengineyo.

### 1.1 Suala la Utafiti

Azimio kuu la utafiti huu ni kuchunguza maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika Riwaya za *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Cherry (2017) anasema kuwa wakati wa kubaleghe, mabadiliko mengi sana hutokea na huweza kuathiri ukuaji wa vijana. Vilevile, vijana hukumbwa na changamoto si haba na wanahitaji mwongozo bora maishani. Hivyo basi chanzo cha matatizo haya sharti kichunguzwe ili suluhisho lipatikane. Lengo kuu la utafiti huu hivyo basi ni kuonyesha jinsi waandishi wa riwaya teule wanavyobainisha mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe. Waandishi wa riwaya teule wameonyesha kuwa mabadiliko na ukuaji miongoni mwa vijana baleghe hutokana na changamoto zinazowakumba. Hivyo basi, wameonyesha jinsi vijana wanaweza kusuluhisha changamoto zinazowakumba ili waepukane na athari mbeleni.

Kuna tafiti nyingine ambazo zimeshughulikia masuala ya vijana. Kwa mfano; Wafula (1999), Kaui (2008), Kibet (2006), Nyamemba (2015) na Kihara (2016). Wamezungumzia nafasi ya vijana katika jamii. Pia, wameangazia jinsi waandishi walivyosawiri changamoto zinazowakumba vijana. Hata hivyo, tafiti zao huepuka kutaja mabadiliko na ukuaji wa vijana. Ni kutokana na kutochunguza kikamilifu suala la mabadiliko na ukuaji wa vijana ndipo utafiti huu unapata fursa kuonyesha

nafasi ya fasihi katika kuleta mabadiliko kwa kuangazia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya teule.

### 1.2 Malengo ya Utafiti

1. Kubainisha aina ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya teule.

2. Kutambua changamoto wanazopitia vijana na suluhu zake.

3. Kutathmini mambo yanayochangia maendeleo ya wahusika vijana.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

1. Je, mabadiliko na ukuaji wa vijana umebainika vipi katika riwaya teule?

2. Ni changamoto zipi wanazopitia vijana na zinasuluhishwa vipi?

3.Ni mambo yapi yanayochangia maendeleo ya wahusika vijana?

### 1.4 Sababu za Kuchagua Mada

Kwa mujibu wa Awiti na Scott (2016), idadi ya vijana ni asilimia kubwa sana katika jamii. Hivyo basi, vijana ndio uti wa mgongo wa jamii. Bila vijana hatuna viongozi wa mustakabali. Hata hivyo, vijana hukumbwa na matatizo mengi sana. Kwa hivyo, nafasi ya fasihi katika kuleta mabadiliko na ukuaji miongoni mwa vijana baleghe inadhihirishwa kupitia mada hii.

Aidha, masuala machache sana yameshughulikiwa kuhusu kikundi hiki cha vijana wanaobaleghe katika utanzu wa riwaya. Wafula (1999), Kaui (2008) na wengine wameangazia vijana kwa ujumla na wameegemea zaidi utanzu wa tamthilia. Wameangalia jinsi vijana wanavyoikomboa nchi kwa kupigania haki zao, vijana

wanaobadilisha mitazamo ya wanajamii kuhusu masuala kama vile utamaduni. Vilevile, kuna wale ambao wamechunguza vijana wa kike ilhali wengine wamechunguza vijana wa kiume. Hata hivyo, hawajajikita kwa maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe. Kama anavyoeleza Cherry (2017), wakati wa kubaleghe, mabadiliko mengi sana hutokea na huweza kuathiri ukuaji wao. Hivyo basi, vijana wanahitaji mwongozo bora maishani. Kwa hivyo, ni muhimu sana kuchunguza mabadiliko yanayotokea miongoni mwa vijana ili kufahamu chanzo chake.

Sababu nyingine ya kuchagua mada hii ni kuwa, katika jamii ya sasa vijana wamepotoka kimaadili. Baadhi ya vijana huonyesha mabadiliko hasi kama vile kutumia dawa za kulevya wanapokumbwa na changamoto kama vile malezi mabaya. Kama wanavyosema Awiti na Scott (2016) vijana wengi wameathirika zaidi hivi kwamba wengi wao hufa aidha kwa magonjwa mbalimbaliau kutokana na athari za dawa za kulevya. Ili matatizo haya yatatuliwe, ni muhimu kuchunguza chanzo mabadiliko ya tabia ili kupata suluhu.

Utafiti huu ni muhimu kwa waandishi wa kazi za fasihi, wachanganuzi wa masuala ya kijamii na kisiasa kwani wataelewa masuala yanayowaathiri vijana na hivyo kutafuta mbinu mwafaka za kushughulikia masuala hayo. Aidha, vijana baleghe watapata njia mwafaka ya kusuluhisha matatizo yanayowakumba.

### 1.5 Upeo na Mipaka

Utafiti huu umeshughulikia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika *Chozi Langu* (Mogambi, 2014) na *Dunia Mashaka Makuu* ( Omar, 2015). Utafiti

huu umetilia maanani changamoto wanazopitia vijana baleghe katika jamii na suluhu na mambo yanayochangia maendeleo yao.

Katika utafiti huu, vijana wanaobaleghe waliangaziwa, yaani kuanzia umri wa 10 mpaka 19. Wahusika vijana ambao ni wahusika wakuu walitumiwa kuonyesha aina mbalimbali ya mabadiliko na ukuaji wa vijana. Kulingana na maelezo ya waandishi husika, vijana hawa wanapatikana katika umri huu.

Vitabu *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015), vilichaguliwa kimakusudi kwa sababu vinazungumzia masuala yanayowaathiri vijana baleghe na vijana ndio wahusika wakuu. Kwa hivyo, vina data ya kumfaa mtafiti. Pia, wahusika wakuu katika kila riwaya teule ni wa kike na wa kiume. Hivyo basi, kiwakilishi mwafaka cha jamii.

**1.6 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada**

Kuna baadhi ya wahakiki ambao wameshughulikia masuala yanayowahusu vijana katika tanzu mbalimbali za fasihi. Kwa mfano, kuna wale walioutazama usawiri wa vijana katika tamthilia na riwaya za Kiswahili. Wengine wamewachambua wahusika wa kike kwa jumla wakiwemo vijana wa kike katika fasihi ya Kiswahili kwa kurejelea ushairi, tamthilia na riwaya.

Wafula (1999) amehakiki Tamthilia ya *Wakati Ukuta* (1971) akiwa na lengo la kubainisha jinsi suala la mvutano wa kitamaduni linavyosawiriwa. Kulingana na utafiti huu, mtunzi alifanikiwa kudhihirisha namna mabadiliko ya wakati yanalazimisha mabadiliko ya mtazamo wa watu juu ya maisha. Aidha, amefaulu kuonyesha mgongano wa fikra, mawazo na wa utamaduni baina ya vijana na

wazee. Pia amegundua ya kwamba, vijana wanawakilisha utamaduni mpya wenye athari za kizungu na wazee bado wanashikilia utamaduni wao.

Jambo hili linakuwa chanzo cha mgogoro kati ya wazazi na vijana. Vilevile, katika *Uasi* (1980), Wafula (1999) anaonyesha uasi wa vijana dhidi ya desturi kongwe ambazo zimepitwa na wakati kama vile kuwaoza wasichana wabichi kwa wazee matajiri wanaopaswa kuwa mabinti zao. Uasi huu unasababisha mgogoro kati ya vijana na wazee. Kulingana na Wafula, Hussein amefaulu kuonyesha kuwa utamaduni wa kizungu unachangia utovu wa tabia miongoni mwa vijana waliopata elimu ya kigeni. Hivyo basi, elimu ya kigeni ni mojawapo ya mambo yanayoleta mabadiliko ya kitabia miongoni mwa vijana. Utafiti wake umelenga suala la mvutano wa kitamaduni baina ya wahusika vijana na wazee katika utanzu wa tamthilia. Mtafiti ameshughulikia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa wahusika vijana katika utanzu wa riwaya. Vilevile, ameonyesha jinsi elimu na utamaduni wa kigeni unavyochochea mabadiliko ya tabia na mawazo ya vijana. Hata hivyo, hajaangazia masuala mengine kama malezi, umaskini, sheria na mengineyo ambayo huchangia mabadiliko miongoni mwa vijana. Utafiti huu umeliziba pengo hilo kwa kuangazia masuala hayo kwa kina. Pia, mambo yanayochangia maendeleo ya vijana yameangaziwa katika utafiti huu, jambo ambalo hakulititilia maanani. Utafiti wake una ukuruba na huu kwani unazungumzia baadhi ya mambo yanayochangia mabadiliko ya tabia miongoni mwa wahusika wakiwemo vijana, kwa hivyo ulikuwa wa manufaa ikizingatiwa kuwa unazungumzia baadhi ya masuala yanayowakumba vijana.

Kibutu (2013), aliangazia maudhui na mitindo ya lugha inayotumiwa kuwasilisha mafunzo ya kukuza vijana katika misingi ya kiuana katika Dhehebu la P.C.E.A, akiwa na lengo la kuonyesha umuhimu wa dini katika kufunza maadili. Kwa kutumia nadharia ya Semeotiki, Kibutu amegundua ya kwamba, wawasilishaji walitumia tamathali za usemi ikiwa ni pamoja na misemo, methali na tashibihi kwa lengo la kufunza maadili na kueleza uana kulingana na jamii za kiafrika. Pia, lugha teule ilitumiwa kulingana na mada. Katika utafiti wake, ameeleza kuwa, baada ya ukoloni, Waafrika waliasi utamaduni wao, mwingiliano wa kijamii ulipungua na mafunzo kwa vijana yakapungua.

Kibutu amejikita katika dini kama asasi ya kutolea mafunzo kwa vijana na kuwakuza. Mtafiti ameangazia dini pamoja na asasi nyingine kama vile elimu, sheria na nyinginezo ambazo huchangia maendeleo ya vijana. Utafiti huu umelenga kutambua changamoto mbalimbali wanazopitia vijana katika jamii, jambo ambalo Kibutu hajalishughulikia. Utafiti wake uliupa msingi utafiti huu kwa kueleza mambo yanayochangia mabadiliko na maendeleo ya vijana.

Katika usawiri wa wahusika vijana, kuna baadhi ya wahakiki ambao wameonyesha jinsi vijana walivyosawiriwa katika tanzu mbalimbali za fasihi. Kwa mfano katika tamthilia za Kiswahili, Kaui (2008) amechunguza taswira mbalimbali za vijana katika Tamthilia za *Wakati Ukuta* (1971), *Uasi* (1980), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000) na *Pango* (2003) na jinsi zinavyoakisi mabadiliko katika jamii zinazohusika. Amechunguza namna wahusika vijana wamekuwa wakisawiriwa katika mpito wa wakati. Kaui amegundua ya kwamba, elimu na mitindo ya kigeni

ni mamlaka waliyoipata vijana kutoka kwa ustaarabu wa wakoloni. Ameonyesha kuwa, vijana wana uwezo wa kujipa mamlaka na kuyatumia sawa na wazee katika jamii. Hata hivyo, njia za kufanya hivyo ni tofauti na za wazee. Suala hili linazua mgongano kati ya wazee na vijana.

Kauli ya Kaui inaungwa mkono na Kibet (2016) ambaye ameangazia usawiri wa vijana katika tamthilia ya *Mbaya wetu.* (2015). Ametathimini iwapo vijana wenye elimu na wasio na elimu ni wa kimabadiliko, na katika matokeo yake amebaini kuwa elimu iliwapa vijana uwezo na mamlaka zaidi ya kupambana na mila na tamaduni zao. Watafiti hawa wameafikiana kuwa vijana wamesawiriwa kama waasi dhidi ya mila na tamaduni za Kiafrika na mabadiliko yaliyoletwa na masomo yaliwapa uwezo zaidi kuweza kupambana na mila kandamizi zinazotokana na tamaduni zao. Utafiti huu umezungumzia kwa kina masuala mengine ikiwemo elimu yanayochangia maendeleo ya vijana. Hivyo basi, utafiti wao umechangia sana katika kuongoza utafiti huu kwani wamezungumzia elimu kama suala linaloleta mabadiliko miongoni mwa vijana. Hata hivyo, Kaui (2008) na Kibet (2016) hawajaangazia kwa kina changamoto zinazowakumba vijana katika jamii. Pia, utafiti wao unatofautiana na huu kwa kuwa wameangazia usawiri wa vijana kwa jumla katika utanzu wa tamthilia na hawajachunguza kwa kina mambo yanayochangia mabadiliko ya tabia ya vijana wanapokua. Huu umebainisha changamoto wanazopitia vijana na masuala mbalimbali ambayo ni chanzo cha mabadiliko ya tabia ya vijana baleghe katika utanzu wa riwaya. Tofauti nyingine ni kwamba, Kaui (2008) ametumia Nadharia ya Ki- faucoult ilhali mtafiti ametumia Nadharia ya Uhalisia na ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii.

Kwa mujibu wa Kihara (2016), amechunguza nafasi ya vijana katika *Pendo la Karaha* (2014) na *Kovu Moyoni* (2014) kwa kutumia nadharia ya Uhalisia Hakiki. Matokeo ni kwamba, vijana wamepewa nafasi chanya na hasi katika jamii. Kama anavyoeleza Kihara (2016), katika riwaya za vijana wamesawiriwa kama watovu wa nidhamu na waasi dhidi ya utamaduni. Hii ndiyo changamoto kubwa zaidi inayowakumba vijana. Hata hivyo, mwandishi ameweza kuwakweza vijana kwa nafasi chanya kama vile kujikomboa kiuchumi. Hata hivyo, Kihara (2016) hajabainisha suluhu kwa changamoto zinazowakumba vijana na mambo yanayochangia maendeleo ya vijana katika jamii. Utafiti huu ulikuwa faafu kwa kuliziba pengo hilo. Utafiti wa Kihara (2016) ulimfaidi mtafiti kwani ameshughulikia baadhi ya changamoto zinazowakumbavijana katika jamii.

Nyamemba (2015) na Mureithi (2016), wamechunguza maswala ya vijana na jinsi yanavyoshughulikiwa na waandishi mbalimbali wakiwa na lengo la kubainisha changamoto za vijana na jinsi zinavyosawiriwa na waandishi tofauti. Kwa kutumia nadharia ya Uhalisia Nyamemba (2015) na Mureithi (2016) wamegundua ya kwamba vijana wanakumbwa na changamoto sawa katika jamii tofauti. Kwa mujibu wa Nyamemba (2015) waandishi wote katika *Tunu ya Ushairi* (2015) wana mwelekeo sawa kuhusu vijana. Mureithi vilevile kwa kutumia riwaya ya Upotevu (2005) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (2007) ameonyesha kuwa changamoto zinazowakumba vijana zinafanana. Hata hivyo, Nyamemba (2015) na Mureithi (2016) wamemwacha kijana katika hali ya kukata tamaa kwa kutotoa suluhu kwa changamoto zinazomkumba. Vilevile, hawajaeleza aina ya mabadiliko na ukuaji miongoni mwa vijana baleghe. Utafiti huu ulikuwa mwafaka katika kubainisha

jinsi vijana wanaonyesha mabadiliko chanya licha ya kukumbwana changamoto mbalimbali. Pia, ulibainisha mambo yanayowasaidia vijana kujiendeleza katika jamii.

Katika usawiri wa wahusika wa kike, kuna kazi nyingi ambazo zimeangalia nafasi ya mwanamke akiwemo kijana wa kike katika jamii. Kimani (2003), kwa kutumia Nadharia ya Mtazamo-kike, amechunguza maudhui ya dhuluma dhidi ya wanawake katika Fasihi ya Kiswahili. Kwa kuangazia suala la wanawake, ameweza kumchunguza pia kijana wa kike kwa lengo la kubainisha na kuainisha hali tofauti za dhuluma dhidi ya wanawake na athari zake. Anatoa kauli kuwa dhuluma hizi zinawakabili kwa sababu ya maumbile yao na kwamba wanaume wanawachukulia wanawake kama viumbe duni katika jamii.

Momanyi (1998), amehakiki Ushairi wa Kiswahili na ameangalia usawiri wa mwanamke Muislamu katika jamii ya Waswahili na amegundua ya kwamba, utamaduni wa Waswahili Waislamu, unambagua na kumdunisha mwanamke. Mwanamke amesawiriwa kama kifaa cha utumishi kama vile kidau, konde na tunda. Utafiti wa Momanyi (1998) na Kimani(2003) una ukuruba na huu kwa kuwa umemwangazia mwanamke akiwemo kijana wa kike kwa kuonyesha matatizo yanayomkumba mwanamke kwa mfano kubaguliwa, kutukanwa na kutishwa. Hivyo basi, ulikuwa wa manufaa kwa mtafiti kwani ameangazia masuala hayo yanayowakumba vijana wa kike. Tofauti ni kuwa Momanyi (1998) ametumia Nadharia Uchanganuzi-Nafsia na amejifunga zaidi kumhakiki mwanamke Muislamu na kujikita katika utanzu wa kishairi. Utafiti huu umetumia Nadharia ya

Uhalisia na ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii na umeangazia kijana wa kike na wa kiume katika jamii mbalimbali katika utanzu wa riwaya. Pia, Momanyi (1998) na Kimani (2003) wameangazia zaidi usawiri wa mwanamke akiwemo kijana wa kike na hawajaelekea kubainisha masuala mbalimbali yanayochangia maendeleo ya kijana wa kike. Utafiti huu umeshughulikia mambo yanayochangia mabadiliko na maendeleo ya vijana kwa kina. Vilevile, wamechunguza wahusika wa kike kwa ujumla kwa kutumia  ilhali huu umeangazia kijana wa kike na wa kiume.

## 1.7 Misingi ya Nadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia mbili; nadharia ya Uhalisia na nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii. Nadharia mbili zimetumiwa kwa sababu mabadiliko na ukuaji miongoni mwa vijana wanaobaleghe hutokea kutokana na sababu mbalimbali na vijana hukumbwa na changamoto nyingi sana. Hivyo basi, mabadiliko na changamoto hizo zinafaa kuangaliwa kwa mikabala mbalimbali. nadharia ya uhalisia iliteuliwa kutokana na sababu kuwa fasihi ya vijana inafaa iambatane na matukio halisi kama yanavyotokea katika jamii na wahusika ambao vijana wanaweza kujihusisha nayo. Kwa upande wapili, Nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii (Erickson na Erickson, 1998) ni nadharia ya ukuaji ambayo inafaa kuelezea hali mbalimbali zinazochangia katika mabadiliko na ukuaji wa kijana. Erickson na Erickson (1998) wanasema kwamba utangamano na mtagusano wa kijamii una athari kwa maisha ya kijana na ni muhimu sana katika ukuaji wake. Kwa hivyo, mtafiti ameazimia kupata mchango kutokana na nadharia ya Kisaikolojia kwa sababu kuna baadhi ya wahusika vijana katika riwaya teule wanaodhihirisha mabadiliko kutokana na utangamano wa kijamii. Nadharia

nyingine ambayo ingefaa kutumiwa badala ya nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ni nadharia ya Kiutambuzi ya Piaget (1978) ambayo inasisitiza ukuaji wa kiakili wa vijana. Hata hivyo, nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ilimfaa sana mtafiti kwani mihimili yake inatosheleza malengo ya utafiti.

Mtafiti ametumia nadharia ya Uhalisia kueleza hali halisi, ilhali nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii imeelezea hali mbalimbali zinazochangia mabadiliko na ukuaji wa vijana. Vijana baleghe hupitia mabadiliko ya hisia na fikra ambayo huweza kuleta migogoro baina yao na wazazi. Mabadiliko ya kimwili hutarajiwa kwenda sambamba na ukuaji. Hivyo basi, suala la mabadiliko na ukuaji ni la kijamii na Kisaikolojia kwani jamii ina nafasi ya kuwaongoza vijana. Aidha, mhusika kijana hawezi kusawiriwa katika umri huu wa kubaleghe bila kumhusisha na hali halisi ya jamii. Vilevile, ni muhimu atazamwe kama mtu binafsi, mwenye hisia, fikra na mwelekeo fulani.

### 1.7.1 Nadharia ya Uhalisia

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) uhalisia ni kazi ya kifasihi inayowasilisha ulimwengu wa maisha ya kijamii ambako wahusika huwasilisha hali halisi waliyomo. Kazi za kihalisia zinatarajiwa kuonyesha hali halisi ya maisha katika jamii inayohusika. Uchunguzi wa utanzu wa riwaya unafaa uambatane na matukio halisi kwa kiasi kikubwa. Wanauhalisia huwasawiri wahusika kama wale wanaopatikana katika ulimwengu halisi, mandhari na mazingira halisi.

George Lukacs mfuasi wa Karl Marx kutoka Hungary ni mmoja wa wataalamu wanaohusishwa na nadharia ya Uhalisia. George Lukacs amekuwa na athari kubwa

sana kutokana na msimamo wake kuhusu uhalisia. Anauona uhalisia kama lengo kuu la mwandishi na anaamini kuwa mwandishi anasukumwa na nia ya kusawiri uhalisi katika ukamilifu wake katika wakati fulani maalum. Katika mtazamo huu wa uhalisia, yanayoshughulikiwa yawe yanatokea au kutendeka katika ulimwengu halisi. Msanii lazima aelewe jamii yake kama kitu kinachobadilika. Yaani, msanii anafaa kuwa kurunzi ya jamii. Msanii pia anafaa kutumia kipawa chake kutoa taswira ya mazingira yanayoaminika. Hivyo basi, mchango mkuu wa nadharia hii ni kuweka bayana hali ya maisha jinsi yalivyo.

Kwa mujibu wa Wafula na Njogu (2007), uhalisia ulianza kudhihirika kuanzia mwaka wa1850 nyakati za mwandishi wa Kifaransa Gustav Flaubert ambaye alikuwa mmoja wa waasisi wa uhalisia. Waandishi na wahakiki wengi waliamini kwamba dhima ya mwandishi ni kuonyesha ukweli jinsi ulivyo yaani kuonyesha picha za mazingira ambamo jamii inapatikana.

Wanauhalisia waliamini ya kuwa malengo ya mwandishi kwa jamii ni kuwarudisha watu katika ulimwengu wao wa kawaida. Jukumu la mwandishi ni kudhihirisha ukweli. Hivyo basi anafaa kuwachora wahusika na mazingira yanayokubalika katika jamii. Lengo la mtafiti la kutumia nadharia hii ilikuwa ni kuihakiki kazi ya fasihi ili kuona ni kwa kiasi gani anadhihirisha uhalisia na umuhimu wake katika fasihi ya Kiswahili. Fasihi ya vijana huhusu matukio halisi yanayoathiri vijana katika jamii. Hivyo basi, mhakiki anafaa kutazama jinsi ukweli ulivyojidhihirisha katika utunzi wa kuchora hali halisi. Kulingana na Ntarangwi (2004), mhalisia anafaa kuweka wanajamii katika ulimwengu wao wa kawaida. Waandishi wa fasihi

ya vijana huonyesha vile vijana hukumbwa na changamoto mbalimbali na jinsi wanavyojaribu kutatua matatizo hayo.

Mihimili ya nadharia ya Uhalisia ni ifuatayo;

1. Fasihi husawiri uhalisia wa maisha.

   Kazi nyingi katika misingi ya kihalisia huangazia maisha katika ngazi zote kama vile siasa, uchumi, utamaduni na jamii. Mhimili huu ulitumika katika kutambua changamoto wanazopitia vijana katika riwaya teule na suluhu zake.
2. Mandhari, matukio na mazingira yaonyeshe kila kitu kama kilivyo. Maudhui na matukio yalingane na yale ya jamii inayorejelewa. Mhimili huu ulitumika kubainisha maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana.
3. Wahusika katika kazi ya fasihi huwa vielelezo halisi vya binadamu wa kawaida. Mhimili huu ulitumika kuonyesha uhalisia wa wahusika vijana na jinsi wanavyoendeleza maudhui ya mabadiliko na ukuaji.

### 1.7.2 Nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ya Erickson.

Nadharia hii iliasisiwa na Erickson (1950) na ikaendelezwa baadaye kwa kazi yake katika Erickson na Erickson (1998). Kwa mujibu wa Erickson na Erickson (1998), ukuaji wa mwanadamu hutokea katika hatua mbalimbali. Wanasisitiza athari ya utangamano na uhusiano wa kijamii ambao ni muhimu sana katika ukuaji wa binadamu. Kulingana na Dacey na John (2009), mtazamo wa Erikson (1950) kuhusu ukuaji wa mtu ulitokana na uchunguzi wake wa kina wa jamii mbalimbali zilizokuwa na tamaduni mbalimbali. Erickson alifanya uchunguzi kwaWajerumani, Wahindi na vijana walioishi Marekani. Pia, mawazo Erickson (1950) yanatokana

na uchunguzi wa kina wa mashujaa wa kihistoria kama Martin Luther na Mahatma Gadhi.

Dacey na John (2009) wanasema kuwa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii inaendelea kutumika katika vizazi vya sasa na imesalia kuwa muhimu sana katika ukuaji wa binadamu. Nadharia hii huangazia ukuaji wa kijamii wa mtoto unaotokana na mtagusano wa nguvu za kimaumbile na utamaduni, yaani mtoto anahisi kufanya hivi ilhali utamaduni unamhitaji afanye vingine.

Kwa mujibu wa Erickson na Erickson (1998) binadamu hupitia hatua nane muhimu zinazojumuisha migogoro ya kisaikolojia na ya kijamii. Kadri akuavyo, hatua za ukuaji wa kijamii huibuliwa. Lazima asuluhishe migogoro katika kila hatua kabla ya kusonga kwa nyingine. Iwapo atasuluhisha mgogoro ipasavyo, atajenga mbinu zinazohitajika kwa ukuaji wa nafsi. Katika hatua hii, vijana wanafaa kupewa mwongozo unaofaa. Iwapo hatua imeshughulikiwa ipasavyo, mtu atahisi kuwa anaelewa mambo vizuri na hivyo atajiona kuwa na umuhimu katika jamii.

Kwa madhumuni ya utafiti huu mtafiti ameangazia hatua muhimu ambayo imejikita katika umri huu wa kubaleghe, yaani hatua ya utambulisho dhidi ya usambazaji majukumu. Hatua hii huanza kati ya umri wa miaka 11 mpaka 18.

Hatua hii huwa muhimu sana katika kukuza nafsi na utambuzi na huendelea hadi utu uzima. Katika umri huu wa kubaleghe vijana hujaribu kujitegemea na kukuza nafsi. Vijana wanakua na kujitambua bila kutegemea wazazi. Cherry (2017) anasema kuwa katika hatua hii, vijana wanaanza kujihusisha na kikundi fulani ambacho kina mienendo sawia na wao. Wale wanaopewa motisha kutokana na

uvumbuzi wao watakuwa na ujasiri na watakuza nafsi na pia watajitegemea. Wakati huu kijana hujitambua kuwa yeye ni mwanamume au mwanamke na majukumu yake katika jamii. Yule ambaye hapewi msingi bora huchanganyikiwa na hukosa kuelewa jukumu lake katika jamii.

Utambulisho nafsi hurejelea itikadi, imani na maadili ambayo humwongoza mtu. McLeod (2013), anakubaliana na mawazo ya Erickson na Erickson ( 1998) anaposema kuwa, kufaulu katika hatua hii humfanya kijana awe na uwezo wa kuishi kulingana na matakwa ya jamii na kukubali kuishi na wengine pasi na kuangalia tofauti zao. Katika hatua hii, kijana huwa na utambulisho ambao anaupata kutokana na mtagusano na jamii. Utambulisho huhusishwa na ukuaji wa ujuzi. Erickson anasisitiza kuwa utambulisho wa kijana hubadilika kulingana na ujuzi mpya au utangamano na jamii.

Anapokuwa na ujuzi mpya, changamoto zinatokea zinazomkuza au kutomkomaza kiakili. Hisia za binadamu kuhusu utambulisho nafsi hujengwa kutokana na tajiriba na utangamano na wengine na huongoza vitendo vyake, itikadi na tabia anapoendelea kukua. Mahitaji yake ya kibinafsi hukinzana na ya jamii na hivyo huibua mgogoro. Mgogoro huzuka kwani wanaona wanatawaliwa na wazazi. Kama anavyosema Kroger (2004), kutokana na utangamano na jamii, kijana hukuza nafsi. Jamii humpa mawaidha ya kumwelekeza maishani.

Mihimili ya nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ni ifuatayo:

1. Katika hatua ya kujitambulisha, kijana hutaka kujitegemea na kukuza nafsi yake. Wale wanaopewa motisha huwa na ujasiri na hujitegemea. Wale

ambao hawapewi mwongozo unaofaa huchanganyikiwa na hukosa mwelekeo maishani. Mhimili huu umetumika kutathmini mambo yanayochangia maendeleo ya vijana katika jamii.

2. Mahitaji ya kibinafsi hukinzana na ya kijamii kwa hivyo, huibua mgogoro, kwani huona wanatawaliwa na wazazi. Mhimili huu utatumika kuchunguza chanzo cha mabadiliko ya tabia na hisia za vijana na ukuaji wao.

### 1.8 Mbinu za Utafiti

Sehemu hii imegawanywa katika sehemu tatukama ifuatavyo:

#### 1.8.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu ni wa kimaelezo ambao hutegemea maelezo katika uwasilishi na uchanganuzi wake. Data iliyokusanywa kutoka kwa riwaya teule huelezwa kwa kina.

#### 1.8.2 Mahala pa Utafiti

Utafiti huu ulifanywa maktabani katika Chuo Kikuu cha Kenyatta na Chuo Kikuu cha Nairobi. Mtafiti alipata data kwa kusoma kwa upana riwaya teule. Makala na machapisho yaliyoandikwa kuhusu mada kama vile tasnifu na vitabu vinavyoeleza masuala ya vijana vilisomwa.

#### 1.8.3 Sampuli Lengwa

Utafiti huu uliteua sampuli ukitumia mbinu-kusudio. Huu ni uteuzi wa data yenye sifa zinazolenga utafiti. Mbinu-kusudio ilimwezesha mtafiti kuteua riwaya mbili, *Chozi Langu* ( Mogambi, 2014) na *Dunia Mashaka Makuu* ( Omar, 2015). Riwaya hizi ziliteuliwa kwa njia ya maksudi kwa sababu ni miongoni mwa kazi za fasihi

zinazoangazia masuala ya vijana baleghe kwa undani zaidi. Kazi nyingine zinazozungumzia masuala ya vijana baleghe ni *Safari ya Usiku* (Mogambi, 2007), *Pigo La Ujana* (Muthusi, 2013). Hata hivyo, mtafiti alichagua riwaya mbili kwa misingi ifuatayo:

1. Riwaya ambazo wahusika wakuu ni vijana. Wa kike mmoja katika *Chozi Langu (2014).* Wa kike mmoja na wa kiume wawili katika *Dunia Mashaka Makuu (2015),* kwa hivyo ni kiwakilishi bora cha jamii.
2. Wahusika vijana wanapatikana kwa umri lengwa yaani wanaobaleghe, umri wa miaka 10 hadi 19.
3. Hadithi zinazopatikana katika riwaya hizi zinagusia suala la mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe. Isitoshe, riwaya hizi zimeshughulikia masuala mbalimbali yanayochangia maendeleo ya vijana baleghe. Pia, viliandikwa na waandishi kutoka maeneo tofauti.

**1.8.4 Ukusanyaji wa Data**

Data ilikusanywa kwa kusoma kwa kina riwaya teule. Data ya kimsingi ilikuwa maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe, changamoto wanazopitia vijana baleghe na mambo yanayochangia maendeleo ya vijana. Aidha, mtafiti alisoma vitabu vya wataalamu mbalimbali vinavyotaja masuala ya mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe ili kupata uelewa zaidi kuhusu dhana hizo. Pia, alisoma masuala yanayohusu vijana kutoka mtandaoni. Tasnifu zinazoshughulikia masuala ya vijana katika utafiti pia zilisomwa. Mtafiti aliongozwa na malengo ya utafiti katika ukusanyaji wa data. Data imeainishwa kulingana na maudhui ya mabadiliko

na ukuaji wa vijana na malengo ya utafiti. Mtafiti alisoma kwa kuchunguza jinsi masuala hayo yamejadiliwa. Dhana ya vijana na changamoto zinazowakumba vijana zilisomwa kutoka katika vitabu vinavyozungumzia masuala hayo.

### 1.8.5 Uchanganuzi wa Data

Data iliyokusanywa maktabani imechanganuliwa kwa kuipanga katika makundi kwa kuzingatia maswali, malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia ambazo zimeongoza utafiti huu. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti kwa mfano, katika lengo la kwanza mtafiti aliainisha aina ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume. Lengo la pili lilimsaidia mtafiti kutambua changamotowanazopitia vijana wa kike na wa kiume na suluhu zake katika riwaya. Lengo la tatu mtafiti alibainisha mambo yanavyochangia maendeleo ya vijana wa kike na wa kiume.

### 1.8.6 Uwasilishaji wa Matokeo

Matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Kwa kuongozwa na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia teule, mtafiti ametoa mifano mahususi kwa kuzingatia sura mbalimbali. Maelezo haya yalifafanua aina ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume katika riwaya teule. Pia, changamoto wanazopitia vijana wa kike na wa kiume katika jamii na suluhu zake zimebainishwa. Vilevile, mambo yanayochangia maendeleo ya vijana katika riwaya teule yamebainishwa.

### 1.9 Hitimisho

Katika sura ya kwanza, mambo ya kimsingi yameshughulikiwa. Mambo haya ni pamoja na usuli wa mada, suala kuu la utafiti, malengo na maswali ya utafiti. Vilevile, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka na yaliyoandikwa kuhusu mada yamebainishwa. Misingi ya Nadharia ya Uhalisia na ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ya Erickson imejadiliwa na pia mbinu za utafiti. Sura ifuatayo imeshughulikia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya teule.

# SURA YA PILI

## MAUDHUI YA MABADILIKO NA UKUAJI WA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LANGU* (2014) NA *DUNIA MASHAKA MAKUU* (2015)

### 2.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia aina mbalimbali ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume katika riwaya teule. Riwaya za *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015) zinataja aina za mabadiliko miongoni mwa vijana yanayotokana na mambo mbalimbali yakiwemo malezi, ushauri nasaha na mengineyo. Nadharia ya Uhalisia na ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii zimetumika katika kubainisha maudhui haya.

### 2.1 Muhtasari wa riwaya ya *Chozi Langu* ( Mogambi, 2014)

Riwaya hii iliandikwa na Hezron Mogambi. Riwaya inahusu mhusika wa kike kwa jina Mliwa. Familia ya Mliwa ina watu watano; Mliwa ambaye ni kifungua mimba, babake Mliwa anayeitwa Kajogoo, mamake anayeitwa Bonuke na ndugu zake wa kike wawili; Chanda na Chandeka. Maisha ya Mliwa yameangaziwa tangu anapozaliwa, anapoenda shule, anapobaleghe hadi anapohitimu kuwa mwanahabari. Kupitia kwa Mliwa, mwandishi ameangazia masuala yanayomwathiri mwanamke katika jamii. Masuala kama dhuluma, kubaguliwa kiuana, ubakaji, msongo wa mawazo na mapenzi yameangaziwa zaidi. Pia ameangazia matatizo yanayowakumba vijana wa kike hasa kutengwa kutokana na kulelewa na mzazi mmoja. Mliwa anazaliwa katika mazingira magumu ambayo watoto wa kike wanadunishwa na wanaonekana kama mkosi. Matatizo ya Mliwa

yanaanza pindi anapozaliwa. Kuzaliwa kwa Mliwa kulimnyima Kajogoo furaha na utulivu kwani alikuwa anamtarajia mtoto wa kiume. Kulingana na Kajogoo, kupata mtoto wa kwanza wa kike ni kama laana na ni aibu kubwa sana katika jamii. Kwa sababu hiyo Mliwa ananyimwa nafasi ya kwenda shule kwani babake hakuona haja ya kuelimisha aila yao. Imedhihirika kuwa, masaibu ya Mliwa yaliongezeka mamake Bonuke alipojifungua tena watoto wa kike Chanda na Chandeka. Kajogoo akawa na chuki kwa Bonuke, Mliwa na ndugu zake.

Mliwa alishuhudia dhuluma ambazo babake alimfanyia mamake kila siku kwa mfano, kumpiga, kumfokea na kuja nyumbani kila siku akiwa mlevi. Mliwa hakumbuki ni mara ngapi wamelala njaa. Mliwa anajiuliza ni hadi lini mamake ataendelea kuvumilia dhuluma za namna hiyo? Katika umri wa miaka kumi, Mliwa ameyaona mengi na sasa anamshauri mama yake atafute nafasi ya kujiokoa mapema. Bonuke anaamua kuachana na Kajogoo ili awalee binti zake. Maisha ya Mliwa yanachukua mkondo mpya anapopata ufadhili kutoka kwa Wazungu kutoka Marekani waliokuja kwa kanisa lao. Anaendelea na masomo yake katika darasa la nane. Huko shuleni hakuwa na amani kwani wenzake walimcheka kwa kuwa ana umri mkubwa zaidi. Hii ilitokana na sababu kuwa Mliwa alichelewa kuhudhuria masomo wakati wenzake walikuwa wakienda shule. Hata hivyo, aliendelea kutia bidii masomoni.

Matokeo ya mtihani wa kitaifa yalipotangazwa Mliwa alipita na alama za juu zaidi na hivyo akajiunga na shule ya upili ya kutwa ya St. Stephen’s. Shuleni Mliwa alibobea katika kila jambo si masomoni, si michezoni, si katika mijadala. Alikuwa

akitunga mashairi kila Ijumaa na kuyatundika kwa ubao. Vilevile, alipenda sana kuandika makala katika lugha ya Kiswahili na hapo akapewa jina 'Jicho la Shule'. Alipoamua kushiriki katika shindano la utangazaji lililoandaliwa na Redio Kisu, aliibuka mshindi kwa kuchukua nafasi ya kwanza. Wasimamizi wa Redio Kisu wakampa ahadi kuwa wangemfadhili katika masomo yake hadi chuo kikuu. Hata hivyo, alikuwa na wanafunzi ambao walimwonea wivu kutokana na umaarufu wake. Wanafunzi hao walimbandika jina 'Mathee' kutokana na umri wake mkubwa. Zaidi ya hayo, walimsimanga na kumwita mwenye hana asili wala fasili kutokana na kulelewa na mama tu. Matusi haya yalimkosesha Mliwa amani na kila mara alikuwa analia. Trufena na Mawazo wakakawa karibu naye kumshauri kuwa anafaa kuyapuuza maneno ya mahasidi wake. Ushauri huo ukampa nguvu na matumaini tena. Akawa na falsafa kuwa masomo mbele na hakuna atakayembabaisha.

Maisha ya Mliwa yalibadilika mara moja baada ya unyama aliotendewa na Chifu Moegi ambaye pia ni mzee wa kanisa. Mliwa alipokuwa anatoka shuleni usiku baada ya mvua kubwa kunyesha,anadanganywa na Chifu Moegi kwamba angempeleka Mliwa hadi kwao. Chifu Moegi anapata fursa ya kumbaka Mliwa. Mliwa aliathirika kisaikolojia kutokana na ubakaji. Hakuwa anakula wala kulala. Akaanza kutembea mtaani huku akiongea peke yake. Zaidi ya hayo, akaacha kwenda shule. Wanafunzi wenzake pamoja na wanakijiji waliandamana kupigania haki ya Mliwa. Hatimaye ikabainika kuwa Chifu Moegi ndiye mhusika wa unyama huo. Chifu Moegi alichukuliwa hatua kisheria kwa kupewa adhabu ya kifungo cha maisha. Mamake Bonuke akatafuta njia ya kumsaidia Mliwa kutoka kwa washauri

nasaha. Mliwa akapata ushauri nasaha kutoka kwa mama Trufena na alipopata nafuu, alirudi shuleni kuendelea na masomo yake. Hatimaye, Mliwa anafaulu katika mtihani wake wa kidato cha nne na kujiunga katika chuo kikuu kusomea uanahabari. Akahitimu na kuwa mwanahabari maarufu zaidi. Akabadilisha maisha ya mamake kwa kumfungulia duka kubwa la jumla. Vilevile, Mliwa na mama yake wakaanzisha wakfu wa Mliwabo. Jukumu lake kubwa lilikuwa kutoa ushauri nasaha kwa wahanga wa majanga mbalimbali kama vile dhuluma ya kimapenzi. Chanda akahitimu kuwa muuguzi naye Chandeka kuwa mwalimu wa shule ya upili.

### 2.2 Muhtasari wa riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (Omar, 2015)

*Dunia Mashaka Makuu* (2015) ni riwaya iliyoandikwa na Lamin H. Omar. Riwaya hii inahusu vijana wawili; Dunia ambaye ni kijana wa kiume na Yasibu kijana wa kike. Dunia na Yasibu ni wahusika wakuu ambao ni watoto wa Bwana Mashaka na Bi. Nusura. Hii ni riwaya ya kisasa inayotuangazia makosa yanayofanyika nyumbani, shuleni na hata mijini. Inatuonyesha athari ya malezi kwa vijana baleghe. Kwa kiujumla riwaya hii inazungumzia wajibu wa wazazi, walimu na jamii kwa ujumla katika kuwaelekeza vijana. Mwandishi anazungumzia masuala kama malezi, athari za dawa za kulevya, mimba za ujanani, vifungo vya jela na dhuluma.

Kupitia wahusika vijana, mwandishi anaonyesha jinsi wazazi hukosa kuwaelekeza vijana ipasavyo. Vilevile, ameonyesha jinsi vijana hujipata katika hali ngumu wanapokosa kufuata ushauri wa wazazi. Bwana Mashaka ni tajiri ambaye anamiliki

mashamba makubwa na mifugo wengi mno. Anawalea wanawe kwa masharti makali mno. Vitisho na matusi ndiyo iliyokuwa lugha kwa wanawe. Dunia alizaliwa wakati mama yake Bi. Nusura alipigwa dafrao na fahali. Kutokana na tukio hili Bwana Mashaka akashikilia kuwa kuzaliwa kwa Dunia kulibashiri maafa.

Bwana Mashaka anamlaumu Dunia kwa kila kosa ndogo. Dunia anapoteleza kidogo, baba yake anamtusi kuwa Dunia ni mjalaana na kuwa kuzaliwa kwake kulionyesha kuwa angekuwa mtoto wa 'mikosi'. Dunia anapomwomba babake msamaha baada ya kuripotiwa na mwalimu mkuu kuwa hakuwa amefika shuleni kwa siku kadhaa, babake anakataa kumsamehe kabisa na akakataa kumlipia karo ya shule. Mwalimu mkuu anaamua kumlipia Dunia karo ya shule baada ya kuona mabadiliko yake. Dunia anapita mtihani wa darasa la nane lakini anayakataa mashauri ya wazazi wake, walimu na wazee wengine wanaomtaka aendelee na masomo. Anakataa hadharani kuwa hangeendelea na masomo baada ya kushawishiwa na rafikiye Pazia. Ujasiri huo wa kukataa mbele ya hadhara unatokana na madhara ya bangi aliyopewa na rafikiye Pazia.

Yasibu naye anadekezwa sana na baba yake. Bwana Mashaka hakutaka Yasibu afanye kazi yoyote kwa nyumba yao hata kutumwa maji tu. Kazi zote zilifanywa na watumishi wa humo ndani. Bwana Mashaka anamfungia bintiye nyumbani wala hataki atoke nje kama wenzake. Anapofikisha umri wa miaka kumi na mitano, Yasibu anaomba uhuru wa kutembea na kujifanyia mambo. Hata hivyo, Yasibu anautumia uhuru huo vibaya kwa kujiingiza katika mapenzi na Pazia. Yasibu

alikosa heshima kwa wazazi hasa mama yake. Matokeo ya mtihani ya Yasibu yakaanza kudorora. Akaanza kushika mkia darasani.

Hatimaye, ikabainika kuwa Yasibu ana ujauzito na mhusika ni Pazia. Masomo ya Yasibu yakakatizwa baada ya kufukuzwa shuleni. Pazia akaendelea na masomo huku Yasibu akilea. Pazia akamkataa Yasibu kwa kumwambia kuwa yeye Pazia hakuhusika. Babake Yasibu pia akamchukia sana Yasibu na hata akaamua kumfungia chumbani mwake kwani Yasibu alimwaibisha. Matusi ya kila mara kutoka kwa babake yanamfanya Yasibu kutaka kujitia kitanzi lakini anabadilisha mawazo yake baada ya kushauriwa na Mzee Mafusho kupitia kwa wimbo. Hata hivyo, anaamua kutoroka nyumbani na mwanawe Yadhuru.

Dunia pia anatorokea mjini Mwambao ambako anapata matatizo mengi mno; yakiwemo kufungwa jela pasipo na makosa, kukosa chakula, mavazi na makazi. Dunia akajuta sana kuacha masomo yake na kutorokea mjini na hapo akagundua kuwa Pazia alimhadaa. Baada ya kifungo, Dunia na Mpoto wanatia bidii ili wapate mahitaji ya kimsingi. Matatizo ya Dunia yalizidi wakati alifungwa jela kwa mara ya pili kwa kushukiwa mwizi. Baada ya kupitia mateso mengi kule gerezani, Dunia akaamua kurudi nyumbani kuomba msamaha kwa wazazi wake ili aanze maisha upya.

Vilevile, Yasibu anapata taabu mno kule Mwambao. Ikawa vigumu kwake kula, kuvaa na kulala. Akaamua kujiingiza katika mapenzi na Mzee Fadhili. Mzee Fadhili alikuwa tajiri. Alimpa ahadi Yasibu kuwa angemuoa, lakini baada ya kumpa mimba akamfukuza Yasibu kama mbwa. Yasibu alitoka kwa Fadhili akiwa

keshaambukizwa ugonjwa wa Ukimwi. Hakuwa na mtu wa kumsaidia kupata chakula chake na wanawe. Kwa hivyo, akaamua kujiingiza katika ukahaba ili apate mahitaji muhimu. Kabla aende nyumbani kwao kuwaomba wazazi wake msamaha kwa kutoroka nyumbani, anazidiwa na ugonjwa ambao unamuua.

### 2.3 Dhana ya Mabadiliko

Mabadiliko ni hali ya kuwa tofauti na ilivyokuwa mwanzo. (TUKI, 2004). Mabadiliko huweza kutokea katika tabia, hali ya maisha, hisia na afya. Mabadiliko miongoni mwa vijana baleghe huweza kutokea kwa sababu mbalimbali. Kwa mfano mabadiliko ya tabia hutokana na malezi na ushauri anaopewa kijana. Kulingana na Plotnik (1996), mabadiliko yanayotokea wakati wa kubaleghe huwafanya vijana kujitegemea na kujitambua. Vijana wengi huwa na changamoto ya kutoa uamuzi kati ya  kazi ya shule, matumizi ya mihadarati, mapenzi na marafiki wao. Motisha wanayopewa huwajasirisha na hujiona kuwa wana uwezo wa kutekeleza majukumu mbalimbali katika jamii. Wanapokashifiwa kila wakati huweza kujiona duni na hukata tamaa.

Kimsingi, kijana anapokua kuna mabadiliko ya kimwili ambayo hutokea. Zaidi ya mabadiliko ya kimwili, kuna mabadiliko ya tabia na hisia. Katika umri huu kijana hutaka kujitegemea na kukuza nafsi yake na huanza kukabiliana na changamoto mbalimbali. (Cherry, 2017). Cherry anasema kuwa aghalabu kijana huchaganyikiwa na huweza kuwa na hisia mbalimbali. Kamote (2016) anakubaliana na Cherry kuwa wakati wa ujana mabadiliko ya kijamii yanatokea pamoja na mabadiliko ya kimwili. Vijana wengi wanashindwa kuhimili mihemko

vizuri na wakati mwingine kuathiri maendeleo yao kwa ujumla. Hivyo basi ushauri mwafaka unafaa ili wajielewe. McNeely na Blanchard (2009) wanasema kwamba kuyaelewa mabadiliko haya miongoni mwa vijana baleghe na kufahamu nini kinachotokea na kwa nini huwezesha vijana pamoja na watu wazima kufurahia maisha. Katika utafiti huu mtafiti alijikita katika mabadiliko ya tabia, hali ya maisha, afya na hisia za vijana. Mabadiliko wanayozungumzia waandishi wa riwaya teule ni yale yanayotokea katika jamii halisi.

## 2.4 Dhana ya Ukuaji

Ukuaji ni hali ya kuongezeka akili au kuwa na busara. ( McLeod, 2013). Kukua kwa binadamu kimwili kunaambatana na kukua kwake kisaikolojia. Ukuaji huu huandamana na mabadiliko katika hisia na fikra za kijana. Kulingana na McNeely na Blanchard (2009), ukuaji hutokea katika maeneo mbalimbali kwa mfano ukuaji wa kimwili, kiakili, kihisia, kijamii na kimaadili.

Kijana anapokua kimwili inatarajiwa kuwa anakua pia kihisia, kiakili, kijamii na kimaadili. McNeely na Blanchard wanasema kuwa vijana baleghe wanaweza kuonekana kama watu wazima na hata hutaka wachukuliwe kama watu wazima. Hata hivyo, bado wako katika hatua ya ukuaji. Hivyo basi, jinsi wanavyotangamana na jamii huathiri ukuaji wao.

Katika *Chozi Langu* (2014), mwandishi ameeleza ukuaji wa vijana kutokana na mambo mbalimbali kama vile hali ngumu ya maisha na ushauri nasaha. Kulingana na mwandishi, hali ngumu ya maisha humfanya kijana akue kiakili, kitabia na kimaadili. Katika *Chozi Langu* (2014) mwandishi ameonyesha jinsi vijana huweza

kutatua matatizo yao wanapokua. Vilevile, katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha jinsi wahusika vijana huzinduka baada ya kupitia hali ngumu ya maisha. Kijana anapokua, mabadiliko mengi hutokea na huweza kuwa chanya au hasi. Chanzo cha mabadiliko hutegemea jinsi alivyolelewa au alivyotangamana na jamii. Hivyo basi, maudhui ya mabadiliko na ukuaji yanaingiliana na kukamilishana kwa kiwango kikubwa.

## 2.5 Mabadiliko Miongoni mwa Vijana wa Kike na wa Kiume katika Riwaya teule

### 2.5.1 Mabadiliko ya Hali ya Afya

Mabadiliko ya hali ya afya miongoni mwa vijana wa kike yanatokana na dhuluma za kimapenzi kwa mfano, ubakaji, ugonjwa wa zinaa na mimba za ujanani. Katika *Chozi Langu* (2014) mabadiliko ya hali ya afya yanayotokea kwa mhusika Mliwa yanatokana na kubakwa na Chifu Moegi. Baada ya kubakwa, Mliwa ananyamaza na anaanza kutumia ishara tu. Anaathirika Kisaikolojia na kuanza kuokota taka ovyo. Anakosa usingizi na hamu ya chakula. Aliyekuwa na akili timamu anaanza kutembea mtaani akiokota taka na kuongea pekee. Tabia hii ilimshangaza sana mamake Bonuke. Alikosa kuelewa kinachomfanya mwanawe awe na tabia kama hiyo. Mwandishi anasema;

> Siku tatu baadaye, Mliwa alianza kuasi kula. Hii haikuwa kawaida yake. Hali hii ilimsikitisha na kumtia hofu Bonuke. Baada ya kushindwa la kufanya, aliamua kuwatembelea watu kadhaa kuwashitakia hali ile ya bintiye.( Uk 139)

Mamake aliona si hali ya kawaida na ndio maana akataka kutafuta usaidizi kutoka kwa watu wengine. Analalamika kuwa hajui yaliyotendeka usiku na kumbadilisha binti yake. Imebainika kuwa ubakaji ni kitendo kiovu sana kinachobadilisha hali ya afya ya vijana wa kike na huweza kusababisha kifo. Mliwa anawakilisha wasichana wanaobakwa na kuathirika zaidi. Kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya Uhalisia, maudhui na matukio yalingane na yale ya jamii mtafiti anafahamu kuwa matukio haya hutendeka katika jamii ya kisasa. Wasichana wanaobakwa huathirika kisaikolojia na iwapo hawatapewa ushauri mwafaka, wao huweza kujitia kitanzi kwa sababu ya aibu. Mama mmoja anasema;

> "Wacha mtoto apumzike, alikuwa ameteseka sana. Kutembea akitema maneno makali yanayotuchoma sote masikio ndiko kuishi kweli? Eh? Ama mlivutiwa na kule kuokotaokota takataka ovyo akitembea bila dira?" (Uk 204)

Haya maneno yanasemwa na mama mmoja baada ya watu kufikiria kuwa Mliwa amejitia kitanzi baada ya kubakwa na Chifu Moegi. Mtafiti amegundua kwamba hali hii isiposhughulikiwa kwa haraka au kwa njia inayofaa huweza kusababisha matatizo makubwa zaidi kwa mfano kujitia kitanzi.

Aidha, Yasibu katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) anaonyesha mabadiliko ya Afya baada ya kupata ujauzito. Mwandishi anasema kuwa afya ya Yasibu inaanza kuzorota wakati alikuwa na mimba. Mwandishi anasema;

> Afya ya Yasibu ilianza kutatanisha. Haikuwa ya kawaida. Usiku kucha alikokomoka na kutapika. Kisunzi na fikifiki ya mwili haikumwishia. Mwili wake mgumu wa uanawali ulianza kumomonyoka. (Uk 75)

Kauli hii inaonyesha kuwa Yasibu ambaye alikuwa mwenye siha, sasa anaonyesha kudhoofika. Haya ni matokeo ya mimba. Vilevile, Yasibu anabadilika kiafya baada ya kuambukizwa Ukimwi. Afya ya Yasibu inazorota wakati alianza kuugua. Mwandishi anasema;

> Yasibu hakuweza kula chakula. Mwili wake ulidhoofika. Akakonda kama ng'onda. (Uk 182)

Taarifa hii inaonyesha mabadiliko ya kiafya ya Yasibu. Licha ya hayo, wenzake walimtenga Yasibu na hakuwa na rafiki kwa sababu ya ugonjwa wake.

Vilevile, *Dunia Mashaka Makuu* (2015), mwandishi ameonyesha mabadiliko ya afya miongoni mwa vijana wa kiume. Afya ya Dunia inabadilika wakati alipokuwa akiugua homa kali. Aliugua kwa majuma mawili pasi na kutoka nje. Mwili wake ukabadilika na kudhoofika. Akaonekana kama mzee ilhali ni kijana wa miaka kumi na minne. Mwandishi anasema;

> Mwili wake mwembamba na mweusi wa kimo kirefu, ulimpevusha, asionekane mwenye umri wa miaka kumi na minne. Uso wake wa mviringo ambao daima ulinawiri, sasa ulinywea. (Uk 34)

Taarifa hii inadhihirisha mabadiliko ya kiafya yaliyotokea kwa Dunia wakati alipokuwa anaagua homa kali. Licha ya hayo, Dunia alisononeka zaidi alipotelekezwa na babake. Mwandishi anaeleza kuwa Bwana Mashaka alimchukia zaidi kwa kuwa mtoro wa shule. Hata hivyo, Dunia aliomba babake msamaha mara nyingi lakini babake hakumsamehe. Suala la kutosamehewa na babake lilimkosesha amani Dunia.

Mwandishi anasema;

> "Aliishi na babake ndani ya nyumba bila mapenzi. Babake mara nyingi hakumuuliza la jua au la mvua, la mchana wala la usiku. Dunia alitamani apate nafasi ya kuzungumza na mzee wake juu ya mambo mengi, ya shuleni na yale ya nyumbani bali baba mtu hakudiriki." (Uk 35)

Taarifa hii inaonyesha kuwa Dunia anaathirika kiafya anapopuuzwa na babake. Kwa mujibu wa Jeffrey na Brown (2003) vijana wanaweza kudhoofika kiafya kutokana na malezi mabaya ya wazazi. Babake Dunia anakosa kumpa nafasi mwanawe suala ambalo linamwathiri kisaikolojia.

### 2.5.2 Mabadiliko ya Hali ya Maisha

Katika *Chozi Langu* (2014), mwandishi ameonyesha kuwa vijana wa kike wanaweza kubadilisha hali ya maisha wanapotia bidii katika masuala mbalimbali. Hali ya maisha ya Mliwa inabadilika wakati anaamua kujitosa katika shindano la utangazaji na kuibuka mshindi. Kila mwanafunzi alitaka kuwa karibu naye. Gazeti la kila Jumapili lilibeba habari za ushindi wa Mliwa. Mliwa aliyekuwa anadharauliwa na wenzake shuleni sasa akapata sifa na kuthaminiwa. Akajiona ni mtangazaji mashuhuri. Mwandishi anasema;

> Mliwa akaanza kuwaza kuhusu hali yake mpya. Alianza kuwaza jinsi angekuwa akitembea kwenye barabara za miji mikubwa kama Nairobi huku watu wote wamemtumbulia macho. (Uk 106)

Taarifa hii inaonyesha hali mpya ya Mliwa baada ya kuwa mshindi wa shindano la utangazaji. Shirika la utangazaji likamwahidi kumlipia karo hadi chuo kikuu na kumpa kazi baadaye.

Mliwa anadhihirisha mabadiliko ya hali yake baada ya kufaulu mtihani wa kidato cha nne na kujiunga na chuo kikuu kusomea uanahabari. Mwandishi anasema kuwa, baada ya kuhitimu, Mliwa anapata kazi ya Utangazaji katika kituo maarufu cha Redio Kisu. Mabadiliko haya yanatokana na juhudi alizofanya akiwa shuleni. Ingawa Mliwa alilelewa na mama tu, hicho hakikuwa kikwazo kwake kufaulu. Isitoshe, maisha magumu yalikuwa kichocheo kwa kufaulu kwake. Mtafiti alibaini kuwa, Mliwa alitia bidii masomoni ili abadilishe hali yake na ya mamake. Isitoshe, alitia bidii ili amwaibishe babake ambaye aliwakataa wakiwa wachanga. Anasema;

> "Ningeshinda hapa halafu baadaye niwe mtangazaji mashuhuri, ningeibadilisha hali ya familia yetu na kumwauni mama… ningemwaibisha Kajogoo aliyetufukuza kama mbwa mwitu usiku." (Uk 81)

Mliwa anafaulu na kuwa Mtangazaji. Hali ya maisha ya kimaskini yanabadilika. Anamfungulia mama yake duka kubwa la jumla.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) hali ya maisha ya Yasibu inabadilika baada ya kupata mimba, babake anamchukia zaidi na kumtusi kila mara. Yasibu anapoona kwao hakukaliki sababu ya matusi ya babake anaamua kutoroka kwao na kwenda Mwambao. Kule Mwambao, hali yake inabadilika kwani mazingira yanakuwa tofauti sana na ya kwao. Anakosa makazi na kuamua kulala nje ya duka. Yasibu

aliyelelewa katika familia ya kitajiri sasa anabaki maskini hohehahe. Mwandishi anasema;

> Yasibu hakupata usingizi. Baridi, mbu, kutatarika na mara nyingine kulia kwa Yadhuru. (Uk 113)

Yasibu anadhihirisha mabadiliko ya hali ya maisha anapojiingiza katika uhusiano wa kimapenzi na mzee Fadhili kwa sababu ya shida za kifedha alizokuwa nazo. Mwanzoni, aliishi na Fakiri ambaye hakuweza kuyakimu maisha yake na ya mwanawe Yadhuru. Yasibu alipoona kuwa Fadhili ana mali, anahamia kwake na kumwacha Fakiri. Yasibu ni kielelezo halisi cha binadamu wa kawaida. Mhimili huu wa nadharia ya Uhalisia umemsaidia mtafiti kubaini kuwa Yasibu ni kama wasichana wengine katika jamii ya kisasa ambao hufuata wanaume kwa sababu ya mali. Wasichana hawa huwa hawajali umri wa wanaume au hali yao ya kiafya. Hupofushwa na pesa za wanaume hawa na mwishowe hujipata katika hali mbaya. Yasibu alitamani maisha mazuri na ya anasa. Alipoona kuwa Mzee Fadhili anaweza kumtimizia, Yasibu hakusita kumfuata. Mwandishi anasema;

> "Sebule ilipambwa kwa kila mapambo ya kisasa; runinga, sofa za matakia. Yasibu alijihisi kama aliyefika peponi. (Uk 159)

Mwandishi anasema kuwa maisha ya Yasibu yaliharibika baada ya kuondoka kwa Fakiri kwani baada ya muda mfupi, Fadhili alimfukuza kama mbwa.

Vijana wa kiume huweza kubadilisha hali ya maisha yao wanapofanya kazi kwa bidii. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), hali ya maisha ya Dunia inabadilika

baada ya kupita mtihani. Babake anamwonyesha mapenzi na kuahidi kuwa atamlipia karo hadi chuo kikuu. Kila mtu anamsifu na kumpenda Dunia. Kabla ya haya, babake alimchukia Dunia na kumlaumu kwa kila jambo. Babake alikataa kumlipia karo ya shule. Mwalimu Mkuu alijitolea kumlipia karo na hivyo Dunia alijikakamua na kupita mtihani. Mwalimu Busara anasema;

> "Huyu ndiye kijana Dunia Mashaka Makuu, fahari ya watu wote Kibaoni. Leo tumekusanyika hivi ili tusherekee kufaulu kwake, tunywe na tule, baada ya hotuba yangu na wenzangu."(Uk 132)

Hata hivyo, Dunia anakataa kuendelea na masomo. Anatorokea mjini Mwambao. Hali ya maisha ya Dunia inabadilika pindi alipofika mjini. Maisha mjini yakageuka ya dhiki. Dunia aliyekuwa anaishi katika jumba la kifahari na kula vizuri sasa akazuiliwa gerezani ambapo hali ya humo gerezani ni tofauti sana na kwao. Dunia anasema;

> "Usiku huu watu huko nyumbani wamo juu ya vitanda vyenye magodoro manene na shuka nzito walizojifunika gubigubi. Hapo walipo hawahisi baridi. Sisi bado ni vijana. Saa hizi tungekuwa majumbani labda tumelala raha mustarehe." (Uk172).

Hii ni hali tofauti sana na ya kwao nyumbani. Hii inatokana na ukaidi wake wa kutowasikiliza wazee na walimu wake. Baada ya kifungo, Dunia na Mpoto wanatia bidii katika kazi zao kwa nia ya kuyabadilisha maisha yao. Waliishi maisha duni katika Mtaa wa mabanda wa Jitengeni.

Dunia na Mpoto ni vielelezo halisi vya vijana wanaokaidi amri ya wazazi na baadaye hujipata katika hali ya umaskini. Kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya

uhalisia kuwa mandhari na matukio yaonyeshe kila kitu kama kilivyo, imebainika kuwa matukio kama haya hujitokeza katika jamii ambapo vijana huwacha masomo na kukimbilia mjini ambako wanakumbana na matatizo mengi mno. Kuna wale ambao hujuta na hubadilika ili waanze maisha upya. Mwandishi anasema;

> Dunia na rafikiye Mpoto walidhamiria kuyabadilisha maisha waliyoishi. Sasa walirauka kila siku wakaingia bandarini na madukani kufanya uhamali wa kila aina. Ugumu wa maisha ulianza kupungua polepole. Mabadiliko ya kweli ndiyo hayo yaliyowajia. (Uk 178)

Kauli hii inaonyesha mabadiliko ya hali ya maisha yaliyotokea kwao. Dunia na Mpoto baada ya kutia bidii katika kazi zao. Mabadiliko yanatokea baada ya Dunia kupata kazi na kukodisha chumba ndani ya nyumba nzuri Mtaa wa Kadiri.

### 2.5.3 Mabadiliko ya Tabia

Vijana wa kike hudhihirisha mabadiliko hasi baada ya kudhulumiwa kimapenzi. Hata hivyo wanaposhauriwa, huweza kuonyesha mabadiliko chanya. Mliwa katika *Chozi Langu* (2014) ametumiwa kuonyesha mabadiliko ya tabia yanayotokea baada ya kupewa ushauri nasaha. Mamake Trufena anampa Mliwa ushauri nasaha baada ya kubakwa. Akawa mchangamfu na kurejea katika hali yake ya kawaida. Hali hii inamchochea kuendelea na masomo yake ili awe wakili wa kutetea haki za wanawake wanaodhulumiwa. Mliwa anasema;

> "Mama, pole kwa yote yaliyotokea. Muhimu ni kuwa sasa nimerudi na hali yangu ni kawaida….nimeshughulikiwa na washauri nasaha na madaktari wa kila aina. Sasa niko tayari kurudi shuleni kuendelea na masomo yangu." (Uk 219)

Maneno haya yanaonyesha mabadiliko ya Mliwa baada ya kupewa ushauri nasaha. Amekuwa tena mzima na ana azma ya kuendelea na masomo yake. Mliwa anataka kusoma zaidi ili awe wakili wa kupigania haki za vijana wanaodhulumiwa. Mtafiti alibaini ya kuwa, ushauri nasaha kwa wahasiriwa wa ubakaji ni muhimu sana kwani huwapa tena matumaini. Mwandishi anasema;

> Binti mmoja aliyebakwa alijitia kitanzi. (Uk 219)

Bila kushauriwa vijana hujiona hawafai kuishi na hujitia kitanzi.

Vilevile, Mliwa anaonyesha mabadiliko ya kitabia baada ya kupewa ushauri na rafiki yake Mawazo. Mawazo alimpa moyo Mliwa kuwa hafai kuhangaishwa na wanafunzi ambao wana wivu kwake na kila wakati walipomwita kuwa hana asili wala fasili. Vijana hawa walimbandika jina *"Mathee"* kutokana na umri wake mkubwa. Kutokana na haya, wanafunzi wengi walimtoroka, Mliwa akabaki pekee yake. Kutokana na hali hii, Mliwa alishinda pekee shuleni akilia kila wakati. Mwandishi anasema;

> Mahasidi wa Mliwa walishangaa ghaya walipoona kuwa maneno waliyozua kila mara hayakumpiga mshipa hata chembe. Walishangaa kumwona kasimama imara hata masomoni mwake tena. (Uk 116)

Hii ni baada ya kupewa ushauri na rafiki yake Mawazo. Akaona kuwa azma yake hapo shuleni ni kufaulu. Hakushtuliwa tena na maneno ya wenzake.

Mliwa anaonyesha mabadiliko ya tabia baada ya baba yake kumbagua kwa misingi ya kiuana na kumnyima nafasi ya kwenda shule. Anakuwa na huzuni na kuonyesha

chuki kwa babake hasa anapoona watoto wa rika lake wanapoenda shule. Baada ya mamake Mliwa kupata mtoto wa kike kwa mara ya tatu, babake Kajogoo anawatelekeza na kumwachia mamake majukumu yote ya nyumbani. Mwandishi anasema;

> Bonuke aliporudi nyumbani baada ya siku mbili, Kajogoo hakumjali tena. Mliwa ndiye aliyemsaidia mara nyingi pale nyumbani. Ilibidi mambo ya shule ayaweke chemba. (Uk 40)

Chanzo cha mabadiliko haya ni ubaguzi wa kiuana aliofanyiwa Mliwa kwani babake hakuona umuhimu wa Mliwa kuhudhuria masomo.

Aidha, mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameonyesha mabadiliko ya tabia ya Yasibu baada ya babake kumpa uhuru wa kutembea. Anakosa heshima kwa wazazi wake. Anaanza kuja nyumbani kuchelewa. Babake aligundua kuwa mabadiliko haya yanatokana na uhuru aliompa, kwa hivyo akaamua kuzibadilisha amri. Yasibu kwa sauti kubwa na kavu anajibu kuwa;

> "Afadhili mtu kujifia" (Uk 31)

Kauli hii inamshtua Bwana Mashaka ambaye tena analegeza kamba. Kwa mujibu wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii, mahitaji ya kibinafsi ya vijana hukinzana na ya kijamii kwa hivyo huibua mgogoro kwani vijana huona kuwa wanatawaliwa na wazazi. Mhimili huu umemsaidia mtafiti kubaini chanzo cha mabadiliko ya tabia ya Yasibu. Yasibu anapewa uhuru na baba yake lakini anautumia vibaya. Babake anapomnyima tena uhuru kunazuka mgogoro kati yake na babake.

Kulingana na mwandishi, tabia ya Yasibu huko shuleni ilibadilika kabisa. Anaanza kusinzia darasani. Mwalimu wake Bi. Mpole anashangazwa na mabadiliko ya Yasibu. Tabia hii ya kulala darasani inaanza kudhihirika wakati Yasibu anapata ujauzito. Mwalimu anasema;

> "Tabia ya kusinzia darasani yanikirihi na siitaki kabisa. Tahadhari sana na jambo hilo linalikuzuzua. Usilipe nafasi likaota mizizi kwani litayatia doa maendeleo yako masomoni." (Uk 54)

Maneno haya yanalenga kumshauri Yasibu aachane na mapenzi yanayomzuzua. Jambo ambalo Bi. Mpole hakufahamu ni kuwa Yasibu alikuwa ashapata ujauzito. Zaidi ya hayo, Yasibu akaanza kushika mkia kila wakati wanapofanya mtihani. Aidha, Yasibu anadhihirisha mabadiliko ya tabia kutokana na hali ngumu ya maisha, akaajingiza katika ukahaba. Akaanza kutegemea wanaume ili kupata chakula. Akawa anapigania wanaume. Mwandishi anasema;

> Dunia alisimama ghafla mbele ya dadake aliyegaagaa mchangani nyuma ya klabu akitweta kwa nguvu, mwili ukimgwaya akitapika mapande ya damu. (Uk 180)

Kauli hii inaonyesha ugomvi uliokuwepo kati ya Yasibu na wasichana wengine ambao walimpiga kwa kuona kuwa Yasibu anawanyang'anya wanaume wao. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Uhalisia, Yasibu ni kielelezo halisi cha binadamu wa kawaida na ametumika kuendeleza maudhui ya mabadiliko ya tabia. Yasibu anawakilisha wasichana wa kisasa ambao hujiingiza katika ukahaba wanapokumbwa na hali ngumu ya maisha, Yasibu anaamua kuwa kahaba ili ajikimu kimaisha.

Mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015), ameonyesha mabadiliko ya tabia ya vijana wa kiume wanapotelekezwa na wazazi wao. Dunia alibadilika tabia na kuanza kutumia dawa za kulevya baada ya kukosa mapenzi ya babake. Babake anamtusi kila mara na kumwita kuwa si mtoto wa heri hata kidogo. Anatafuta mapenzi kutoka kwa rafikiye Pazia ambaye anamshinikiza kutumia vileo. Dunia anabadilika tabia na kuwa mkaidi. Zaidi ya hayo, anaacha kwenda shule. Mwandishi anasema;

> Dunia alikosa kwenda shule, akishiriki kufuatana na vijana wengine watoro. (Uk 32)

Hata hivyo, Dunia anaonyesha mabadiliko chanya ya tabia baada ya kushauriwa na mwalimu mkuu na babake. Anaachana na Pazia rafikiye na kuanza kuhudhuria masomo kama ilivyokuwa mwanzoni. Akawa kielelezo cha shule nzima. Akawa mahiri darasani. Mwandishi anasema;

> Maneno ya babake yalimzindua akili. Aliyazingatia. Hakushiriki tena Pazia. Alikwenda kwa Mwalimu Mkuu na akamwomba msamaha na akamweleza dhamira yake ya kuendelea na masomo. (Uk 34)

Licha ya kuonyesha mabadiliko haya, babake anakosa kumwamini tena. Imebainika kuwa baada ya kukataliwa na babake, Dunia akaanza tena kushirikiana na Pazia. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii mahitaji ya kibinafsi hukinzana na ya kijamii kwa hivyo huibua mgogoro kwa sababu vijana huona kuwa wanatawaliwa na wazazi. Mahitaji ya kibinafsi ya Dunia yanakinzana na ya baba yake, kwa hivyo kunakuwa na mgogoro kati yao.

Dunia anaanza kwenda kwa akina Pazia badala ya nyumbani kwao. Mabadiliko ya Dunia yanatokana na ubinafsi wa babake ambaye baada ya Dunia kuteleza, hamkubali tena bali anaendelea kumtusi kila wakati. Dunia anachanganyikiwa. Mwandishi anasema;

> Mambo sasa yalibadilika. Dunia alimtumainia Pazia kwa mambo kadha wa kadha, naye Pazia akamsaidia Dunia, asiwe wa kumfukuza wala kumpuuza. Alipata nafasi ya kumghilibu na kumzuzua. (Uk 82)

Mtafiti amebaini kuwa mabadiliko ya ghafla yanatokana na matumizi ya vileo. Pazia anampa Dunia vileo ili apate ujasiri wa kukataa kusoma. Licha ya hayo, anamkumbusha Dunia alivyopuuzwa na babake wakati alimwitaji sana. Pazia anasema;

> "Siku hiyo ya hadhara Dunia haifai uwe kichwa kikavu, utashindwa na mambo. Ni lazima siku hiyo ujitie na vikali kichwani ndipo utakapokuwa imara. Nitahakikisha hiyo siku umewaka." (Uk 129)

Taarifa hii inadhihirisha kuwa, Dunia alibadilisha msimamo wake kuhusu kuendelea na masomo baada ya kuvuta bangi. Kama anavyosema Stringer (2017), haya ni madhara ya bangi ambayo husababisha mabadiliko ya tabia ya vijana. Hata hivyo, Dunia anabadilisha tabia yake ya ukaidi na kuamua kurudi nyumbani kuomba msamaha baada ya kuhitimisha kifungo. Anafungwa gerezani kwa miezi sita na kazi ngumu. Kutokana na mateso haya gerezani, Dunia anajuta na kulia kwa uchungu. Anasema;

> "Aa! Nimetubu! Nisameheni jamani! Narejea nyumbani sasa. Sina pa kukimbilia." (Uk 208).

Haya ni maneno ambayo anasema akilia wakati alikuwa akipasua jabali ngumu kule gerezani. Anapokumbuka ushauri aliopewa na wazazi na walimu wake aendelee na masomo, anajuta zaidi kwa kutowasikiliza. Mateso haya yalimfanya Dunia kubadilisha mawazo yake. Aliamua kurudi nyumbani aombe msamaha na aanze maisha upya ingawa mwanzoni alikuwa ameapa kuwa hatorudi kwao tena.

### 2.5.4 Mabadiliko ya Hisia

Kamote (2016) anasema kuwa mabadiliko mengi ya kihisia hutokea katika kipindi cha ujana. Mabadiliko ya kihisia ni pamoja na hasira, woga, mapenzi, aibu, wasiwasi, ujasiri, unyonge, furaha na chuki. Mabadiliko haya huathiri tabia ya vijana kwa sababu yanaweza kusababisha kuchanganya akili au hisia zinazotatanisha. Katika *Chozi Langu* (2014) Mliwa anadhihirisha mabadiliko ya hisia baada ya kudhulumiwa na Bi. Rai. Mliwa alimwona kuwa mtu asiye na utu.

Mwanzoni Mliwa anafurahia sana kwenda kuishi na Bi. Rai. Baada ya Mliwa kupata sifa kemkem alipokuwa mshindi wa shindano la utangazaji, Bi. Rai akamwomba Mliwa aishi naye na kumwahidi kuwa angemlipia karo ya shule. Furaha yake ikageuka majuto na machukizi pindi alipofika kwa Bi. Rai ambaye alimdhulumu Mliwa na kumfokea kila wakati. Wakoi wake wakamwonyesha madharau yasiyo mfano. Alijutia uamuzi wa kumtembelea halati wake. Mtazamo wa Mliwa kwa Bi. Rai ukabadilika. Naye akabadilisha uamuzi wake akarudi kwao nyumbani. Mwandishi anasema;

> Siku zilizofuatia ziligeuka na kuwa kizungumkuti kwa Mliwa pale kwa halati wake. Ilibainika kuwa ingawa alikuwa amekaribishwa na

> halatiye pale hakutakikana kamwe. Tuhuma, matusi na masimango zikageuka kuwa mafuta aliyopakwa moyoni kila kukicha na wakoize. (Uk 98)

Kulingana na taarifa hii, Mliwa anabadilisha mtazamo wake kwa Bi. Rai kutokana na dhuluma alizofanyiwa. Furaha yake ikabadilika na kuwa majuto na huzuni.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha athari ya kutawisha vijana wa kike kupitia kwa Yasibu. Tunaambiwa ya kwamba, Yasibu alikuwa mwenye huzuni na mpweke kutokana na hali ya kutawishwa. Baada ya kupewa uhuru na idhini ya kujifanyia mambo, hisia za Yasibu zilibadilika kwa ghafla. Anakuwa mchangamfu zaidi. Kwa mujibu wa Kezilahabi (2005), vijana wa kike wanahitaji uhuru fulani kutoka kwa baba zao ili wafahamu mazuri na mabaya. Mwandishi anasema;

> Bwana Mashaka alivutiwa na uchangamfu wa ghafla wa mwanawe tangu siku ile alipompa idhini ya kujiamulia mambo yake mwenyewe. Yasibu sasa alijipikia chakula, akajiendea kuni na maji. (Uk 26)

Uchangamfu na furaha ilitokea wakati aliporuhusiwa na babake kutembea na wenzake. Vilevile, hisia za mapenzi za Yasibu kwake Pazia zinabadilika baada ya Pazia kukataa kuwa alimpachika mimba. Yasibu aliyempenda na kumwamini Pazia kuwa na kijana mzuri, sasa anamwona kama katili asiye na utu wowote. Anafikiria kujitoa uhai wake lakini anabadilisha nia yake baada ya kusikia sauti ya Mzee Mafusho akiimba;

‘Mbona u hali hiyo kukazani?
Punguza chilio muhisani
Kuond’wi pecheo duniani
Kuko kufa moyoni kwa nini?’ (Uk 95)

Maneno hayo yanamzindua Yasibu. Kutokana na ushauri kupitia wimbo huu Yasibu anabadilisha nia yake ya kujiua na kurudi nyumbani. Hisia alizokuwa nazo za uchungu zinabadilika na anaamua kuendelea kuishi.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), mwandishi ameonyesha mabadiliko ya hisia miongoni mwa vijana wa kiume. Hisia za Dunia kwa Pazia zilibadilika baada ya Dunia kugundua kuwa Pazia alimlaghai. Pazia naye akaendelea na masomo yake na kupata kazi nzuri. Dunia alikuwa na hasira na chuki kwa Pazia hasa alipomkumbusha yaliyopita na kusema kuwa yeye Dunia alikataa kusoma. Kwa mujibu wa Stringer (2017) vijana baleghe wanapokuwa vizuizini wanafaa kufunzwa mambo muhimu yatakayowasaidia baada ya kumaliza kifungo. Lengo la magereza ya vijana baleghe ni kuwafunza adabu ili wawe wema bali si kuwatamausha. Mateso ya gerezani aliyopata Dunia yamemzuia kufanya tena maovu.

Mwandishi anasema;

> Dunia alichemka kwa hasira kama yachemkavyo maji moto sufuriani. Nafsi yake ilimtuma amrukie Pazia amkabe umio papo hapo ima fa ima ndipo alipoyakumbuka maneno haya:"*haitazaa siku nyingine kama hiyo ya leo-siku ya kutoka tena gerezani*…." (Uk 216)

Kutokana na kauli hii, mtafiti amebaini kuwa, mateso ya gerezani aliyopata Dunia yamemzuia kufanya tena maovu, kwani hataki tena kurudi gerezani.

Vilevile, hisia za mapenzi za Pazia kwake Yasibu zinabadilika ghafla alipoambiwa na Yasibu kuwa ana mimba. Mapenzi ya Pazia kwa Yasibu yanageuka kuwa madharau. Pazia aliyejidai kumpenda Yasibu, anamdharau na kumwambia kuwa hahusiki kamwe. Anasema;

> "Sina wasaa mimi wa kumtunga msichana wa shule mimba. Kalitafute fala jingine ulipe mzigo huo" (uk. 93)

Pazia anamwambia hivyo na kumwacha Yasibu akiwa ameduwaa. Hajui vile Pazia alivyogeuka na kuwa wa roho kavu kama ile.

Katika *Chozi Langu* (2014), hisia za mapenzi za Talimbo kwake Mliwa zinageuka kuwa chuki na hasira baada ya Mliwa kukataa kuwa na uhusiana na Talimbo. Talimbo alitaka Mliwa awe mpenzi wake lakini Mliwa akakataa jambo hilo kwa kuwa aliona si wakati mwafaka wa kujiingiza katika mapenzi. Kutokana na haya, Talimbo akaanza kumtusi Mliwa. Anasema;

> "Hilo ni jungu kuu. Limekula chumvi si haba. Huoni hata uso wake unavyoonyesha makunyazi ya mwanamke mzee?" (Uk 69)

Haya ni mabadiliko ya hisia ya Talimbo kutokana na kukataliwa na Mliwa.

## 2.6 Ukuaji Miongoni mwa Vijana wa Kike na wa Kiume Katika Riwaya teule

### 2.6.1 Ukuaji wa Kiakili

Kulingana na McNeely na Blanchard (2009) ukuaji wa kiakili ni wakati ambapo kijana huweza kufikiria na kutatua matatizo yanayomkumba. Mwandishi wa *Chozi Langu* (2014) ameonyesha jinsi vijana wa kike hukua kiakili kadri umri wao unavyosonga. Kulingana na Kroger (2004) ukuaji wa aina yeyote hutegemea malezi na jinsi wahusika wanavyotangamana na wanajamii. Mliwa anadhihirisha ukuaji wa kiakili kadri umri wake unaposonga. Baada ya kuona mateso aliyoyapitia mamake mikononi mwa babake, anaona ni vyema wahame. Anasema;

> "Mama afadhali kuhama hapa tukaishi kwingine. Naona maisha haya yanakutatiza sana. Ingawa umri wangu si mkubwa, naona ni kama unateseka sana."(Uk 40)

Kauli hii inaonyesha kuwa Mliwa amekua kiakili. Ameweza kuona matatizo anayopitia mamake na badala ya kunyamaza anajaribu kutoa suluhu ya matatizo ya mamake kuwa anafaa ahame. Katika umri wake huo mdogo Mliwa anaona kuwa hakuna mtu yeyote anayestahili kunyanyaswa. Mwandishi anasema kuwa katika umri huu wa miaka 13, aliyaona mengi. Babake akimpiga mamake anapotoka ulevini.

Vilevile, Mliwa anadhihirisha kuwa amekua kiakili kupitia kwa mawazo yake kumhusu hale wake. Mamake Mliwa aliposikia kuwa dadake Bi. Rai alitaka kumchukua Mliwa aishi naye, hakufurahishwa na wazo hilo kwani alimjua Bi. Rai kama mwanamke mwenye maringo na majivuno. Mliwa anasema kuwa, hatakataa wito na zaidi ya hayo anahitaji msaada wa Bi. Rai kwani alimwahidi kuwa atamlipia karo. Kama anavyosema Kamote (2016) ukuaji wa kiakili ni pale ambapo kijana ataweza kujifunza na kutatua matatizo yanayomkabili. Mliwa anamwambia mamake kuwa ;

> “Tena aliahidi kunilipa karo ya shule ya muhula ujao. Mama, nitakwenda tu kwa kuwa sisi ni wahitaji.”(Uk 88)

Taarifa hii inaonyesha kuwa Mliwa anafahamu vyema kuwa anahitaji karo ya shule ili aendelee na masomo yake. Bi. Rai amejitolea kumlipia kwa hivyo hana budi kukubali wito wake.

Vilevile, mwandishi amemsawiri Mliwa kama kijana ambaye amepevuka kimawazo kwa kila jambo analolifanya. Imebainika kuwa jinsi Mliwa alivyokuwa akitangamana na wenzake shuleni, mamake na wakoi wake, hivyo ndivyo alivyozidi kufahamu mengi. Aidha, ukuaji wake ulitokana na changamoto na migogoro aliyokumbana nayo katika maisha yake. Imebainika kuwa, Mliwa aliweza kukabiliana na migogoro na changamoto hizo moja baada ya nyingine na kila anaposhinda alijengeka kisaikolojia. Kwa mujibu wa Kroger (2004), iwapo mtu ataweza kusuluhisha mgogoro ipasavyo, ataweza kujenga mbinu mpya zinazohitajika katika ukuaji wa nafsi. Mliwa anasema;

> "Binadamu wote wangetambua kuwa umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu, dunia ingekuwa pahala salama pa kuishi. Kwa bahati mbaya, tofauti ndogo ndogo kama vile jinsia, rangi, tamaduni, kabila-zote zimewafanya wanadamu kuutupilia mbali utu wao." (Uk 231)

Kauli hii inaonyesha busara ya Mliwa. Anasema maneno haya baada ya kupitia changamoto nyingi sana maishani kama vile kutukanwa, kubaguliwa, umaskini na kubakwa. Lakini baada ya kutatua shida hizi zote anaibuka kuwa na busara nyingi mno kuhusiana na maisha. Kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya Uhalisia, wahusika huwa vielelezo halisi wa binadamu wa kawaida. Mliwa ni kielelezo cha wasichana katika jamii halisi ambao huwa hawakati tamaa hata baada ya kupitia matatizo mengi.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Yasibu anaonyesha kuwa amekua kiakili wakati anaamua kutojitia kitanzi wakati alikuwa amekataliwa na babake na Pazia ambaye alimtunga mimba. Ukuaji huu unatokana na ushauri alioupata kupitia kwa wimbo aliokuwa anaimba mzee Mafusho. Yasibu anang'amua kuwa yale ambayo anataka kufanya si ya busara hata kidogo. Anasema;

> "Khaa! Siyakati maisha yangu. Nitajaribu namna nyingine ya kuyakomesha mateso haya. Ikizidi mwanangu Yadhuru ningemwachia nani?" (Uk 95)

Kauli hii inaonyesha kuwa Yasibu anatafuta njia mbadala ya kusuluhisha matatizo yake. Anaona kujiua si kusuluhisha tatizo bali kuleta shida zaidi hasa kwa mwanawe Yadhuru. Aidha, Yasibu anaonyesha ukuaji wa kiakili pale ambapo anaamua kurudi kwao Kibaoni akiwa na lengo la kutatua shida zake. Baada ya

kutalikiwa na mumewe Bwana Fadhili, Yasibu na wanawe wakakosa mahali pa kuishi na chakula. Marafiki wote wakamtoroka. Akawa anazunguka akiomba tu. Kwa sababu hii, akaona heri arudi kwa wazazi wake pindi apatapo nafuu. Anasema;

> “Mwenyezi Mungu akikujalia salama Fakiri, nitafutie nauli walau ya kwenda nyumbani kwa wazazi wangu. Roho inaniuma na inanituma nirudi Kibaoni kwa baba na mama.”( Uk 201)

Kauli hii inaonyesha majuto ya Yasibu baada ya kupitia matatizo mengi. Anaamua kubadilisha msimamo wake baada ya kutambua kuwa aliwakosea wazazi wake kwa kutoroka nyumbani kwao.

Aidha, mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015), anaonyesha kuwa vijana wa kiume hukua kiakili baada ya kupitia mateso. Dunia anaonyesha kuwa amekua kiakili wakati anatambua kuwa alifanya makosa kutoroka kwao nyumbani na kukataa kuendelea na masomo. Dunia anataka kuanza maisha upya, arekebishe makosa aliyoyafanya. Akaona suluhu ni kurudi kwao Kibaoni kupata radhi za wazazi wake na kuanza maisha upya, kwani kuishi Mwambao kungemletea matatizo mengi zaidi. Dunia anasema;

> “Nisamehe baba, nisamehe, nimeyaona mateso baba, ulimwengu ukanifunza nikawa sina kwingine kwa kukimbilia ila hapa kwako. Usinikane baba!” (Uk 221)

Taarifa hii inaonyesha kuwa ulimwengu ulimfunza Dunia na sasa amekua kiakili kwani ametambua kuwa alifanya makosa makubwa sana kuiacha elimu. Amepata

mateso mengi sana kwa kukosa elimu. Mateso aliyoyapata Dunia kule Mwambao yamemkomaza akili.

Dunia na Mpoto wanaonyesha kuwa wamekua kiakili walipoamua kujitafutia kibarua kama njia ya kusuluhisha tatizo la umaskini. Mwandishi anasema kuwa, baada ya kifungo cha miezi sita, waliishi katika vibanda. Wakakosa chakula, mavazi na malazi. Waliamua kutafuta kibarua ili wayakimu maisha yao. Mwandishi anasema;

> Dunia na rafikiye Mpoto walidhamiria kuyabadilisha maisha waliyoishi. Sasa walirauka kila siku wakaingia bandarini na madukani kufanya uhamali wa kila aina. Mwenyezi Mungu aliwalipa kwa nia zao njema za kujipatia riziki ya jasho lao. (Uk 178)

Dunia na Mpoto wametambua kuwa kukaa bwete hakutakuwa na manufaa yeyote. Wanaamua kujitafutia riziki.

Katika *Chozi langu* (2014) mwandishi ameonyesha kuwa Mawazo rafikiye Mliwa vilevile anaonyesha kuwa amekomaa kiakili. Wanafunzi wenzake wanapomtusi Mliwa kuwa hana asili wala fasili, yeye anaonyesha mawazo tofauti. Anamtetea Mliwa kila wakati anapotusiwa. Licha ya hayo, anampa ushauri Mliwa jinsi ya kukabiliana na shida hiyo. Anasema;

> "Kwani kumjua babake mzazi sisi umuhimu gani? Nikifikiria lililo muhimu ni kujua unalotaka kuchangia duniani." (Uk 112)

Kauli hii inaonyesha kuwa Mawazo amekomaa kiakili.

### 2.6.2 Ukuaji wa Kimaadili

Kamote (2016) anasema kuwa ukuaji wa kimaadili ni uwezo wa kujenga tabia kutokana na mfumo wa kuamini ili kujua lisilo sahihi na lililo sahihi. Mliwa katika *Chozi Langu* (2014) anadhihirisha ukuaji wa kimaadili anapoamua kutoka kwa hale wake kwa sababu ya dhuluma aliyofanyiwa na wakoi wake, anarudi kwao nyumbani na kumjulisha mamake yaliyotendeka. Mamake anamweleza kuwa ni ukweli dadake amebadilika tangu apate pesa nyingi. Mliwa naye, anamweleza mamake kuwa pesa si kila kitu. Kilicho muhimu duniani ni utu. Anasema;

> “Usijali mama, pesa si kila kitu duniani. Ukiviringia vya duniani, utakwisha na kuviacha papa. Katika umri wangu wangu mdogo, nimefahamu sasa utu ndio kila kitu.”(Uk 101)

Kauli hii inaonyesha kuwa Mliwa amekua kimaadili. Mliwa anafahamu kuwa pesa tu sio muhimu bali utu.

Mliwa vilevile ametumiwa kuendeleza maudhui ya ukuaji wa kimaadili pale ambapo anakataa kujihusisha kimapenzi na kijana mwenzake Talimbo. Anaona hakuna haja ya uhusiano wa aina ile ambao unaweza kuwa kama wa wazazi wake. Mliwa aliona jinsi mamake alivyoteseka kutokana na dhuluma aliyofanyiwa na babake. Ameona na amejifunza mengi kutokana na ndoa hiyo ya wazazi wake. Kutokana na hilo Mliwa anaona hakuna haja ya kuwa katika uhusiano wa namna hiyo. Mwandishi anasema;

> Picha ya jinywa pana la babake likimtafuna mamake ingali mbichi katika akili yake. Kama uhusiano wa kijinsia tofauti unaweza kuwa kama wa wazazi wake, basi kwa nini ajitose?’ (Uk 68)

Mtafiti alibaini kuwa Mliwa amejifunza kutokana na mateso aliyoyapata, ametambua lililo nzuri na lisilo nzuri katika maisha yake.

Kulingana na mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Yasibu anatambua kuwa alifanya makosa kutoroka kwao. Anamwomba Fakiri ampe nauli ili arudi nyumbani kuomba wazazi wake msamaha. Hii inatokea wakati anapata mateso mengi mjini Mwambao kwa mfano, kukosa makazi, chakula. Licha ya hayo, anaugua ugonjwa usio na tiba na kila mtu anamkimbia. Anasema;

> "Roho yangu inaniuma na inanituma nirudi Kibaoni kwa baba na mama, nikautue mzigo ulio moyoni mwangu ambao sasa wanishinda kuubeba." (Uk 200)

Kauli hii inaonyesha kuwa Yasibu sasa amekua kimaadili baada ya shida alizopitia. Anataka arudi kwao ili awaombe wazazi wake msamaha.

Yasibu anadhihirisha ukuaji wa kimaadili pale anapogundua kuwa alifanya makosa kuhama kwake Fakiri. Mwandishi anasema kuwa, Fakiri ni kijana mwenye utu aliyemkaribisha Yasibu kwake siku ya kwanza Mwambao. Licha ya umaskini wake, Fakiri alijaribu kumpa Yasibu mavazi, chakula na vitu vinginevyo. Lakini Yasibu alipokutana na tajiri Fadhili aliamua kuhamia kwake. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya uhalisia, mazingira na matukio yalingane na yale ya jamii inayorejelewa. Matukio haya na mazingira yanashuhudiwa katika jamii halisi. Wasichana wabichi wanapoacha masomo hukimbilia mjini wakitarajia kuwa mambo yatakuwa sawa. Lakini wanapopata matatizo wao hujuta na baadaye

hufahamu kuwa walikosea. Fadhili alimfukuza Yasibu kwake na hapo akakumbuka utu wa Fakiri. Akajuta kumtoroka Fakiri. Yasibu anasema;

> "Kwa nini sikuuzingatia wasia wa mama pale nilipoamua kumtoroka Fakiri? Kwa hakika nilifanya makosa kwa kutouthamini utu."( Uk 186)

Yasibu anajuta kwa kumtoroka Fakiri aliyemsaidia wakati wa shida. Sasa anafahamu kuwa hakufanya sahihi kabisa. Anaamua kwenda kumwomba Fakiri msamaha.

Vilevile, katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha kuwa ukuaji wa vijana wa kiume mara nyingi hutokana na ushauri nasaha kutoka kwa wazazi, walimu, wazee na vijana wenzao. Dunia anatambua kuwa alifanya makosa kuacha kuendelea na masomo baada ya kushauriwa na rafikiye Mpoto. Mpoto anamwambia wakiwa gerezani kuwa alifanya makosa makubwa sana kuacha shule. Anasema;

> "Kukataa kwako shuleni kunasikitisha sana. Kwa nini ulikataa kuelimika? Hungekuwa hapa falau una elimu, ukabakisha uking'olewa meno." (Uk 174)

Maneno haya yanamzindua Dunia. Anafahamu kuwa hakufanya jambo la busara kutoroka kwao na kuacha shuleni. Anapata mateso mengi sana na akang'amua kuwa Pazia alimponza. Anajuta sana akiwa gerezani. Anasema;

> "Falau ningeyabaini mateso haya singeyashika mashauri ya Pazia."Wembe ushanikata jamani! Damu yanichuruzika! Nisaidieni!" (Uk 208)

Kauli hii inaonyesha kuwa Dunia amekua kimaadili kwani ametambua kuwa hakufanya vizuri kuacha masomo. Stringer (2017) anasema kuwa, sheria huwafunza vijana maadili mema. Sasa Dunia amejua lipi lililo sahihi na lipi lisilo sahihi. Baada ya kifungo anaamua kurudi kwao kuomba msamaha kwa wazazi wake.

Kwa mujibu Kiprugut (2011), Imani za kidini huwaongoza vijana katika maisha na kuhimiza uadilifu. Dunia anadhihirisha kuwa amekua kimaadili kutokana na imani za kidini pale ambapo anakataa kuiba aliposhauriwa na Mpoto. Anasema kuwa;

> "Uchukuaji wa mali isiyo halali yako ni wizi na wizi ni kitendo kiovu mbele ya Muumba wa ardhi na mbingu." (Uk 177)

Elimu ya shuleni pia imesawiriwa kama njia moja ya kuwakomaza vijana. Dunia akiwa gerezani anakumbuka maelezo ya mwalimu wake kuhusu elimu ambayo aliikataa. Dunia sasa anaona umuhimu wa elimu kwani angekuwa nayo hangekuwa taabani. Mwalimu Busara anasema kuwa;

> "Elimu humtoa kijana kwenye uduni wa tabia ikamweza kwenye ulingo wa matendo ya adili. Si mno mwenye kuelimika kutenda matendo ya uhayawani." (Uk 131)

Mwandishi ameonyesha umuhimu wa elimu katika kufunza maadili. Vijana wanapopata elimu huelekezwa vyema kimaadili.

### 2.6.3 Ukuaji wa Kijamii

Erickson na Erickson (1998) wanaeleza kuwa vijana wanapokua Kijamii wanapata uwezo wa kujenga na kuendeleza uhusiano na watu wengine. Vijana wanapokua kimaadili hukua pia kijamii kwani watapata uwezo wa kujenga uhusiano mwema na watu. Cherry (2017) na McLeod (2013) wanakubaliana na kauli ya Erickson na Erickson (1998) wanapoeleza kwamba utangamano na mtagusano wa kijamii ni muhimu katika ukuaji wa mtoto. Kwa mujibu wa mwandishi wa *Chozi Langu* (2014), Mliwa alidhulumiwa na wakoi na hale wake na hiyo ikawa njia moja ya kumkomaza. Mliwa amepata ufahamu kuwa ingawa hale wake ana pesa nyingi, amekosa utu jambo ambalo ni muhimu sana. Hivyo basi, kutokana na utangamano wake na hale wake ameweza kukomaa. Mliwa anasema;

> "Pesa si kila kitu duniani. Ukiviringia vya duniani, utakwisha na kuviacha papa hapa. Katika umri wangu mdogo, nimefahamu kuwa utu ndio kila kitu. Kama ninavyojua, kuinamako ndiko kuinukako." (Uk 101)

Taarifa hii inaonyesha kuwa, Mliwa ametambua kuwa ili kuwa na uhusiano mwema na watu ni muhimu kuwa na utu lakini si pesa tu. Mliwa anakuwa na busara kila anapokua. Mliwa anawaelezea wenzake jinsi ya kuishi pamoja kwa njia inayofaa.

Tunaambiwa kuwa suala la kufukuzwa na babake lilimsumbua Mliwa moyoni. Hakuwa na furaha. Wenzake walimwona kuwa hafai kwa sababu babake aliwafukuza kwao. Hata hivyo, baada ya kupewa ushauri na mamaye na rafikiye Mawazo, Mliwa akajua jinsi atakavyoishi na wenzake hapo shuleni. Akafahamu lililompeleka shuleni. Anasema;

> “Potelea mbali. Watasema mchana lakini usiku watalala. Nitaendelea kujikuza kwa kila hali na namna.” (Uk 116)

Hii ikawa falsafa yake mpya kila mara aliposikia maneno mabaya kumhusu. Mliwa amepata mbinu ya kukabiliana na changamoto hii ya kubaguliwa.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi amemtumia mhusika Yasibu katika kudhihirisha ukuaji wa kijamii pale anapoamua kumtafuta Fakiri ili amwombe msamaha kwa kumtoroka. Baada ya kuona kuwa hana rafiki wa kumkimbilia, Yasibu alisononeka sana. Hivyo basi, aliona heri arudi kwa Fakiri amwombe msamaha ili yeye na Fakiri wawe na uhusiano mwema. Yasibu anasema;

> “Haidhuru! Nitakwenda vivyo hivyo. Hata akinifukuza itakuwa sawa kwani atakuwa amekamilisha jambo nililolianza.”(Uk 186)

Yasibu alikuwa amevuruga uhusiano kati yake na Fakiri, kwa hivyo, anaamua kwenda kumuomba Fakiri msamaha ili kuujenga uhusiano wao upya.

Aidha, katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), mwandishi ameonyesha kuwa, kuna elimu ambayo vijana huipata darasani na nyingine katika ulimwengu. Yoyote ile huwafunza vijana jinsi ya kuishi na watu wengine katika jamii. Dunia anaonyesha kuwa amekua kijamii pale ambapo anampisha Mzee Mjumbe kiti katika basi ili aketi. Dunia alikuwa anarejea nyumbani baada ya dhiki na mateso aliyoyapata gerezani. Anakutana na Mzee Mjumbe na pale anampisha aketi. Mzee Mjumbe anasema;

> “Ahaa! Angalia mfano wa adabu njema yoo! Kakuna hata chijana mwengine mnaye muola mempisha ntu nzima chiti ila ye. Wazee wapata taabu kulihali vijana wankaa raha mustarehe.”(Uk 213)

Baada ya Dunia kupuuza ushauri wa Mzee Mjumbe wakati alipokuwa akitoroka kwao nyumbani, sasa anajaribu kujenga uhusiano mwema kati yake na Mzee Mjumbe baada ya kupata dhiki.

Mwandishi amesawiri dini kama asasi ambayo inawakomaza vijana. Baadhi ya wahusika katika riwaya hii wamekua kutokana na mafundisho ya dini waliyoyapata. Fakiri anaonyesha kuwa amekua kijamii anapomsamehe Yasibu ambaye alimtoroka baada ya kukutana na Fadhili. Ingawa Fakiri alimsaidia sana Yasibu na mwanawe wakati alikuwa na shida, anamtoroka na kufuata Fadhili. Fakiri anaumia sana lakini kwa ajili ya kujenga uhusiano mwema, Fakiri anamsamehe Yasibu. Kwa mujibu wa McNeely na Blanchard (2009) ukuaji wa kijamii kimaadili na kihisia huingiliana kwa kiasi kikubwa. Kijana anapojua kudhibiti hisia zake, itakuwa rahisi sana kuwa na uhusiano bora na wengine. Licha ya maumivu aliyoyapata Fakiri baada ya kuachwa na Yasibu, anaamua kumsamehe ili waendelee kuishi kama hapo awali. Mwandishi anasema;

> Aliwaza jinsi moyo ulivyomdunda siku hiyo juu ya hatua yake ya kumkaribisha mtu asiyemjua. Aliona hayo yalikuwa makosa yake mwenyewe. Punde si punde, dhana tofauti ilimjia Fakiri kwamba mema yote aliyomtendea Yasibu ilikuwa ni kazi ya Mungu. (Uk 165)

Taarifa hii inaonyesha dini imechangia katika ukuaji wa kijamii wa Fakiri kwani ameamua kumsamehe Yasibu.

Katika *Chozi Langu* (2014) mwandishi ameonyesha kuwa Mawazo rafikiye Mliwa anafahamu kuwa si vyema kumtenga Mliwa kutokana na hali yake ya baba yake kuwafukuza. Wengine wakimtusi Mliwa na kumwita kuwa hana asili wala fasili, yeye anashirikiana na Mliwa hata anampa mawaidha kuhusiana na maisha ya Mliwa. Anasema;

> "Huwezi kujisumbua kuhusu jambo usiloweza kulitatua. Kilicho muhimu kwako ni kujikaza kwa kila namna uyagange maisha yako ya halafu. Usiwategemee binadamu wanaokutakia mabaya."(Uk 115)

Maneno haya yanadhihirisha kwamba Mawazo amekua kijamii kwani anaweza kutangamana na wenzao vyema bila kuwabagua.

### 2.6.4 Ukuaji wa Kihisia

Kwa mujibu wa McLeod (2013) vijana wataonyesha ukuaji wa kihisia wakati wataweza kutofautisha na kudhibiti mihemko ya aina mbalimbali. Katika *Chozi langu* (2014) mwandishi anaonyesha jinsi baadhi ya vijana wa kike huweza kudhibiti hisia za kimapenzi. Mliwa amekua kihisia kwani anaweza kudhibiti hisia zake za kimapenzi. Mwandishi anasema ya kuwa, Talimbo kijana wa kiume alipotaka wawe na uhusiano wa kimapenzi naye, Mliwa anaona kuwa huo si wakati mwafaka wa kujiingiza katika mapenzi. Anasema;

> "Talimbo, hilo ni pendekezo zuri lakini huu si wakati wake. Tukimaliza masomo labda tufikirie mambo kama hayo. Kwa sasa tushirikiane tu kama wanafunzi marafiki."(Uk 68)

Anasema kuwa yeye ni mwanafunzi na anajua lengo lake pale shuleni ni kusoma. Hii inatokana na mambo magumu aliyoyapitia kule nyumbani.

Mliwa anaonyesha kuwa amekua kihisia baada ya kupewa ushauri nasaha na mama Trufena. Kulingana na mwandishi, Mliwa alikuwa mwenye wasiwasi mwingi na huzuni baada ya kubakwa na Chifu Moegi. Baada ya kupewa ushauri nasaha, Mliwa anaonekana mchangamfu na pia anamsamehe Chifu Moegi. Mwandishi anasema kuwa, baada ya kurudi shuleni, aliwaelezea wenzake kuwa hakuna aliye mkamilifu kila mtu ana dosari. Anasisitiza umuhimu wa kusameheana kwa kuwa aliyekamilika ni Maulana pekee. Anasema;

> "Kumbuka maisha kwa kawaida ni magumu kuliko kifuu cha nazi. Afadhali kuwa mwenye wingi wa msamaha na toba. Ukiishi na kisasi moyoni, kitakuumiza mwenyewe. Mimi nimeamua kusahau yaliyopita na kuganga yajayo." (Uk 230)

Hii kauli inaonyesha kuwa Mliwa amekua kwani amejua jinsi ya kudhibiti hisia za uchungu na huzuni. Amejua kuwa msamaha ni njia ya kipekee ya kuondoa kinyongo moyoni. Ukuaji wa Mliwa ulitokana na changamoto alizopata maishani hususan kubakwa.

Kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya Uhalisia, wahusika huwa vielelezo halisi vya binadamu wa kawaida. Hivyo, basi, Mliwa ni kielelezo cha wasichana wanaopitia changamoto kama kubakwa. Mliwa ametumiwa kuendeleza maudhui ya ukuaji wa kihisia anapoweza kukabiliana na changamoto nyingi hasa ubakaji. Hizi ni changamoto ambazo vijana wa kike katika umri huu hupitia katika jamii halisi. Kupitia dhuluma hii, Mliwa anapata mshauri nasaha ambaye anamshauri jinsi ya

kukabiliana nayo. Mliwa anajitokeza kuwa aliye na busara zaidi baada ya kushauriwa. Akajitambua tena kuwa ana umuhimu katika jamii na akaazimia kukuza nafsi yake zaidi.

Katika *Dunia Mashaka Makuu (*2015) mwandishi ameonyesha kuwa, vijana wa kiume hukua kihisia baada ya kupitia matatizo mengi. Dunia amekua kihisia kutokana na mafunzo ya ulimwengu. Alipokuwa akirudi nyumbani baada ya kumaliza kifungo, anakutana na Pazia ambaye anamkejeli kwa kumwambia kuwa yeye Dunia alikataa kuendelea na masomo licha ya kushauriwa na watu. Licha ya hayo, Pazia anamweleza Dunia kuwa yeye Pazia sasa ni Mkurugenzi katika kampuni ya mafuta. Dunia anakasirika sana na maneno ya Pazia na anatamani amrukie amkate umio. Dunia anakumbuka ahadi aliyojipa akitoka gerezani kuwa hatawahi kurudi tena gerezani. Mwandishi anasema;

> Dunia aligeuka huku akitetemeka kwa ghadhabu, akaondoka. Umahiri wa mwanadamu ni pale anapomudu kuizuia hasira yake wakati ikimtuma kutenda jambo lisiliostahili. Kwa kulitimiza hili, bila shaka Dunia aliibuka mshindi. (Uk 216)

Mtafiti amebaini kuwa Dunia aliweza kuthibiti hisia zake za hasira kutokana na mateso aliyoyapata gerezani. Baada ya kifungo, Dunia aliapa kuwa hangerudi tena gerezani kwa vyovyote vile. Anadhihirisha ukuaji wa kihisia anapoamua kutulia na kuendelea na safari yake. Kama wanavyosema McNeely na Blanchard (2009), ukuaji wa kihisia ni kuwa na uwezo kuona, kupima na kuzuia hisia. Hivyo basi, hakuona haja ya kuzua ugomvi kati yake na Pazia.

Vilevile, katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi kupitia kwa wahusika vijana, ameonyesha kuwa, hisia za kimapenzi miongoni mwa vijana baleghe haziwezi kupuuzwa, kwani wengi wao hawawezi kudhibiti mihemko ya aina hiyo. Vijana wa jinsia tofauti wanapokaa pamoja, inakuwa vigumu sana kuzuia hisia za namna hiyo. Hiyo ndio maana matokeo ya mtihani hudorora na wasichana wengi hupata mimba. Dunia anasema;

> "Hisia za miili ndizo zinazowasumbua wavulana na wasichana hao. Wavulana hasa huathiriwa mno na hisia hizi hata wasimudu kujizuia na ndiyo maana katika shule hii wavulana hushindwa na wavulana daima."(Uk 84)

Kwa mujibu wa Cherry (2017) vijana katika umri huu wa kubaleghe hukumbwa na hisia za kimapenzi na pasipo uangalifu, wengi wao huathirika kwa mfano wasichana hupata mimba za ujanani. Talimbo anashindwa kudhibiti mihemko ya hisia za kimapenzi ndio maana anakasirika zaidi wakati Mliwa anapokataa ombi lake la kuwa na uhusiano. Kukataliwa kwake kunazua chuki kwake Mliwa na anaanza kumrushia matusi kila wakati. Haya ni mambo yanayoshuhudiwa katika jamii. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya uhalisia, wahusika wa kazi ya fasihi huwa vielelezo halisi vya binadamu wa kawaida.

Mliwa, Talimbo, Dunia, Mpoto na Pazia ni viwakilishi vya vijana katika jamii na matukio yanayopatikana katika riwaya teule hushuhudiwa katika jamii. Vijana baleghe wanafaa kushauriwa vilivyo kuhusu suala la mapenzi ili waweze kudhibiti hisia zao. La sivyo, wengine hujitia kitanzi kwa sababu ya kukataliwa au kuwadhuru wale waliowakataa. Kwa mfano kulingana na Mumbi (2017), kisa

kilishuhudiwa kule Mirera Naivasha mnamo tarehe 29 Januari, mwaka 2019 ambapo mvulana wa miaka 17 alimuua msichana miaka 15 kwa kumdunga kisu zaidi ya mara kumi baada ya msichana kukataa kufanya mapenzi na yule mvulana.

## 2.7 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti amechanganua kwa kina maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya za *Chozi Langu (2014)* na *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Waandishi wameonyesha mabadiliko na ukuaji unaotokea katika maisha ya vijana baleghe na chanzo chake. Aidha, vijana wa kike hudhihirisha mabadiliko hasi wanapobakwa, kubaguliwa kiuana au kutawishwa. Wanaposhauriwa, hudhihirisha mabadiliko chanya na Ukuaji. Vijana wa kiume nao wanapokosa mapenzi kwao nyumbani kwa mfano, matusi na kutukanwa kila mara husababisha mabadiliko hasi kama vile kuanza kutumia mihadarati kujiliwaza. Aidha, matumizi ya mihadarati husababisha mabadiliko hasi.

Mihimili ya nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii imekuwa muhimu sana katika kubainisha chanzo cha mabadiliko na ukuaji wa vijana. Kwa mfano, kijana anataka kufanya lile na jamii inamtaka afanye hili. Kwa hivyo kunazua mgogoro baina ya jamii, wazazi na vijana. Vijana hupata migogoro mbalimbali ambapo wakitatua kwa njia inayofaa huonyesha mabadiliko chanya. Nadharia ya Uhalisia imetumika kuonyesha uhalisia wa mambo na kwamba wahusika waliotumika kuendeleza maudhui ya mabadiliko na ukuaji ni vielelezo halisi vya binadamu wa kawaida. Katika sura ya tatu changamoto wanazopitia vijana katika jamii na suluhu zake zitashughulikiwa.

# SURA YA TATU

# CHANGAMOTO WANAZOPITIA VIJANA KATIKA JAMII NA SULUHU ZAKE

## 3.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana yamejadiliwa kwa kina. Sura hii imeshughulikia changamoto wanazopitia vijana wa kike na wa kiume katika jamii na jinsi wanavyotoa suluhu kwa kujikita katika *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu (2015).*

Kuna umuhimu wa kuangazia suala la ujana duniani ili kubaini changamoto wanazopitia vijana baleghe. Changamoto zinazowakabili vijana zinaegemea mhimili wa nadharia ya uhalisia inayosema kuwa fasihi husawiri uhalisia wa maisha katika ngazi zote za kiuchumi, kisiasa, kiutamaduni na kijamii. Katika kuchanganua changamoto hizo, ni muhimu matukio halisi yazingatiwe kama yanavyojitokeza katika jamii. Pia, msanii huangalia matatizo ya jamii na kuchunguza chanzo chake.

Changamoto hizi ni jumla ya mambo ambayo vijana hukumbana nayo katika maisha wanapokua. Kwa mujibu wa McLeod (2013) katika umri wa kubaleghe, kijana hupitia mgogoro wa kisaikolojia ambao ni utambulisho dhidi ya usambazaji majukumu. Kulingana na Wood (2011), hatari katika hatua hii ni kuwa vijana huchanganyikiwa wasijue wao ni nani au wanapatikana katika kundi lipi.

Katika hatua hii vijana hufikiria na kupanga malengo mazuri ya maisha na kujifunza mambo mapya. Aidha, kijana huanza kuwa na hisia za kimwili na

hutamani kuwa na uhuru katika maamuzi. Hiki ni kipindi chenye changamoto nyingi sana kwa sababu kijana anakumbana na hali mpya ya mabadiliko ya mwili na anajiona yupo tofauti na alivyokuwa mwanzo.

Kijana huweza kuchanganyika akili kwa sababu anatarajiwa kutekeleza majukumu ya watu wazima na ya watoto kwa nyakati tofauti tofauti. Hata hivyo, McNeely na Blanchard (2009) wanasema kwamba, huu ni wakati vijana wanafaa kujitambua na kujikuza na sio kupata matatizo. Wale wanaopata mwelekeo na motisha ya kufanya jambo fulani wataibuka na ujasiri na kujitegemea vilivyo. Wanaokosa mwelekeo huchanganyikiwa na hata kupotoka kimaadili.

Baada ya uhuru, viongozi walioshika hatamu hawakuweka chini sera dhabiti ya kushughulikia maisha ya vijana. Waandishi wa fasihi pia hawakulipa uzito suala la vijana katika uandishi wao. Kama anavyosema Mutembei (2013), fasihi zilizokuwepo wakati wa ukoloni zilizungumzia masuala ya utumwa. Baada ya ukoloni fasihi zilizungumzia usaliti wa kisiasa. Lakini baadaye katika miaka ya 1980 na kuendelea waandishi wakaanza kuzungumzia masuala ya vijana. Kwa mfano, *Safari ya Usiku* (2007), *Tumaini (*2006) na *Siku Njema* (2003). Hata hivyo, *Dunia Mashaka Makuu* (2015) na *Chozi Langu* (2014 *)*zinajitokeza kama kazi ambazo zimeangazia changamoto zinazowakabili vijana baleghe na jinsi wahusika hawa wanavyojaribu kujikwamua kutoka kwa matatizo hayo.

Waandishi wamedhamiria kumuasa, kumwelimisha, kumzindua na kumfichulia msomaji uhalisia wa maisha. Maisha yanavyosawiriwa katika riwaya za *Chozi Langu (2014)* na *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ni mfano wa maisha ya kila siku

ambayo vijana hupitia na changamoto ambazo wanapitia katika nchi ya Kenya na Barani Afrika kwa ujumla. Kwa mujibu wa Naliaka (2012), changamoto hizi hupatikana katika kila jamii, licha ya kuwa huweza kutofautiana. Mwandishi ameonyesha kuwa changamoto hizi huweza kutoka kwa vijana wenyewe au hutokana na wahusika wengine. Kupitia changamoto hizo, waandishi wa riwaya teule wameonyesha jinsi baadhi ya vijana husuluhisha matatizo yanayowakumba. Kuna changamoto zinazowakumba vijana kwa ujumla kwa mfano; umaskini, ukosefu wa usalama, msongo wa mawazo, ukosefu wa malezi bora, uhusiano wa kimapenzi na ukosefu wa elimu. Vijana wa kike hukumbwa zaidi na changamoto kama vile; dhuluma, kubaguliwa kiuana na mimba za ujanani. Vijana wa kiume nao hukumbwa zaidi na vizuizi na vifungo vya jela na matumizi ya mihadarati .

## 3.1 Changamoto Wanazopitia Vijana wa Kike na wa Kiume katika Riwaya teule

### 3.1.1 Umaskini

Maskini ni mtu mwenye kipato kidogo ambaye huishi kwa dhiki. Aidha, umaskini ni hali ya kutoweza kujikimu kimaisha. Vijana hujipata katika hali hii ya umaskini kwa kuzaliwa katika familia ya kimaskini au kwa kuyapuuza mambo muhimu ya kuwaendeleza kimaisha. Katika riwaya ya *Chozi Langu* (2014) mwandishi ameonyesha bayana jinsi umaskini huathiri masomo ya vijana wa kike. Anasema kuwa watoto hukosa matumaini ya kwenda shule kwa sababu ya kukosa karo ya shule.

Mwandishi anasema;

> Kwingine mtaani watoto waliotimu umri wa kwenda shule walikuwa wakichezacheza kwa furaha wasijue yaliyowangoja, wenzao wakiwa shuleni. (Uk 9)

Wengi katika hali hii hukosa kuhudhuria masomo na hubaki wakifanya vibarua ili kujiendeleza kimaisha. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Uhalisia kuwa fasihi husawiri uhalisia wa maisha, Mliwa anadhihirisha mambo halisi yanayotendeka katika jamii ya kisasa. Kama wanavyosema Onyango na Tostensen (2015) asilimia 34 ya vijana wanaoishi mijini huishi katika mitaa ya vibanda na hufanya kazi za kijungu jiko ili wapate chakula. Mliwa, amesawiriwa kama msichana ambaye anakumbana na changamoto ya umaskini kwani alizaliwa katika hali hii. Mwandishi anasema;

> Mvua iliponyesha kwa ghafla, kama ilivyofanya mara nyingi, iliwabidi wengi kulala kimahangaiko, wasipate pa kutulia. Baadhi ya wakazi walisombwa na maji taka haswa. Wakazi wengi wakiishi maisha ya kijungu jiko, hawakuwa na cha mno.……humu ndimo alimozaliwa Mliwa. ( uk 1)

Mliwa alilelewa katika mtaa duni na masaibu yake yalizidi wakati babake aliwafukuza wadogo wake na mama yao. Sababu ya kufukuzwa ni kwamba mamake hakuweza kuzaa mtoto wa kiume. Mliwa akaathirika zaidi. Mamake alihamia kwa mtaa duni zaidi kwa vile hakuwa na kazi ya malipo mazuri. Kama wanavyosema Dacey na John (2009), wazazi wanapotalikiana watoto huathirika kwani mzazi mmoja huweza kukumbwa na tatizo la kifedha.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Yasibu anayapuuza mashauri ya wazazi wake na kuacha masomo yake akiwa na umri wa miaka 15 baada ya kupata ujauzito. Maisha yakawa magumu pale nyumbani kwa sababu ya uhasama wa babake mzazi. Akaamua kutorokea mjini Mwambao. Huko maisha hayakuwa mazuri kama yalivyokuwa kwao. Akakosa chakula kizuri, mavazi na hata malazi.

Mwandishi anaeleza kuwa;

> Upenu mdogo wa ukumbi wa udongo mwekundu ulimlaki Yasibu. Ukumbi huu ulikuwa wa futi kumi na mbili urefu na futi kumi na moja upana. Pembeni palikuwa na mtungi wa maji. Katikati ya ukumbi huu kilisaki kiti nyuma ya kimeza cha miguu iliyokongoka misumari ikaregarega. Mafiga matatu yaliimarishwa pembe nyingine ya ukumbi, sanduku bovu la vyombo likiwa karibu na mafiga hayo. Ilikuwa ni tajriba tofauti sana na ile aliyokulia Yasibu huko kwao. (Uk 117)

Ni dhahiri kuwa, Yasibu anakumbana na hali ngumu ambayo ni ya kimaskini. Vilevile amejipata katika hali hii baada ya kuwa mjamzito na masomo yake kukatizwa.

Dunia pia anajipata katika hali ya umaskini baada ya kukataa kuendelea na masomo. Licha ya kuelezewa umuhimu wa masomo, Dunia aliyapuuza mawaidha hayo na kuacha shule akiwa darasa la nane na kukimbilia mjini asikokujua. Kule alikumbana na hali ngumu sana ya kiuchumi hata akajuta kutoroka kwao. Mwandishi anasema;

> Uamuzi wake wa kuja kuishi mjini Mwambao uliingia hatihati, akajiuliza iwapo ulikuwa wa busara au la. Ghafla, alijipata amevurugika akili, mbele kwatisha kwenda na nyuma hakurudiki. (Uk 152)

Mwandishi ameonyesha jinsi uamuzi wa Dunia ulimtia mashakani na hata akajuta. Hali ikawa ngumu zaidi, akakosa chakula, mavazi na hata malazi baada ya kuibiwa mkoba wake uliokuwa na nguo zake na pesa kidogo alizobeba. Mwandishi anasema kuwa;

> Dunia alishuka vidaraja hadi chini, nje ya jumba, taulo kiuoni. Hakuwa na pesa hata senti moja. Chango zilimnguruma tumboni kwa kukosa kustaftahi, machozi yakamtoka. Akashika njia bila kujua alikokwenda. (Uk 161)

Kutokana na maelezo haya, Dunia anakumbana na changamoto ya umaskini. Yeye mwenyewe amejitia katika hali hiyo kwa kuacha masomo na kukimbilia mjini.

Mpoto anajipata katika hali ya umaskini baada ya kufiwa na wazazi wake. Alilelewa na shangaziye ambaye alifariki hatimaye. Mpoto akawa hana mbele wala nyuma. Akawa mpweke na akakosa mtu wa kumkimbilia. Akaanza kuiba akiwa na umri wa miaka kumi na miwili. Anasema;

> “Wazazi wangu walikufa kwa maradhi yasiyo na tiba ningali mchanga. Nililelewa na shangazi lakini naye akafariki kwa ajali ya gari, nikabaki sina mbele wala nyuma.”(Uk 174)

Vilevile, Fakiri anajipata katika hali ya umaskini baada ya kufiwa na wazazi wake. Fakiri anachukua jukumu la kuwalea wadogo wake kwa kufanya kazi za sulubu akiwa na umri mdogo. Dadake anasema;

> “Nilipoingia darasa la tano wazazi wetu walikufa kwa kufuatana. Fakiri alinichukua tukaja tukaishi hapa.”(Uk 120)

Ni dhahiri kuwa uyatima ni mojawapo ya vyanzo vya umaskini miongoni mwa vijana. Mpoto na Fakiri wanajipata katika hali ya umaskini baada ya kufiwa na wazazi wao.

### 3.1.2 Ukosefu wa Malezi bora

Malezi bora ndio msingi wa maadili mema kwa vijana. Kwa mujibu Jeffrey na Brown (2003), vijana wanapokosa malezi bora kutoka kwa wazazi au walezi, hupotoka kimaadili na hawawezi kukua kijamii au kitabia. Matumizi ya vitisho na kutukanwa havisadii katika kulea watoto. Baadhi ya vijana hukosa malezi bora kwa sababu ya hali ya umaskini. Kwa mujibu wa Naliaka (2012) malezi bora hujumuisha lishe bora, mavazi, makao, elimu na ushauri mwafaka.

Mliwa, katika *Chozi Langu* (2014) ni mfano wa vijana wa kike ambao wanakosa kupata malezi yafaayo kwa sababu ya hali ya umaskini na kubaguliwa kiuana. Mliwa analelewa kwa mtaa duni ambao mazingira ni machafu na pia anakosa chakula wakati mwingine. Mwandishi anasema;

> Nyumba waliokaa akina Mliwa kama nyumba nyingine duni mtaani pale ilikuwa imezama ndani ya kiza kile; haiendi, hairudi, imesimama pale mvua na jua, usiku na mchana. (Uk 130)

Taarifa hii inadhihirisha kiwango cha ukosefu wa makazi bora yanayohuhusisha malezi bora. Mliwa anabaguliwa kiuana na babake mzazi na hivyo anamnyima mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi na amani. Mamake anashindwa kuvumilia dhuluma za mumewe Kajogoo, anaamua kutoroka. Hata hivyo, mtafiti alibaini ya kwamba Mliwa hakuwa na raha haswa anapokumbuka jinsi babake

alivyomtesa mamake. Licha ya hayo, wanafunzi wenzake walikuwa wakimkejeli kuwa yeye hana asili wala fasili jambo lililomkosesha Mliwa amani. Mwandishi anasema;

> Suala kuhusu kufukuzwa na babake ni jambo lililomsumbua moyoni na kumkosesha amani na usingizi. Alikumbuka jinsi mamake alivyoteseka wakiishi na babake Bapa. Alikumbuka wakati mmoja walilala matumbo yakinguruma. Alikumbuka wakati fulani wakilia na kumaliza machozi kwenye visima vyao. (Uk 111)

Hili ni dhihirisho kuwa, mizozo katika ndoa ni changamoto kubwa sana katika ulezi wa watoto. Watoto huathiriwa kisaikolojia na hivyo kuathiri maendeleo yao.

Kajogoo hakuwalea binti zake kwa njia inayofaa. Alimnyima Mliwa nafasi ya kuhudhuria shule kwa kuwa hakuona sababu ya kumuelimisha msichana. Mliwa akiwa na umri wa miaka kumi alikuwa hajaanza kwenda shule. Pia, mizozo aliyokuwa akizua kila mara anaporudi nyumbani iliwapa wanawe wasiwasi. Mliwa anatamani kifo kimchukue badala ya kuona jinsi babake anavyowatesa yeye na mamake. Mwandishi anasema;

> Aliyaita mauti yamchukue kimoyomoyo pale nje alikokuwa…… lakini machozi ndiyo yaliyojibu kwa kumpukutika pukupuku. Alimsikitikia mamake si kidogo ingawa hakuwa na la kufanya kumsaidia katika hali ile. ( Uk 24)

Mtafiti amebaini kuwa ukosefu wa malezi bora humkatisha kijana tamaa ya kuishi. Mliwa anafikiria kujiua kwa sababu ya babake ambaye kila mara anamtesa mamake.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Bwana Mashaka alimpa binti yake Yasibu uhuru wa kupita kiasi. Yasibu akautumia uhuru huo vibaya kwa kujiingiza katika mahusiano yasiyofaa ya kimapenzi na pia akawa anarudi nyumbani usiku. Aidha babake hakujali jinsi Yasibu alivyokuwa anatembea. Hakujali anatembea wapi na nani.

Bwana Mashaka anapogundua kuwa matokeo ya Yasibu ya mtihani yamezorota, na ubaradhuli wake kwa wazazi umepita kiasi, anaamua kubadilisha amri zake kwa kutomruhusu Yasibu kutoka nje tena. Maneno haya yanamghadhabisha Yasibu na hivyo anatishia kujitia kitanzi. Anasema kuwa;

> "Ni afadhali mtu anywe sumu afe kuliko adhabu kama hiyo". (uk.31).

Kutokana na maneno haya ni bayana kuwa uwelewano kati ya Yasibu na babake umekosekana kabisa. Yasibu naye ameona kuwa njia mbadala ni kujitia kitanzi. Aidha babake, Bwana Mashaka hakuziba ufa mapema na sasa anataka kujenga ukuta ambao umeshabomoka, jambo ambalo ni ngumu mno. Bwana Mashaka alitumia vitisho kumrekebisha Yasibu. Hakutumia busara. Uhuru wa aina hii kwake Yasibu haukufaa kamwe kwani baadaye anapata ujauzito na kuacha kuendelea na masomo.

Bwana Mashaka anamlea Dunia kwa njia ya vitisho na chuki. Anamtusi kila wakati na kumlaumu Dunia kwa kila jambo ndogo. Hata Dunia apojirudi na kuomba msamaha, Bwana Mashaka anakosa kumsamehe. Dunia alipokosa mapenzi kwao nyumbani, alipania kuyatafuta kwa rafikiye Pazia ambaye alipata nafasi

kumghilibu. Akaanza kutumia dawa za kulevya na akaacha kwenda shule. Mwandishi anasema;

> Kwa babake kukosa kumfungulia milango ya uhusiano bora naye, Dunia alimgandama tena Pazia. Pazia akamkaribisha Dunia kwa mikono miwili, kwa vifijo na nderemo. Polepole Dunia alirudia utumiaji wa vileo. (Uk 122)

Mtafiti amebaini kuwa kutokana na kutomwamini Dunia kuwa amebadilika, Bwana Mashaka alimfukuza zaidi Dunia ambaye alitafuta mapenzi kwa rafikiye Pazia. Naye Pazia akatumia nafasi hiyo kumghilibu Dunia.

Vilevile, Bwana Mashaka anakosa kuwajibika katika kuwalea wanawe wakati wanakataa kumlipia Dunia karo ya shule. Licha hayo, hamshughulikii Dunia kwa vyovyote hata wakati anapougua homa kali, babake anakosa kumjulia hali na badala yake kumrushia matusi tu. Jambo hili linamfanya Dunia kujihisi mpweke. Mwandishi anasema;

> Mbali na maradhi yaliyomsibu, Dunia aliumwa na jambo jingine moyoni. Hakuelewa ni kwa nini babake Bwana Mashaka, hakumsamehe. Ijapo alimkosea babake kwa kukosa kwenda shuleni, na mambo mengine ya utovu wa nidhamu, hakuelewa ni kwa nini hangeulizwa ili akiri makosa na aombe msamaha. Aliishi na babake kwa nyumba bila mapenzi. (Uk 35)

Kutokana na kauli hii ni dhahiri kuwa Bwana Mashaka alitumia adhabu kali zaidi kuwarekebisha wanawe. Hakuweka mipaka katika kuadhibu wanawe.

### 3.1.3 Ukosefu wa Elimu bora

Elimu ni mafunzo yanayotolewa kwa jamii, darasani au pasipokuwa darasani. (TUKI, 2004). Elimu imekuwepo tangu mwanzo hata kabla ya ujio wa ukoloni.

Vijana walipata mafunzo kutoka kwa wazee wao kwa njia mbalimbali kwa mfano, kupitia kwa nyimbo, vitendawili na ngano. (Odaga, 1985). Hivi sasa elimu inayofunzwa vyuoni inatarajiwa kufunza maadili miongoni mwa vijana na si kupata ajira tu.

Licha ya elimu ya shule ya msingi kuwa bure nchini Kenya, bado kuna changamoto chungu nzima kuhusiana na suala hili kwani kuna vijana wengi ambao hawahudhurii shule. Ubaguzi wa kijinsia pia ni changamoto kwa watoto kwani kuna wazazi ambao hawaoni umuhimu wa kuwaelimisha wasichana. Katika *Chozi Langu* ( 2014) Mliwa ananyimwa nafasi ya kwenda shule kwa sababu babake haoni umuhimu wa kumuelimisha msichana. Mwandishi anasema;

> Ingawa ana miaka kumi, kwenda kwake shuleni kuligeuka kwa bahati nasibu. Alipohitimu umri wa kwenda shule, hilo hakujishughulisha nalo babake wala halikumpiga mshipa, kila mara alipoulizwa na Bonuke, alijibu kwa kinaya, ‘kwani hata aila yao huenda shule wakingoja kuchumbiwa?’ (Uk 24)

Kauli hii inaonyesha ya kwamba, Kajogoo anatarajia Mliwa akomae na kuolewa. Wazazi hawaoni haja ya mtoto wa kike kwenda shule. Wanawaoza mapema pindi wanapobalehge.

Katika riwaya hii imebainika kuwa watoto wengi hawahudhurii masomo kwa kuwa hawana karo ya shule.

Mwandishi anasema kuwa;

> Kwingine mtaani, watoto waliotimu umri wa kwenda shule walikuwa wakichezacheza kwa furaha wasijue yaliyowangoja, wenzao wakiwa shuleni. (Uk 9)

Hili ni dhihirisho kuwa watoto hawa hawana matumaini ya kesho na hawatarajii kwenda shule kwa sababu ya umaskini.

Kwingineko tunaelezwa kwamba vijana wengi katika shule ya St. Stephen's akiwemo Mliwa, wanafadhiliwa tu na shule, kwani wengi wao wanatoka mtaa duni na hawangeweza kulipa karo ya shule. Kwa hivyo, wafadhili wa shule hii wanawapa vijana matumaini maishani kwa kuwasaidia kielimu.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* ( 2015), Yasibu anakosa kuendelea na masomo yake akiwa katika darasa la saba. Umri wake ulikuwa miaka kumi na mitano. Hii ni kwa sababu ya kupata ujauzito. Kutokana na chuki ya babake, hakuweza kumsamehe wala kumpa nafasi ya kurudi shuleni. Mwandishi anasema;

> Mzee huyo hakuwa na uhusiano mzuri na mwanawe Yasibu. Alimkasirikia Yasibu kwa kuacha masomo wakati alikuwa akielekea darasa la saba. ( Uk 81)

Kwa mujibu wa Adhiambo (2018) wasichana wanapopata ujauzito, hawakubaliwi tena kuendelea na masomo yao. Hii ni kwa sababu wanaionea aibu hali yao yaani walezi na tena wanafunzi. Aidha, wazazi hawaoni haja ya kuwaelimisha wasichana tena baada ya kupata mimba. Vilevile, walimu huwanyima nafasi ya kuendelea na masomo. Mwalimu mkuu anamnyima Yasibu nafasi ya kuendelea na masomo.

Anasema kuwa;

> Mwanafunzi akipata mimba anayehasirika ni yeye kwani simruhusu tena aendelee na masomo. (Uk 87)

Ni bayana kuwa, wasichana huathirika zaidi wanapopata mimba za mapema kwani masomo yao hukatizwa.

Elimu bora huwakuza vijana kimaadili na kuwaendeleza kimaisha. (Walibora, 2012). Vijana wakiwa na elimu, wataweza kuyasuluhisha baadhi ya matatizo yanayowakumba katika jamii. Hili limejitokeza bayana katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Mwandishi ametilia mkazo zaidi suala hili la elimu kwa kuonyesha umuhimu wake kwa vijana wa kiume kwani hao ndio nguzo katika jamii. Aidha, imedhihirika wazi kuwa bila elimu ya darasani na ya kijamii, hakuna maendeleo yoyote.

Dunia anakataa kuendelea na masomo yake licha ya kufaulu mtihani wake wa darasa la nane. Anaenda kinyume na wazazi, walimu na wazee wa kijiji kwa kukataa ushauri wao kuhusu umuhimu wa elimu. Kutokana na shinikizo kutoka kwa rafikiye Pazia, anatorokea mjini kwa nia ya kuanza maisha yake. Anapofika kule mjini anakumbwa na matatizo mengi sana. Akakosa mavazi, makazi na hata chakula. Akafungwa jela kwa kushukiwa kuwa ni jambazi na baada ya kumaliza kifungo akashikana na rafiki yake Mpoto na kuishi mtaa duni. Mwandishi anasema;

> Dunia na Mpoto waliishi katika mtaa wa Jitengeni, katika kibanda cha mgongo kilichoezekwa makuti ambayo hasa yalichakaa na kufanya matundu mengi paani. (Uk 174)

Ukosefu wa elimu huweza kuwapelekea vijana wa kiume kujiingiza katika visa vya wizi ili kuyakimu maisha yao. Wanapokosa ajira wanatafuta njia mbadala ya kupata pesa. Mpoto anamshauri Dunia waibe kwani hawakuwa na chochote. Jambo hili halikumfurahisha Dunia, anasema kuwa;

> "Aa! sahibu yangu, wanuia tuibe! Kutenda hivyo si uungwana hata kidogo. Uchukuaji wa mali isiyo halali ni wizi na wizi ni kitendo kiovu mbele ya muumba na ardhi na mbingu." (Uk 177)

Fakiri naye anahamia mjini baada ya kumaliza masomo ya darasa la nane. Tunaarifiwa kuwa, hakufaulu mtihani ndiyo maana akaamua kwenda mjini kuatafuta kazi ili awasaidie wadogo wake. Hata hivyo, hakuweza kupata kazi nzuri kwani elimu yake ilikuwa ya kiwango cha chini mno.

### 3.1.4 Uhusiano wa Kimapenzi

Hii ni hali ambapo vijana huwa na uhusiano wa kimapenzi na jinsia tofauti. Ni wakati ambao wengi hawajakua kihisia na hawawezi kudhibiti mihemko ya aina yoyote. Hufanya hivi kutokana na shinikizo la marika au hali mbaya ya kiuchumi. Visa vya uhusiano wa kimapenzi miongoni mwa wanafunzi wa shule za upili na za msingi vimekithiri na vijana wa kike huathirika zaidi.

Mliwa katika *Chozi Langu*, (2014) anakataa maombi ya mwenzake Talimbo ya kuwa mpenziwe. Talimbo anaanza kumrushia matusi. Hilo halikubadilisha msimamo wa Mliwa. Huenda hii ndiyo mojawapo ya sababu zilizomfanya Mliwa kufaulu mtihani wake.

Talimbo anamwambia Mliwa anasema:

> "Talimbo, hilo ni pendekezo zuri lakini huu si wakati wake. Tukimaliza masomo labda ndio tufikirie mambo kama hayo." ( Uk 68)

Kauli hii inaonyesha kuwa Mliwa hakuwa tayari kujiingiza kwa mapenzi ya kiholela. Aliyapa masomo kipaumbele.

Bi. Moyo anaelezea jinsi alishindwa kuthibiti mihemko ya kihisia wakati wa ujana wake. Jambo hili lilifanya aolewe akiwa na umri wa miaka 17. Anasema kuwa;

> "Baada ya kupiga vita vikali na hisia zangu, nilipata nafuu na kukifuta kimya kile kikuu kwa kujikohoza kidogo. Yule kijana aliniangalia mara moja kwa jicho la kusailisaili. Jambo hili lilinichemsha damu hasa macho yangu na yake yalipokutana. Kuna kitu kilichofanyika lakini sikikujua isipokuwa kukihisi. Mara nikajikuta moyo ukinidunda na kunizidia. Mwaka huo nilikuwa nimehitimu umri wa miaka kumi na saba tu!" (Uk 61)

Kulingana na maneno haya, imebainika kuwa, Bi. Moyo hakujua jinsi ya kukabiliana na changamoto hii. Hii ndiyo maana anaolewa akiwa mbichi wakati usiofaa.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), mwandishi ameonyesha athari ya uhusiano wa mapenzi kwa vijana wa kike. Licha ya kupata magonjwa ya zinaa kwa mfano Ukimwi wasichana huweza kupata mimba za mapema na masomo yao hukatizwa huku wenzao wa kiume waliohusika wakiendelea na masomo yao. Yasibu anahusiana na Pazia kimapenzi. Pazia ambaye ni kijana wa kiume wa umri wa miaka 15 mkubwa kidogo kumliko Yasibu anamhadaa kwa kumwambia kuwa

anahitaji uhuru wake na si kufungiwa tu nyumbani na wazazi wake. Pazia anamwambia;

> “Aa! twende nawe Yasibu! Huko twendako kuna raha nyingi, wewe wakaa nyumbani tu kwa nini? Twende kuni pamoja kisha ucheze na vifuu, upike wali wa tanga. Ni lini utakapopoteza taharuki ya kila aina, ukafanya urafiki nasi?”( Uk 21)

Yasibu akamwomba babake ampe ruhusa ya kutoka nje. Babake alikubali lakini Yasibu akaitumia fursa hiyo vibaya. Pazia akatumia nafasi hiyo kwa kumpachika mimba. Masomo ya Yasibu yakakatizwa akiwa na umri wa miaka 15.

Vilevile, mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameonyesha jinsi wazee huwahadaa wasichana wadogo na kuwafanya wajiingize katika mapenzi. Fadhili anamhadaa Yasibu kuwa atamwoa na baada tu ya kumpa mimba anachoka naye na kumfukuza. Zaidi ya hayo anamwambukiza Yasibu ugonjwa wa Ukimwi. Ugonjwa ambao baadaye unamuua Yasibu. Mwandishi anasema kuwa;

> Siku mbili baada ya mazungumzo hayo, maradhi yalimjia juu kama moto wa kifuu. Fakiri na dadake maua walimpeleka hospitalini ya gharama kubwa ili apate afueni lakini afueni isipatikane asilani. Hazikupita siku nyingi Yasibu aliaga dunia. (Uk  201)

Hii taarifa inaonyesha athari ya mapenzi ya kiholela. Yasibu anaambukizwa ugonjwa wa Ukimwi baada ya kuwa na uhusiano na Mzee Fadhili ambaye alikuwa na Ukimwi. Vilevile, katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Pazia anajiingiza katika mapenzi na Yasibu na hatimaye anampachika mimba. Pazia anamchochea Yasibu kumwomba babake amruhusu kutembea na wenzake na hivyo akapata njia

ya kumhadaa Yasibu. Masomo ya Yasibu yanakatizwa ilhali Pazia anaendelea na masomo. Zaidi ya hayo, Pazia anakana kuwa yeye hakuhusika na suala hilo. Anasema;

> "Hiyo mimba si yangu. Sina wasaa mimi wa kumtunga msichana wa shule mimba. Kalitafute fala jingine ulipe mzigo huo." (Uk 93)

Mtafiti amebaini kuwa vijana wa kiume wanapowatunga wenzao wa kike mimba, hao huendelea na masomo ilhali wa kike huacha kusoma ili kulea watoto. Wasichana hupata athari kubwa sana wanapojiingiza katika mapenzi.

Katika *Chozi Langu* (2014) mtafiti amebaini kuwa Talimbo anapomtaka Mliwa akubali ombi lake la kuwa wapenzi, Mliwa kwa busara anakataa ombi lake. Anasema;

> "Talimbo, hilo ni pendekezo nzuri lakini huu si wakati wake. Tukimaliza masomo labda ndio tufikirie mambo kama hayo."(Uk 68)

Kutokana na jawabu hili, Talimbo anakuwa adui mkubwa wa Mliwa. Anamsimanga kila wakati na kumbandika jina 'Mathee.' Talimbo anaona kukataliwa na msichana ni aibu kubwa mno. Hivyo basi, anaanza kumtusi kama njia moja ya kujiondolea aibu.

Mhimili wa nadharia ya Uhalisia unaeleza kuwa fasihi husawiri uhalisia wa maisha katika ngazi zote. Masuala ya mapenzi miongoni mwa vijana wa kike na kiume yamekithiri katika jamii. Wazee kama Mzee Fadhili katika jamii ni wengi mno ambao huwaahidi vijana zawadi mbalimbali iwapo watakubali kuwa na uhusiano

nao. Jambo la kusikitisha ni kuona wasichana wa umri mdogo wananaswa katika mtego huo. Kama samaki ananaswapo kwa chambo kwa ndoana ya mvuvi, wasichana hawa huvutiwa na zawadi na pesa wanazopewa na hawa wazee au kwa kuwapa ahadi kuwa watawaoa, lakini hatimaye wanaambukizwa magonjwa kama vile Ukimwi na mengineyo ya zinaa.

### 3.1.5 Ukosefu wa Usalama

Usalama ni hali ya kutowepo hatari au fujo. (TUKI, 2004). Iwapo kuna mizozo kati ya wazazi, kijana atakosa amani katika mazingira hayo. Baba na mama wasiposikizana humwathiri sana mtoto katika maisha yake. Jambo hilo humpa wasiwasi, hofu na hata kukosa matumaini maishani. Vijana hukosa usalama iwapo watadhulumiwa kwa namna mbalimbali.

Katika *Chozi Langu* (2014), Mliwa hana usalama kwao nyumbani. Hii ni kwa sababu babake mzazi huja nyumbani akiwa amelewa na kumpiga mamake. Jambo hili linamkosesha Mliwa amani na kwa hivyo kwa umri wake huo mdogo anamshauri mamake wahame. Mwandishi anasema;

> Mliwa alirudi kitandani shingo upande akiwa kiu yake haijakatika. Alijifunika blanketi huku moyo na masikio yake yakiwa wazi. Alitaka kujua mbwembwe zote za babake. Alikuwa anafahamu kuwa fika kuwa babake alimtesa sana mamake hasa nyakati za usiku. Jambo hili lilimmyima Mliwa usingizi na amani ya moyo. (Uk 36 )

Usalama unapokosekana nyumbani, mamake Mliwa anakimbia kituoni mwa polisi baada ya kupigwa na mumewe ili wanawe wapate amani. Jambo la kusikitisha ni

kuwa walinda usalama hawakuwa tayari kumsaidia pamoja na wanawe. Kinyume na matarajio walimsuta kwa kuwa kichwa kigumu kwa mumewe. Askari anasema:

> "Hiyo tu? Nilifikiria ni kitu kikubwa! Mama, fanya adabu uende nyumbani. Umemwacha mumeo na nani sasa? Huoni unawatesa watoto kwa baridi hii kali?" (Uk 49)

Mliwa anashikwa na wasiwasi akiwa anatoka shuleni. Mvua kubwa iliyonyesha jioni ile iliwazuia yeye na rafikiye Trufena kwenda nyumbani mapema. Baada ya mvua, Trufena alijiwa na dereva wao ambaye alikataa kumfikisha Mliwa kwao akidai sehemu hizo ni hatari wakati huo. Mliwa anasema;

> "Siku hizi majambazi nao wamezidi. Kwanza ilikuwa kitu kidogo, sasa wanachukua kila kitu yakiwemo maisha yako ukikutana nao!" ( Uk121)

Watu ambao tunatarajia wawape vijana usalama ni wao wenyewe ambao wanahatarisha maisha ya vijana. Viongozi wa kanisa na kiserikali wanafaa kuwapa vijana na watu wengine usalama. Kama wanavyosema Jeffrey na Brown (2003), viongozi wa kanisa wamekuwa wakiwadhulumu sana vijana na watoto. Chifu Moegi ambaye pia ni mzee wa kanisa, anampa ahadi kuwa atampeleka Mliwa hadi kwao usiku huo. Jambo ambalo Mliwa hakutambua ni kuwa huyo Chifu alikuwa mbwa mwitu aliyevalia ngozi ya kondoo. Chifu Moegi alitumia fursa hiyo kumbaka Mliwa. Kama anavyosema Kiprugut (2011), baadhi ya waumini hutumia matatizo ya waumini wenzao kama kisingizio cha kuwadhulumu.

Mwandishi anasema;

> Mliwa aliona ilifaa kupata usaidizi kwa Chifu aliyemjua na kumwamini ili amsindikize kwa gari lake hadi kwao. Alihofu kukutana na majambazi na walaghai waliokuwa wamechukua hatamu janibu hizo za kwao. (Uk 123)

Mliwa anakosa usalama shuleni wakati wenzake wanapombandika jina 'Mathee' 'jungu kuu' na wengine kumwita mamake malaya kwa sababu ya kuachana na babake. Matusi haya yanamuumiza sana Mliwa na anabaki pekee. Kama wanavyosema Jeffrey na Brown (2003), vijana kuitwa majina yasiyofaa ni dhuluma ya kisaikolojia. Pia kijana anapodhulumiwa na wenzake, aidha kwa kumkejeli na kumfanyia masihara, humkosesha amani na hivyo, anaweza kujiona duni, kujiondoa katika vikundi na hata kufikiria kujiua. Wanasema kuwa;

> "Huyu ni 'mathee.' Kwa nini anasoma nasi wadogo tulivyo?" Mvulana mmoja alisema. Malalamiko kama haya hayakumpiga mshipa Mliwa. Hata hivyo, hilo la kuitwa mama' lilimkera na kumkeketa maini kama kisu butu kikatavyo nyama". (Uk 65)

Hii taarifa inaonyesha kuwa Mliwa alikosa usalama shuleni kwa sababu ya umri wake mkubwa.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Yasibu naye aliamua kutorokea mjini alipokosa usalama kwao. Alijaribu sana kumwomba babake msamaha kwa kosa alilolifanya la kupata mimba lakini babake alikataa kumsamehe. Huko mjini alikosa usalama alioutafuta, akapata taabu, akadanganywa na Mzee Fadhili kuwa

angemuoa. Yule mzee akamfukuza baada ya kumwambukiza ugonjwa wa Ukimwi uliomuua Yasibu. Mwandishi anasema;

> Yasibu alitoroka kwao alfajiri, akashika njia. Nyumba yao iligeuka shimo la kutisha lililokuwa ni taabu kuishi ndani. 'Ikiwa kwetu nilimozaliwa mmegeuka handaki la moto, wapi kutanihifadhi?' Yasibu aliwaza. ( Uk 93)

Hii taarifa inaonyesha kuwa Yasibu alikosa usalama kwao nyumbani. Alipofika mjini, hakuweza kupata usalama huko. Ni dhahiri kuwa vijana wa kike huweza kukosa usalama kila mahali wanakoenda.

Mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameonyesha kuwa, usalama unapokosekana nyumbani, vijana wa kiume huweza kukimbilia kwingine ili kupata usalama. Vijana wengi katika umri huu hukimbilia kwa marafiki ili kupata amani. Marafiki wabaya huenda wakawashauri watumie vileo au wajiingize katika ukahaba. Dunia anakimbilia rafiki yake Pazia baada ya ugomvi kati yake na babake. Babake anamtusi kila siku na kumwona kama 'bahati mbaya.' Licha ya Dunia kujaribu sana kuwa na uhusiano mwema na babake, babake anakataa kabisa kumkaribisha. Hivyo, anaazimia kutafuta usalama kwa Pazia rafikiye. Pazia naye anampotosha kwa kumwingiza katika utumiaji wa vileo. Isitoshe, anamshauri aache kuendelea na masomo yake licha ya Dunia kufaulu vizuri sana katika darasa la nane. Mwandishi anasema;

> Dunia alimtumainia Pazia, kwa mambo kadha wa kadha, naye Pazia akamsaidia Dunia, asiweze kumfukuza wala kumpuuza. Alipata nafasi ya kuzidi kumghilibu na kumzuzua. (Uk 82)

Aidha, vijana hasa wa kiume hushukiwa kuwa wezi na askari walinda doria. Dunia anashukiwa kuwa jambazi anapopatikana bustanini akiwa nusu uchi. Askari washika doria hawakumpa nafasi Dunia ajieleze alijipata vipi katika hali hiyo. Ukweli ni kwamba alikuwa ameibiwa kila kitu ikiwemo mavazi na kile alichobaki nacho ni taulo tu. Askari wanamuuliza Dunia;

> "Wafanya nini hapa saa hizi Dunia, tena ukiwa nusu uchi? Wewe ni jambazi! Leo ni leo utalala korokoroni!" ( Uk 163)

Imebainika kuwa, badala ya askari hawa kumpa Dunia usalama, walimshika na kufunga jela kwa tuhuma ya ukaidi. Kule gerezani kunakosa usalama kwake Dunia na wafungwa wengine. Maisha ya Dunia yanakuwa katika hali ya hatari alipokuwa huko. Huko kulikuwa na maambukizi ya magonjwa mbalimbali na mauaji ya wafungwa. Dunia kwa umri wake mdogo, anadungwa kisu kwa kukosa kumpa mfungwa chakula chake. Mwandishi anasema;

> Yule mahabusu alikimbilia jikoni na kumyang'anya kisu mwambuaji viazi akaja akamrarua Dunia usoni, damu ikamfumka. Dunia alikimbizwa hospitalini alikotibiwa kwa wiki zima. ( Uk 207)

Hili ni dhihirisho kuwa Dunia alikosa usalama hata akiwa katika jela

### 3.1.6 Msongo wa Mawazo

Hii ni hali ya hofu na uchovu mtu apatayo baada ya kusongwa na mambo mengi na mazito akilini. Ni mojawapo ya matatizo makubwa sana ya kisaikolojia ambayo vijana hukabiliana nayo. Vijana katika hali hii hujihisi wapweke, kukataliwa na hata kukata tamaa na huweza hata kujitia kitanzi. Hali hii vilevile hutokana na

mambo yanayowaathiri katika jamii. Vijana wa kike huzongwa na mawazo kutokana na sababu mbalimbali kama vile mahusiano mabaya katika jamii na marafiki, mimba za ujanani, matukio ya kuumiza kama vile chuki na ubakaji.

Mliwa anazongwa na mawazo kuhusu babake ambaye aliwafukuza kwao. Wenzake wanamfanyia utani kila wakati wakimtusi jinsi hana asili wala fasili. Wengine wanambandika jina 'mathee' kwa sababu ya umri wake mkubwa kuwaliko. Matusi haya hayakumpa Mliwa utulivu pale shuleni. Mwandishi anasema;

> Shuleni palianza kumwia pagumu. Mliwa alikuwa katikati ya shaki za kilio na kikweukweu kila mara akiwa peke yake. Simango za kuitwa hili na lile kuhusiana na babake zilining'inia kwenye chembe chake cha moyo kama msumari moto kwenye kidonda. (Uk114)

Vijana baleghe huzongwa na mawazo mengi sana kuhusiana na hali zao. Upweke ni tatizo ambalo huwafanya wajione hawana umuhimu wowote maishani. Mliwa anabaki mpweke kwani kila mtu anamtoroka kutokana na hali ya kulelewa na mama pekee.

> Wanafunzi wengi walimkimbia wakamwacha Mliwa peke yake pale shuleni. Wengi wakaogopa kuhusiana naye kwa sababu ya kutaka kuepuka 'mikosi'. Alilia, akalia, akalia. (Uk 115)

Hili ni dhihirisho kuwa Mliwa anazongwa na mawazo kutokana na hali yake ya kulelewa na mzazi mmoja. Vilevile, anakuwa na msongo wa mawazo alipobakwa na Chifu Moegi. Alianza kutembea njiani akizungumza pekee huku akiokota takataka. Mamake anasema kuwa;

> "Juzi amepatikana anazurura sokoni anaokota takataka na kutamka yasiyotamkika". (Uk.182)

Taarifa hii inaonyesha athari ya ubakaji kwa wasichana. Mliwa anapobakwa, wengi wanafikiri amejitia kitanzi. Mamake Trufena anasema;

> "Polisi wameshaeleza wazi kuwa aliyeaga hakuwa Mliwa. Alikuwa binti wa mtu mwingine. Binti huyo alisemekana alijitoa roho kwa sababu ya kufanyiwa unyama na kuchafuliwa na jibaba fulani." (Uk 219)

Utafiti huu umeonyesha ya kuwa msongo wa mawazo unaotokana hasa na ubakaji ni hatari sana miongoni mwa vijana wa kike kwani huweza kusababisha mauko. Huyo binti anayesemeka anajitia kitanzi kwa sababu ya msongo wa mawazo. Huenda alikosa mshauri kwa wakati unaofaa. Aidha, msongo wa mawazo huathiri masomo ya vijana. Kwa mujibu wa mwandishi wa *Chozi Langu* (2014), vigezo vya kuangalia kuwa kijana ako katika hali hii ni hasira, kukosa hamu ya chakula, kulia ovyoovyo, kunyamaza. Mliwa anaacha kwenda shuleni baada ya kubakwa. Hii ni hali ya kukata tama maishani. Mama Trufena anasema;

> "Tulia mwenzangu nikueleze, huzuni, machonzi na mfadhaiko huwa ni ishara muhimu ya kuzingatia katika hali kama hii. Tena, waathiriwa wengi huwa hawana hamu ya kula chakula kando na kukosa usingizi na kuwa na jinamizi." (Uk 220)

Vijana wanapopitia unyama kama huu wengine huweza kunyamaza tu na hawataki kumjulisha mtu mwingine.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), tunaambiwa kuwa, Yasibu hakuwa na raha kutokana hali ya kufungiwa nyumbani. Anakuwa na huzuni na hasira kila wakati. Babake anapomwuliza kile kinachomhuzunisha, anasema kuwa anataka kutembea kama wenzake. Yasibu anasema*;*

> "Ba' nataka n'cheze kama wenzangu. Nataka nende kuni na maji. Nataka nijifulie nguo. Nataka baba n'toke na kurudi nyumbani pasi na kuulizwa." (Uk 23)

Anapotungwa mimba, anakuwa na huzuni na hofu. Anakuwa na upweke kwani anafungiwa kwa nyumba. Zaidi ya hayo, babake mzazi anamchukia na Pazia aliyempa mimba anamkataa. Yasibu anajiona hafai tena kwani hana mtu wa kukimbilia, anaamua kujitia kitanzi tena kwa mara ya pili lakini anaokolewa na Bwana Mafusho. Yasibu anasema;

> "Kwa vyoyote vile sharti nilitekeleze lililonileta huku msituni. Akisimama shinani pa mkuyu, yu tayari kuuparanga hadi kileleni ajirushe na kuyakata maisha yake."( Uk 94)

Msongo wa mawazo huweza kutokana na matatizo katika jamii. Kulingana na taarifa hii, Yasibu anataka kuijitia kitanzi kwa sababu ya mimba.

### 3.1.7 Kubaguliwa Kiuana

Kubaguliwa kiuana ni hali ya kuwabagua watu kwa misingi ya kijinsia. Vijana hubaguliwa kiuana na jamii kwa njia mbalimbali na kwa sababu kadha wa kadha. Kwa mfano katika jamii za Kiafrika msichana amebaguliwa sana na mfumo wa kuumeni. Kama anavyosema Kimani (2003), dhuluma hizi zinawakabili wanawake

kutokana na maumbile yao na kuwa wanaume wanawachukulia kama viumbe duni. Mliwa ni mfano wa msichana anayebaguliwa na babake katika *Chozi Langu* (2014). Babake anamnyima nafasi ya kwenda shule kwa sababu yeye ni msichana. Babake anaona hakuna haja watoto wa aila hiyo kwenda shule. Kwani wataenda tu kuchumbiwa kule shuleni wala si kusoma? Anasema;

> Alipohitimu umri wa kwenda shule, hilo hakujishughulisha nalo babake wala halikumpiga mshipa. Kila mara alipoulizwa na Bonuke, alijibu kwa kinaya. " 'Hata aila yao huenda shule?'"( Uk 24)

Kijana wa kike hubaguliwa hata katika masuala ya malezi. Hao huonekana si watoto na hawana umuhimu wowote katika jamii. Mwanamke anaonekana kama kifaa tu. (Momanyi, 1998). Babake Mliwa hamwoni Mliwa kama mtoto. Bonuke mkewe anapopata mimba ya pili, anaambiwa kuwa;

> "Natumai wakati huu utazaa mtoto. Sina hadi sasa pa kuficha uso wangu. Si kazini, si kijijini kwangu."  (Uk 19)

Kutokana na maelezo haya ni bayana kuwa Mliwa haonekani kama mtoto. Kwa hivyo, anatarajia mkewe azae mtoto wa kiume. Jambo hili linamfanya Mliwa akose malezi mazuri kutoka kwa babake. Kama anavyosema Kezilahabi (2005) watoto wa kike huonekana  kuwa si wa umuhimu katika jamii. Hawapewi nafasi nzuri kama wenzao wa kiume katika baadhi ya jamii. Hao huonekana kama ni mkosi au ni aibu hasa wanapokuwa ni kifungua mimba. Mliwa anaonekana kuwa ni mkosi.

Mwandishi anasema;

> Kuwasili kwa Mliwa duniani kulimkosesha Kajogoo furaha aliyohitaji maishani. Kujaliwa mwana wa kwanza wa aila hiyo ya Mliwa kulionekana kuwa kama mkosi. (Uk 18)

Kajogoo anaona aibu kwa kuwa hana mtoto wa kiume. Kutokana na kujaliwa na mtoto wa kike, Kajogoo anatelekeza familia yake.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) vijana wa kike wanatawishwa. Wavulana wanapopewa fursa ya kutembelea marafiki wao, msichana hufungiwa ndani ya nyumba kufanya kazi za nyumbani. Yasibu anafungiwa nyumbani na hapewi fursa ya kutembea kama Dunia kaka yake. Yasibu anamwambia babake;

> "Sitaki ba! Mimi pia nataka uhuru kidogo tu ba!.......nataka kuwa kama wenzangu. Kwani mimi ni tofauti nao ba!" ( Uk 23*)*

Kutokana na kauli hii, Yasibu haoni tofauti yake na wengine kama Dunia ambao wanapewa fursa ya kutembea ilhali yeye anafungiwa chumbani.

### 3.1.8 Mimba za Ujanani

Vijana baleghe wanapojihusisha katika mapenzi yasiyo halali baadhi ya matokeo huwa kupata ujauzito. Okun (2018) anasema kuwa mimba za mapema miongoni mwa wasichana baleghe ni mojawapo ya matatizo sugu yanayowaathiri wasichana kijamii, kiuchumi, kisiasa na elimu. Mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) anaonyesha mtazamo wa jamii kuhusu wasichana wanaopata mimba za mapema. Wasichana wanapokuwa katika hali hii, huathirika hivi kwamba wanaacha kuendelea na masomo yao ili watunze watoto wao.

Yasibu anapata mimba akiwa na umri wa miaka kumi na mitano tu baada ya kujiingiza katika mapenzi na kijana Pazia. Suala hili linaathiri masomo yake kwani huko shuleni anasinzia darasani, na hatimaye baada ya kujifungua anaacha kwenda shule ili amtunze mtoto wake. Babake anauliza;

> *"*Nina wasiwasi kuhusu binti yetu Yasibu. Afya yake yanipa wayowayo moyoni. Kwani mke wangu humwoni kama amebadilika hali? Wewe wasemaje?"Bi Nusura anajibu: "nisemeje basi na mwanao ni mjamzito?" ( Uk. 76)

Kuacha shule kwa wasichana waliopata ujauzito hutokana na sababu kuwa wanaaibikia hali yao, kwani kutangamana na wengine inakuwa vigumu sana. Sababu nyingine ni kuwa wazazi wa wasichana hawa huchukizwa na tabia hiyo na kukataa kuwalipia tena karo ya shule na pia huenda walimu wakuu kuwakataa tena kuwasajili shuleni. Mwandishi ameonyesha mtazamo wa mwalimu mkuu kuhusu wasichana wanaopata mimba. Anauliza;

> "Takwimu yenye majina ya wanafunzi hao yaonyesha kuwa mwaka huu pekee tumewapoteza wasichana watatu. La kuhuzunisha zaidi ni kuwa wanaotumbukia mtegoni ni wasichana werevu na wenye idili masomoni." ( Uk 90)

Kulingana na mwalimu mkuu msichana ambaye anapata ujauzito hawezi akaruhusiwa tena kuendelea na masomo. Vilevile, mvulana ambaye amehusika katika jambo hilo hafai kurudi shuleni. Mwalimu mkuu anasema;

> "Mwanafunzi akitungwa mimba, anayehasirika ni yeye kwani simruhusu tena aendelee na masomo, hivyo hutokomea na uovu wake". ( Uk 87)

Hii kauli ni kinaya kwani Yasibu anapofukuzwa shule kwa sababu ya kupata ujauzito, Pazia aliyehusika anaendelea na masomo yake.

Kule nyumbani Yasibu hakuwa na amani kwani wazazi wake walimfungia kwa nyumba. Hakuruhusiwa kutoka nje kwani babake aliona kuwa Yasibu alimwaibisha. Babake akamchukia Yasibu na akawa akimtusi kila wakati. Bwana Mashaka anasema;

> "Ameniaibisha. Watoto hawa wameniaziri na kunivunja moyo kwa kususia elimu. Yasibu amekuwa mlezi badala ya mwanafunzi." (Uk 97)

Bwana Mashaka anapata aibu kwa kuwa Yasibu amepata mimba. Haya ni matukio halisi yanayotendeka katika jamii. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Uhalisia, fasihi husawiri uhalisia wa maisha. Mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameweza kutimiza hili kwa kuonyesha changamoto zinazowakumba wasichana katika jamii. Ameonyesha kuwa wazazi na baadhi ya walimu huwa na mtazamo hasi kwa wasichana wanaopata ujauzito. Kwa mujibu wa Siddarth (2018), ripoti iliyofanywa kati ya Juni 2016 na Julai 2017 na Hazina ya Umoja wa Kimataifa ya Idadi ya Watu (UNFP) wasichana 378,398 huacha masomo kwa sababu ya mimba za mapema.

Baadhi ya wasichana wanapokataliwa na wale waliowatunga mimba hufikiria kujitoa uhai. Pazia anakataa kuwa yeye ni mhusika. Jambo hili lilimfanya Yasibu aone ametumbukia katika lindi la giza totoro asijue wa kumwendea ni nani. Anakataliwa na babake mzazi na pia mpenziwe. Kwa hivyo anapoamua kujitoa

uhai anaokolewa na Bwana Mafusho. Haya ni matukio halisi yanayotendeka katika jamii.

### 3.1.9 Dhuluma

Hii ni hali ya kumnyima mtu haki yake au hali ya kumnyanyasa mtu au kumfanyia maonevu. (TUKI, 2004). Kuna aina nyingi za dhuluma, zikiwemo za kimapenzi, kutukanwa, kupigwa na kufanyishwa kazi ngumu. Visa vya vijana wa kike kudhulumiwa vinaripotiwa kila uchao. Haya ni mambo halisi yanayoshuhudiwa katika jamii. Kulingana na mhimili wa nadharia ya Uhalisia, kazi nyingi katika misingi ya kihalisia huangazia ngazi zote kama vile kisiasa, uchumi, utamaduni, na kijamii. Nchini Kenya, visa vya watoto kudhulumiwa vimeripotiwa na vingine havijulikani kwani wahasiriwa huamua kunyamaza tu. Kulingana na ripoti ya Nyamai (2017), watoto kati ya umri wa miaka 6 hadi 15 hudhulumiwa zaidi.

Nyamai (2017) anasema kuwa, vijana baleghe hasa wa kike hudhulumiwa zaidi kimapenzi. Maovu haya hufanywa  na watu ambao ni wa karibu sana kama vile baba, amu, viongozi wa kanisa na wa kiserikali. Wale ambao wanaathirika zaidi ni wasichana wanaotoka katika hali ya kimaskini na yanafanyika wakati wanapoomba msaada kwa viongozi hawa. Katika *Chozi Langu* (2014) mwandishi ameonyesha jinsi wahusika vijana wa kike wanavyodhulumiwa kimapenzi. Hawa ni Mliwa, Maria na binti mmoja aliyejitia kitanzi kwa sababu ya kufanyiwa unyama. Mliwa kwa kuhofia usalama wake anakubali kuingia kwa gari la Chifu Moegi ili afike nyumbani salama. Mliwa alimwamini Chifu Moegi kwa kuwa aliwahi kumfadhili katika masomo yake na pia alikuwa mzee wa kanisa lao. Jambo ambalo Mliwa

hakufahamu ni kuwa Chifu Moegi alikuwa mbwa mwitu aliyevalia ngozi ya kondoo. Chifu Moegi anatumia nafasi hiyo kumbaka Mliwa. Mwandishi anasema;

> Kwa muda, Mliwa alibaki pale gizani maisha yake yamechafuliwa kama nguo nadhifu iliyovamiwa na mwani, ufukweni asubuhi. Ben Moegi naye alikuwa pale ametulia kama mbwa mwitu aliyekwishashambulia vuno pweke akijipongeza taratibu na kufunu mabawa. ( Uk 129)

Vijana wa kike wanapobakwa huathiriwa kiafya na kiakili. Tunaambiwa kuwa baada ya kufanyiwa unyama, afya ya Mliwa ilizorota, akawa hazungumzi na mtu yeyote. Akakataa kwenda shule na akawa anazurura mtaani akiokota takataka. Mamake anasema;

> "Mtoto hasemi lolote… jana nasikia alionekana mjini akiokota takataka na kutema maneno yanayoumiza masikio. Sijui nifanye nini". (Uk 173)

Mliwa ameathirika kiakili na sasa anatembea kama mwenye akili punguani kutokana na dhuluma ya kimapenzi. Aidha, Maria naye hali yake ilibadilika baada ya kubakwa na jirani aliyekuwa na mke na watoto. Tofauti na Mliwa wazazi wa Maria walikubaliana kusuluhisha tatizo hilo kinyumbani. Imebainika kuwa, hii si njia nzuri ya kutetea haki ya wahasiriwa na inatokana na kutowajibika kwa wazazi wa Maria. Yule aliyembaka Maria alifaa kuchukuliwa hatua kali kisheria lakini si kulipa ng'ombe wawili kama fidia. Bonuke anasema;

> "Upuuzi mtupu! Halafu maisha ya Maria? Jamani mtoto mbichi wamemharibia maisha yake ya halafu." (Uk 172)

Imebainika kuwa, vijana wanapodhulumiwa kimapenzi huweza kukosa matumaini ya kuendelea kuishi na hivyo basi wanaamua kujitia kitanzi kwa sababu ya msongo wa mawazo. Katika *Chozi Langu*, (2014), binti mmoja alijitia kitanzi baada ya kubakwa. Aidha, Mliwa anadhulumiwa na Bi. Rai halati wake kwa kufanyishwa kazi ngumu na kunyimwa nafasi ya kudurusu masomo yake ilhali wanawe Bi. Rai wanakaa bwete. Imebainika kuwa Mliwa anafanya kazi zaidi bila kupumzika ilhali umri wake ni mdogo.  Bi. Rai anasema;

> "Mliwa, naondoka. Usisahau kufua nguo na kupiga deki. Halafu uzunguke nyumba yote na uhakikishe kuwa hakuna uchafu. Wakati wa chamcha, upike chakula cha kuwatosha nyie nyote. Halafu uoshe vyombo na kupanga nyumba  vizuri……" (Uk 94)

Hii ni dhuluma kwa Mliwa kwani wenzake walikaa tu yeye akifanya kazi hizi zote. Licha ya kazi hii, walimrushia matusi kila wakati kutokana na hali yao. Mliwa alipoona maonevu haya yamezidi aliona afadhali arudi kwao nyumbani.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Yasibu anadhulumiwa na babake kwa kutukanwa na kutawishwa baada ya kupata ujauzito. Akamfungia kwa nyumba kwani hakutaka atoke nje. Licha ya Yasibu kulalamika, hawakusikia kilio chake. Hata Yasibu alipobadilika na kuomba msamaha kila wakati, babake alikataa kata kata kumsamehe. Hapo ndipo alipoamua kutoroka nyumbani kwao. Mwandishi anasema;

> Nyumba yao iligeuka shimo la kutisha lililokuwa ni taabu kuishi ndani. 'Ikiwa kwetu nilimozaliwa mmegeuka handaki la moto, wapi kutanihifadhi?' Yasibu aliwaza. ( Uk 92)

Vilevile, Yasibu anadhulumiwa kimapenzi na Pazia rafiki ya kakake. Anaanza uhusiano wa kimapenzi na Pazia ambaye anatumia nafasi hiyo kumpachika mimba na mwishowe kukataa kubeba jukumu hilo. Yasibu anaacha shule kutokana na hali yake. Mwandishi anasema;

> Bi. Nusura aliyaona mabadiliko ya mwanawe, akayapeleleza kwa makini sana hadi akatambua yalivyobashiri na yasiyobashiri mambo mazuri kabisa! Alipomdadisi mwanawe kuhusu aliyemleta janga hilo, alishtuka kuambiwa ni Pazia rafikiye Dunia. (Uk 75)

Mzee Fadhili alimdhulumu Yasibu kimapenzi. Mzee Fadhili anamhadaa Yasibu kuwa anampenda. Kutokana na hali ngumu ya maisha, Yasibu anakubali uhusiano huo wa kimapenzi akiwa na matumaini kuwa Fadhili atamtimzia mahitaji yake. Baada ya kuishi naye kwa muda mfupi Fadhili anamfukuza Yasibu bila chochote. Yasibu akatoka kwa Fadhili akiwa na ujauzito na pia akiwa ameambukizwa ugonjwa wa ukimwi.

Vilevile, mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameonyesha kuwa vijana wa kiume huweza kudhulumiwa na wazazi wao au jamii kwa ujumla. Dunia anadhulumiwa na baba yake kwa kutukanwa kila mara. Babake anamwona Dunia kama mtoto ambaye ana nuksi kwani kuzaliwa kwake kulitokana na mamake kupigwa dafrao na fahali, na hivyo Dunia akazaliwa kabla ya siku zake kutimia. Kwa hivyo, babake akawa na chuki zaidi kwake. Bwana Mashaka anasema;

> “Kuzaliwa kwako kulibashiri maafa na maangamizi. Nami nayaona maafa ndiyo haya na kuangamia ndiko huku”. (Uk 101)

Dunia anadhulumiwa na babake wakati alikataa kumlipia karo ya shule. Baada ya Bwana Mashaka kuaambiwa kuwa Dunia haendi shule, alikasirika zaidi na kukosa kumlipia karo ya shule hata baada ya Dunia kubadilika. Alipogunduliwa, alipata ushauri kutoka kwa mwalimu mkuu na akakubali kurudi shuleni. Hata hivyo, baba mzazi hakumwamini tena Dunia. Akaendelea kumrushia matusi na kumwona kama mjalaana.

Dunia anadhulumiwa akiwa gerezani kwa kufungiwa kwa chumba kidogo kilichojaa kunguni. Alipokuwa mgonjwa alistahili kutoa hongo ili apewe matibabu. Mwandishi anasema;

> Alinyolewa kwa wembe butu, akayastahamili maumivu pale wembe huo ulipochuana na ngozi. Mahabusu walidhulumiana wakaonyeshana kiburi. (Uk 167)

Kauli hii inaonyesha jinsi wafungwa hudhulumiwa na askari wakiwa gerezani. Pia, wafungwa wenyewe kwa wenyewe hudhulumiana.

### 3.1.10 Matumizi ya Mihadarati

Dawa za kulevya miongoni mwa vijana ni jambo ambalo limekithiri sana. Dawa za kulevya huharibu akili, na pia hudhoofisha mwili wa mtumiaji. (Chesang, 2013). Kwa hivyo, vijana ambao wanatarajiwa kuwa viongozi wa kesho watashindwa kutekeleza majukumu hayo kwa sababu hawatakuwa na fahamu nzuri na afya nzuri iwapo watafika umri huo. Hii ni kwa sababu baadhi yao hufa kutokana na athari ya dawa za kulevya.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha kuwa matumizi ya dawa za kulevya miongoni mwa vijana wa kiume ni hatari mno kwa sababu huvuruga akili na kumfanya kijana kukosa maadili. Dunia anakuwa mtovu wa nidhamu baada ya kuvuta bangi. Hata baada ya kufaulu vyema sana katika mtihani wa darasa la nane, anapata ujasiri wa kukataa kujiunga na shule ya upili hadharani. Hakujali tena hisia za babake, licha ya babake na walimu wake kumwomba aendelee na masomo. Yeye anaona hiyo ndiyo njia moja ya kumwadhibu mzee wake ambaye hakuwa na haja naye wakati huo na ambaye hakumlipia karo ya shule. Anasema;

> "Sina hamu ya kusoma. Sina hamu maana sioni faida yake. …….siwezi kumfadhili baba fadhili ambazo hakunifadhili." ( Uk 137)

Kauli hii inaonyesha kuwa uamuzi wa Dunia wa kutoendelea na masomo ulichochewa na matumizi ya dawa za kulevya na malezi mabaya. Bwana Mashaka alimtelekeza sana Dunia jambo ambalo lilimuumiza sana. Dunia anaona kuwa babake anampenda tu wakati anafaulu mtihani.

Dunia anatorokea mjini Mwambao. Maisha kule mjini hayakuwa rahisi kwake. Akawa anafungwa jela kila mara hata pasipo na makosa. Mateso yalivyozidi anagundua kuwa kweli amejiharibia maisha. Akiwa mahakamani, Hakimu anamuuliza;

> "Umri wako ni mdogo. Siku hizi vijana wengi wanatoroka vijijini na kukimbilia mijini bila kazi wala bazi. Huselelea mjini hadi wakawa wezi, wanyang'anyi na watumiaji wa mihadarati na kadhalika. Wewe ni miongoni mwa vijana hao. Kwa nini hauko shuleni? Bila shaka wewe ni mkora!" (Uk 171)

Ni wazi kuwa Dunia alifaa kuwa shuleni na wala si mjini Mwambao akizurura. Kulingana na hakimu umri wake ni mdogo sana na akiwa hayuko shuleni basi anafaa kuwa jela kwa sababu kama anavyosema kuna vijana kama Dunia ambao kazi yao ni kuzurura tu wakitafuta vya kuiba na kutumia mihadarati.

Kwa kuzingatia nadharia ya Uhalisia, mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameangazia madhara ya dawa za kulevya kama yanavyojitokeza katika jamii halisi. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Uhalisia kuwa fasihi husawiri uhalisia wa maisha, mwandishi amefichua athari mbaya zinazotokana na utumiaji wa dawa za kulevya. Vijana hufikiria kuwa wanapojiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya watapunguza mawazo huku wakipuuza madhara yake. Stringer (2017) anasema kuwa shinikizo la marika ni mojawapo ya mambo yanayowafanya vijana hasa wa kiume kuanza matumzi ya mihadarati. Kwa sababu ya shinikizo la rika vijana wengi hutaka kujaribisha kila kitu. Dunia anaanza kutumia vileo kutokana na ushawishi wa Pazia.

Pia mambo yanayochangia matumizi ya dawa za kulevya ni ukosefu wa mwelekeo bora, mizozo ya nyumbani, matokeo mabaya shuleni na kujistarehesha. Lakini baada ya kurudi katika hali yao ya kawaida, wanakuta bado kuna yale matatizo hata zaidi. Dunia anaanza kutumia vileo wakati kuna mgogoro kati yake na babake. Babake anamchukia Dunia na kila afanyapo kosa hata bila kukusudia, babake anamkumbusha kuwa kuzaliwa kwake kulikuwa na dosari. Hapo ndipo Pazia rafikiye anaipata fursa hii ya kumfunza matumizi ya dawa za kulevya.

Mwandishi anasema;

> Dunia alianza uraibu wa sigara na akaingilia madawa mengine ya kulevya kutoka kwa rafikiye Pazia……….Pazia mwenyewe hakuyatumia madawa haya kulevya asilani! ( Uk 32)

Kwa maoni ya Cosby, Rick, Charlie, Clement, na Barbara (2000) mojawapo ya changamoto kubwa sana miongoni mwa vijana baleghe ni shinikizo la kutumia dawa za kulevya. Baadhi yao huanza kutumia pombe au sigara kwa sababu wanafikiria kuwa wataonekana 'wakubwa.' Madhara ni kuwa vijana hawa hushindwa hata kuhudhuria vipindi vya masomo shuleni.

### 3.1.11 Vifungo vya Jela na Vizuizi

Vijana katika umri huu huweza kuzuiliwa kwa sababu mbalimbali kama vile matumizi ya dawa za kulevya, ubakaji, wizi na ukatili kama vile mauaji. Hata hivyo, kuna vijana wengine ambao hufungwa jela bila makosa yoyote na hata huuliwa. Jambo la kusikitisha ni kwamba inapogunduliwa baada ya kuua vijana hawa, hakuna hatua inayochukuliwa kwa waliowaua. Kulingana na Stringer (2017), lengo la vijana baleghe kuzuiliwa ni kuwafunza maadili ili warudi katika jamii na waendelee na masomo yao. Hivyo basi, adhabu kali kama mauaji au kifungo cha maisha haifai.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha kuwa vijana wa kiume hukumbwa na changamoto hii katika jamii. Dunia alifungwa mara mbili kwa makosa ambayo hakufanya. Dunia aliibiwa mkoba wake uliokuwa na pesa na nguo akiwa msalani akioga. Hali hii ikamfanya atembee bila nguo isipokuwa tu taulo

aliyokuwa nayo. Wakati alipohisi uchovu na njaa alilala bustanini na hapo askari wakatokea na kumshuku kuwa mwizi. Ingawa Dunia alijitetea hawakumsikiliza na walimpeleka mahakamani. Hii ikawa mara ya kwanza kwake Dunia kufikishwa mahakamani. Hakimu anasema;

> "Umri wako ni mdogo. Siku hizi vijana wengi wanatoroka vijijini na kwenda mijini bila kazi wala bazi. Huselelea mjini hadi wakawa wezi, wanyang'anyi na watumiaji wa mihadarati. Wewe ni miongoni mwa vijana hao. Kwa nini hauko shuleni? Bila shaka u mkora!" (Uk171)

Mtafiti amebaini kuwa, Dunia anashukiwa kuwa mkora kutokana na umri wake na hali yake. Kwani katika umri huu alifaa kuwa shuleni si kuzurura mitaani. Ingawa Dunia alijitetea, hakusikizwa kamwe. Hakimu anaamua kuwa mahakama imempata na hatia na kwa hivyo anafungwa gerezani kwa miezi sita. Katika jamii, vijana huhukumiwa hata kifo bila hatia. Wengine huzuiliwa kwa miaka kadhaa pasipo na hatia. Dunia ni kielelezo cha vijana wa kawaida katika jamii.

Mpoto anashikwa kwa sababu ya wizi. Anaanza kuiba kutokana na hali ngumu ya maisha baada ya kufiwa na wazazi wake wote. Kama anavyosema Stringer (2017), vijana baleghe hufanya makosa kutokana na aidha hali ngumu ya maisha, kutelekezwa kwao au kushinikizwa na wenzao. Mpoto anasema;

> "Nilianza kazi hii ya wizi nikiwa na miaka kumi na miwili. Hakuna askari Mwambao asiyenijua." (Uk 173)

Hii ni dhahiri kuwa Mpoto alianza kuiba kutokana na hali ngumu ya maisha.

## 3.2 Suluhu kwa Changamoto Zinazowakumba Vijana Katika *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015)

### 3.2.1 Umaskini

Katika *Chozi Langu* (2014), mtafiti amebaini kuwa, bidii na hamasisho imesawiriwa kama moja kati ya njia zinazoweza kuwasaidia vijana kujikwamua katika lindi la umaskini. Aidha, elimu ni mojawapo ya suluhu kwa changamoto ya umaskini. Hili linadhihirika kupitia kwa mhusika Mliwa ambaye anatia bidii masomoni na pia anapata motisha kutoka kwa mamake mzazi na wenzake. Mambo haya yanamsaidia katika kufaulu kwake. Tunaambiwa;

> Mliwa alikuwa amepewa kazi nyingi sana za ziada shuleni. Alijua kuwa mtihani ambao angeufanya mwezi wa mwisho wa muhula huo ulikuwa muhimu sana katika maisha yake ya masomo. Alihitaji kujitoa katika hali ya familia yake na kumuani mamake. (Uk.118)

Kauli hii inaonyesha kuwa bidii ni mojawapo wa njia zinazoweza kutoa vijana katika lindi la umaskini.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), mwandishi ameonyesha kuwa, baada ya kifungo, Dunia na rafiki yake Mpoto wanajipata katika hali ngumu ya maisha. Hata hivyo, hawakati tamaa. Wanafanya kazi kwa bidii ili waweze kubadilisha hali hii. Mwandishi anasema;

> Dunia na rafikiye Mpoto walidhamiria kuyabadilisha maisha waliyoishi. Sasa walirauka kila siku wakaingia bandarini na madukani kufanya uhamali wa kila aina. Hakulala njaa tena. Ugumu wa maisha ulianza kupungua polepole. (Uk 177)

Taarifa hii inaonyesha kuwa bidii walioifanya iliwasaidia kutimiza mahitaji yao ya kila siku. Kutokana na maelezo ya mwandishi, vijana wanaweza kusuluhisha changamoto ya umaskini iwapo watatia bidii kwa kazi wafanyazo. Maisha ya Dunia na Mpoto yalibadilika kutokana na bidii waliofanya. Licha ya kukosa elimu ya kutosha, hawakufa moyo bali waliona njia moja tu ya kujikwamua kutoka katika hali ya umaskini ni kufanya kazi kwa bidii.

### 3.2.2 Ukosefu wa Malezi bora

Katika *Chozi Langu* ( 2014) Mliwa alikosa chakula na amani kwa sababu ya ugomvi uliokuwepo kati ya wazazi. Mamake anapoachana na babake, Mliwa anaendelea kusoma na kufaulu kila wakati lakini bado hana raha kwani wenzake wanashinda kumkumbusha hali yake. Mliwa anapata mawaidha kutoka kwa rafiki yake Mawazo. Mawaidha haya yanamsaidia na hivyo anakuwa na mbinu ya kukabiliana na changamoto hiyo. Mwandishi anasema;

> “Mawazo haya yalimjenga upya na kumpa mwelekeo na mwamko mpya. (Uk 11)

Hili na dhihirisho kuwa, hata ingawa Mliwa alikosa malezi ya babake mzazi, mamake alimpa mawaidha ya kila mara yaliyomjenga. Vile vile vijana wenzake kama vile Trufena na Maliwazo walimpa mawaidha. Akapata mtazamo mpya kuhusu maisha yake.

Katika *Dunia Mashaka Makuu*(2015) mwandishi ameonyesha kuwa Yasibu anakuwa na huzuni mwingi sana hasa anapoona wasichana wenzake wakijifanyia mambo ilhali yeye ametawishwa. Kama anavyosema Akoth (2018) wasichana

hutaka kuigiza wenzao kwa kila jambo. Anapopewa uhuru, anautumia uhuru huo vibaya kwa kurudi nyumbani usiku na kukosa heshima kwa wazazi hasa mamake. Kwa mujibu wa Mureithi (2016), vijana hupotoshwa na uhuru uliopita mipaka kwa kufanya watakavyo.

Kwa mujibu wa Jeffrey na Brown (2003), wasichana katika umri huu wanafaa kuelekezwa ipasavyo, na iwapo wanapewa uhuru, uwe na mipaka. Pia, wazazi wanafaa kujua watu wanaotangamana nao na wanatumia vipi muda wao.

Bwana Mashaka alitumia adhabu kali zaidi kuwarekebisha wanawe. Hakuweka mipaka katika kuadhibu wanawe. Kulingana na McNeely na Blanchard (2009), adhabu kali haifai kwani husababisha msongo wa mawazo kwa vijana. Bila kutumia busara wanawe wawili walichanganyikiwa na kupoteza mwelekeo maishani. Dunia anapokosa mapenzi ya babake, anaamua kutafuta suluhu kutoka kwa rafikiye Pazia. Mwandishi anasema;

> Dunia alimtumainia Pazia, naye Pazia akamsaidia Dunia, asiweze kumfukuza wala kumpuuza. Alipata nafasi ya kuzidi kumghilibu na kumzuzua. (Uk 82)

Kulingana na maelezo ya mwandishi, uamuzi ambao Dunia alichukua haukuwa mzuri kwani Pazia alimshauri Dunia aache masomo yake kama njia moja ya ‘kumwadhibu’ babake kwa kumtelekeza. Wazazi hawafai kutumia adhabu kali kwa wanao. Akoth (2018) na Adhiambo (2018) wanasema kuwa, wazazi wanafaa kuwaelekeza kwa upendo na kuwa tayari kuwasamehe vijana wanapoteleza maishani. Ni vyema wazazi kutangamana na vijana ili kuielewa mitindo yao ya

kimaisha hivi kwamba ikibadilika wajue kuwa imebadilika na hivyo basi mzazi atajua jinsi ya kumwelekeza.

### 3.2.3 Ukosefu wa Elimu bora

Katika *Chozi Langu* (2014**)** tunaelezwa kwamba vijana wengi katika shule ya St. Stephen's akiwemo Mliwa, wanafadhiliwa tu na shule, kwani wengi wao wanatoka mtaa duni na hawangeweza kulipa karo ya shule. Kwa hivyo, wafadhili wa shule hii wanawapa vijana matumaini maishani kwa kuwasaidia kielimu. Mwandishi anasema;

> St. Stephen's ilikuwa shule iliyowasaidia wanafunzi wengi kutoka mitaa duni ukiwemo mtaa wa Mwembe kupata angaa kisomo siku hizo na kujidai kuwa waliwahi kuziona kuta za shule ya upili. Ikawa ndiyo shule iliyomvaa na kumfaa Mliwa. (Uk144).

Mliwa anapopata nafasi hii anatia bidii katika masomo. Tunaambiwa kuwa alifaulu katika mitihani na pia akakuza kipawa chake cha utunzi wa mashairi. Mwandishi anasema;

> Mliwa alipopewa nafasi hii, alifahamu barabara kuwa juhudi zake ndizo zingemfungulia milango zaidi ya ufanisi maishani. Kwa sababu hii alipenda kujaribu kila kitu kuona matokeo yake. (Uk 65)

Elimu ni nguzo muhimu kwa vijana kwani kupitia elimu, vijana wataweza kutatua baadhi ya matatizo yanayowakumba. Mwandishi ameonyesha jinsi Mliwa alipojinyakulia kazi ya utangazaji baada ya kufuzu katika chuo kikuu. Vilevile, dadake Chanda anapata kazi ya uuguzi katika hospitali kuu ya Nyikani. Chandeka naye anapata kazi ya ualimu katika shule ya sekondari.

Kulingana na  mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Dunia alikosa elimu bora kwa kutozingatia ushauri wa wazazi wake. Baada ya kuacha masomo, anajikuta katika hali ya umaskini kwani hakuwa na ajira. Vilevile, Fakiri anaacha kuendelea na masomo kwa sababu hakufaulu vyema katika darasa la nane. Anakimbilia mjini na kuanza kufanya kazi za sulubu zenye mapato ya chini sana. Kwa upande mwingine, masomo ya Mpoto yanakatizwa baada ya kufiwa na wazazi wake. Ukosefu wa elimu huweza kuwapelekea vijana kujiingiza katika visa vya wizi ili kuyakimu maisha yao. Mpoto anakosa mfadhili na ndio maana anaanza kuiba.

Hata hivyo, mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameonyesha kuwa vijana hawafai kukata tamaa au kutumia mbinu mbaya za kutafuta mapato. Dunia na Mpoto walifanikiwa licha ya kukosa elimu bora kwa kutia bidii katika kazi walizozifanya. Licha ya ujira mdogo waliweza kuweka akiba na wakakodisha nyumba nzuri. Mwandishi anasema;

> Dunia alikodisha chumba ndani ya nyumba nzuri mtaa wa kadiri. Mavazi yake yakabadilika. Sasa alitembea amevalia suti na buti.(Uk 178)

Wazazi wanafaa kuwahimiza wanao kufanya vyema katika masomo yao ili watimize ndoto zao. Kulingana na mwandishi, Dunia alikosa mwelekezi katika suala la elimu kwani babake hakustahili kukosa kumlipia karo ya shule.

### 3.2.4 Uhusiano wa Kimapenzi

Katika *Chozi Langu* (2014) mtafiti amebaini kuwa Mliwa alielewa athari ya uhusiano wa mapenzi katika umri huo na hakutaka aathirike kimasomo. Kuwa na uhusiano wa mapenzi unafaa kuwa kwa wakati unaofaa. Talimbo anapomtaka Mliwa akubali ombi lake la kuwa wapenzi, Mliwa kwa busara anakataa ombi lake. Anasema;

> "Talimbo, hilo ni pendekezo nzuri lakini huu si wakati wake. tukimaliza masomo labda ndio tufikirie mambo kama hayo."(Uk 68)

Vijana wanafaa kuelewa hili ili wasije kuyaharibu maisha yao. Athari ya mapenzi ya kiholela huweza kusababisha vifo. Kulingana na Adhiambo (2018), wazazi wanafaa kuongea na vijana ili waweze kujua jinsi ya kukabiliana na hisia za kimapenzi.

### 3.2.5 Ukosefu wa usalama

Katika *Chozi Langu* (2014) Mliwa anakosa usalama shuleni anapotusiwa na wenzake kila mara kwa sababu ya umri wake mkubwa. Hata hivyo, anapata mbinu mpya ya kukabiliana na changamoto hiyo baada ya kushauriwa na Maliwazo. Akayapuuza yale majina waliombandika. Anasema;

> "Potelea mbali. Watasema mchana lakini usiku watalala. Nitaendelea kujikuza kwa kila hali na namna."(Uk 116)

Hii ikawa falsafa yake mpya kwa muda kila mara aliposikia baya likisemwa kumhusu. Vilevile, Mliwa anakuwa katika hali ya hatari wakati alipokuwa akitoka

shuleni usiku anapobakwa na Chifu Moegi. Hata hivyo, Mliwa anakabiliana na changamoto hiyo kwa kupata ushauri kutoka kwa wataalamu kama Mama Trufena. Anakubali kurudi shuleni na kuendelea na masomo yake. Chifu Moegi naye anachukuliwa hatua ya kisheria. Kwa mujibu wa McNeely na Blanchard (2009), ni muhimu kuzingatia mazingira ambamo vijana wanaishi na kushughulikia hatari zinazowakumba vijana katika yale mazingira. Wahalifu wote wanafaa kuchukuliwa hatua kisheria kama njia moja ya kupunguza visa vya ubakaji na vinginevyo ambavyo ni hatari kwa vijana.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Dunia anapokosa usalama kwao nyumbani wakati babake anamwita “mkosi,” na kulaumiwa kwa kila jambo, anaamua kumkimbilia rafiki yake Pazia kama njia ya kutafuta suluhu ya changamoto hii. Hatua hiyo haikuwa nzuri kwani Pazia alimghilibu Dunia kwa kumfunza matumizi ya dawa za kulevya. Kulingana na Dacey na John (2003) kijana anapokosa usalama kwao nyumbani huweza kukimbilia kwa marafiki wake ambao mara nyingi huwapotosha wenzao. Dacey na John (2003) wanasema kuwa wazazi wanafaa kuwa karibu na wanao ili wafahamu mabadiliko yanayotokea. Vilevile wanafaa kuwaonyesha wanao mapenzi na wawape mawaidha hasa wanapoteleza.

### 3.2.6 Msongo wa Mawazo

Mliwa katika *Chozi Langu* (2014) anazongwa na mawazo kutokana na hali yake ya kulelewa na mama pekee. Hata hivyo, mwandishi anasema ya kwamba hali hii ndiyo iliyompa Mliwa nguvu zaidi ya kusoma. Hasa alipopata ushauri kutoka kwa rafikiye Mawazo, alipata nguvu mpya na suala hili halikumpiga mshipa tena, kwani

alitafuta mbinu ya kukabiliana na wale wanaomtusi. Alijua lengo lake la kuwa pale shuleni. Mwandishi anasema;

> Mahasidi wa Mliwa pale shuleni walishangaa ghaya walipoona kuwa maneno waliyozua hayakumpiga mshipa hata chembe. Walishangaa kumwona kasimama imara hata masomoni mwake tena. Mawazo hakusita kumwauni kwa wazo hili ama lile palipohitajika. ( Uk 116)

Ni dhahiri kuwa Mliwa alipata mbinu ya kukabiliana na changamoto hii kupitia kwa ushauri aliopewa na rafikiye Mawazo.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha jinsi Yasibu alikuwa kijana mnyonge sana katika kukabiliana na changamoto hii ya kuzongwa na mawazo. Mwandishi anasema kuwa baada ya kukataliwa na Pazia aliyempachika mimba na pia babake kumchukia zaidi, Yasibu aliona heri ajiue. Hii si njia nzuri ya kukabiliana na changamoto hii. Hivyo basi, walimu na wazazi wanafaa kuwapa vijana kama hawa matumaini tena hata baada ya kuteleza.

### 3.2.7 Kubaguliwa Kiuana

Katika *Chozi Langu* (2014) mwandishi ameonyesha kuwa vijana wa kike hawapewi nafasi kama wenzao wa kiume katika baadhi ya jamii. Babake Mliwa anamwona Mliwa kama mkosi kwani alitarajia mtoto wa kiume. Hata hivyo, mamake Mliwa aliendelea kumshauri mwanawe na pia akampeleka shuleni. Mwandishi anasema;

> Kuwasili kwa Mliwa duniani kulimkosesha Kajogoo furaha aliyohitaji maishani. Kujaliwa mwana wa kwanza wa aila hiyo ya Mliwa kulionekana kuwa kama mkosi. (Uk 18)

Hata hivyo, Mliwa hakukata tamaa. Alipopata fursa ya kusoma, alitia bidii masomoni na kufaulu maishani. Alionyesha babake kuwa mtoto wa kike si 'mkosi' kama alivyodhaniwa bali ni baraka. Alipofuzu katika chuo kikuu alipata kazi ya utangazaji kwenye kituo maarufu.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Yasibu anabaguliwa kiuana na babake ambaye anamfungia chumbani. Hata hivyo, Yasibu kwa ujasiri anamwomba babake apewe ruhusa ya kutoka. Anamwambia babake;

> "Sitaki ba! Mimi pia nataka uhuru kidogo tu ba!.......nataka kuwa kama wenzangu. Kwani mimi ni tofauti nao ba!" ( Uk 23*)*

Hata hivyo, hakuutumia uhuru huo kwa njia ifaayo. Anapata mimba na kuacha shule. Kwa mujibu wa Cherry (2017), wazazi wanafaa kuwa waangalifu sana vijana wanapotaka uhuru. Wanafaa kujua vijana hawa wanatembea na nani au wanafanya nini.

### 3.2.8 Mimba za Ujanani

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha jinsi baadhi ya vijana hushindwa kukabiliana na changamoto ya mimba za ujanani. Kuna baadhi ya vijana ambao huamua kuavya mimba kama njia ya kutatua tatizo hili na wengine hata hutaka kujiua. Hii hutokana na chuki wanayopata kutoka kwa wazazi na pia kukataliwa  na wapenzi wao. Yasibu anaona maisha yake yamefika mwisho baada ya kukataliwa na Pazia mpenziwe. Yasibu akahisi maisha yake yametumbukia kwenye giza totoro asitambue apitie wapi. Anapoamua kujitia kitanzi, anabadilisha

msimamo wake baada ya kusikia mashauri kupitia kwa wimbo wa Bwana Mafusho. Anasema;

> Khaa! Siyakati maisha yangu. Nitajaribu namna nyingine ya kuyakomesha mateso haya. Ikizidi mwanangu Yadhuru ningemwachia nani? (Uk 95)

Ni dhahiri kuwa Yasibu aliona kujitoa uhai si njia ya kusuluhisha changamoto inayomkumba. Anaona atafute mbinu tofauti. Kwa mujibu wa Akoth (2018), bila ushauri mwafaka kwa wasichana baleghe, wanaweza kujiingiza katika uhusiano wa mapenzi mapema na matokeo yawe ujauzito au maambukizi ya magonjwa ya zinaa. Akoth (2018) anasema kuwa, wasichana wanafaa kuelimishwa kuhusu madhara ya mapenzi na athari ya kufanya mapenzi kiholela.

### 3.2.9 Dhuluma

Katika *Chozi Langu (*2014) mwandishi ameonyesha jinsi vijana wa kike hutoa suluhu kwa changamoto zinazowakabili. Baada ya Mliwa kubakwa na Chifu Moegi, anaathirika kiakili na sasa anatembea kama mwenye akili punguani. Hata hivyo, kupitia kwa ushauri alioupata kutoka kwa mamake Trufena, anapata nafuu na anakubali kurudi shuleni. Chifu Moegi naye akafungwa jela ambako alihukumiwa kifungo cha maisha. Mwandishi anasema;

> Mliwa alirudi shuleni. Hii ilikuwa miezi sita tangu kutoweka kwake. Shuleni, mlikuwa msisismko wa aina yake kutokana na kurudi kwake. Akiwa mwenye tabasamu, alikwenda darasani na kubisha. (Uk 226)

Aidha, baada ya Mliwa kubakwa, inakuwa changamoto kwake na anaapa kuwasaidia wasichana wengine katika hali hiyo. Kubakwa kwake kunakuwa

kichocheo kikubwa sana maishani mwake cha kupigania haki za wahasiriwa wa mambo kama hayo. Mliwa na mamake Bonuke wanaanzisha wakfu ambao jukumu lake kubwa ni kutoa ushauri nasaha kwa wahanga wa majanga kama lile lililompata Mliwa. Kama wanavyosema McNeely na Blanchard (2009), vijana wanapofahamu kuwa wana uwezo wa kuchagua njia mwafaka au jinsi ya kukabiliana na hali fulani inaweza kuwasaidia kujiendeleza.

Vilevile, mwandishi wa *Chozi Langu* (2014) ameonyesha juhudi ambazo wanafunzi walifanya kupinga dhuluma kama hizi kwa kutoa siri za Chifu Moegi kwa walimu wa Mliwa na pia kwa kuandamana ili haki itendeke. Aidha, Maria naye hali yake ilibadilika baada ya kubakwa na jirani. Tofauti na Mliwa wazazi wa Maria walikubaliana kusuluhisha tatizo hilo kinyumbani. Mtafiti amebaini kuwa, hili si sawa hata kidogo kwani haki lazima itendeke kwa visa kama hivi ili watu wasiendelee kuwabaka mabinti za watu.

Imebainika kuwa, vijana wanapodhulumiwa kimapenzi huweza kukosa matumaini ya kuendelea kuishi na hivyo huona suluhu ni kujitia kitanzi. Unyama huu unapotendeka, ni vyema hatua ya kisheria ichukuliwe kwa wale waliotekeleza mambo hayo na wahasiriwa nao wapewe ushauri na nasaha ili wawe na matumaini. Mliwa anapodhulumiwa na Bi. Rai halati wake kwa kufanyishwa kazi ngumu na kunyimwa nafasi ya kudurusu masomo yake anaona heri arudi kwao kama njia ya kusuluhisha changamoto hiyo. Mwandishi anasema;

> Siku zilizofuata ziligeuka kizungumkuti kwa Mliwa pale kwa halati wake Ilimbainikia kuwa ingawa amekaribishwa na halatiye pale, hakutakikana kamwe. Tuhuma, matusi na masimango zikageuka kuwa mafuta aliyopakwa moyoni kila kukicha na wakoize. Akaanza kunuka na kujihisi asiyetakikana pale. Alipozidiwa na hali,aliona kuwa afadhali abwage zani. (Uk 99)

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Dunia anadhulumiwa na babake kwa kukataa kumlipia karo ya shule**.** Babake alipogundua kuwa Dunia amekuwa mtoro wa shule, alimdadisi na hatimaye kukataa kumlipia karo. Dunia alitafuta suluhu kwa kumwomba babake msamaha kuwa hangerudia tabia hiyo tena. Mwandishi anasema;

> Maneno ya babake yalimzindua akili. Aliyazingatia. Hakumshiriki tena Pazia. Alikwenda kwa mwalimu mkuu kumwomba msamaha na akamwelezea dhamira yake ya kuendelea na masomo. Mwalimu Mkuu akamweleza babake amlipie Dunia karo ya shule lakini akakataa. (Uk 34)

Licha ya kubadilika, babake alikataa kabisa kumlipia karo ya shule. Hata hivyo, mwalimu mkuu akaona jinsi Dunia alivyobadilika kitabia na hapo akaamua kulipa karo ya shule. Dunia akatia bidii masomoni hadi akapita mtihani wa darasa la nane.

### 3.2.10 Matumizi ya Mihadarati

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) imebainika kuwa Dunia anaamua kuacha kabisa kutumia dawa za kulevya. Anapofika mjini Mwambao, maisha yanakuwa magumu sana kinyume na alivyotarajia. Dunia anagundua baadaye kuwa Pazia alimhadaa kwa kumfunza matumizi ya dawa za kulevya akiwa na lengo la kuharibu maisha yake. Tunaambiwa kuwa anapooenda kilabuni na rafikiye Mpoto anaomba

kunywa soda tu. Mpoto anashangaa sana na tabia ya Dunia ya kunywa soda kila wakati wanapokuja kilabuni badala ya pombe. Anamwuliza;

> "Ah! Dunia utakunywa soda hadi lini?" (Uk 179)

Hii ni dhihirisho kuwa, Dunia ameacha tabia yake ya kunywa pombe baada ya kugundua madhara yake. Kulingana na Cosby na wengine (2000) vijana wanafaa kuelimishwa kuhusu madhara ya dawa za kulevya wakiwa katika umri wa kubaleghe ili wasije wakawa na uraibu wa matumizi ya dawa hizo. Vijana hawafai kulaumiwa kwa kila tendo mbaya bali wazazi waongee na vijana kwa upole kuhusu changamoto inayowakumba. Wanapoanza kutumia dawa hizo huwa wanaathirika sana na maisha yao huharibika.

### 3.2.11 Vifungo vya Jela na Vizuizi

Imebainika kwamba Dunia anahukumiwa bila hatia au ithibati kuwa yeye ni mkora. Kwa mujibu wa Stringer (2017), vijana baleghe wanafaa kutengwa na watu wazima wakiwa gerezani kwani wengi wao hufanya makosa kwa kushinikizwa na hali ya umaskini au wenzao. Hivyo basi, lengo la kuwafunga ni kuwafunza adabu ili waendelee kukua ila si kuwapa adhabu kali mno. Hivyo basi, ni vizuri wawasikize vijana hawa kwa makini wafahamu sababu zilizowapelekea kutenda uovu kabla ya kuwachukulia hatua kisheria. Stringer (2017) anasema kuwa, vijana wengine wanahitaji msaada na ushauri tu.

Kwa mujibu wa mwandishi wa Dunia Mashaka Makuu (2015), baada ya kifungo, Dunia anaapa kuwa hangerudi tena gerezani. Kwa hivyo, akaazimia kutojiingiza

kwa mambo yaliyo kinyume na sheria. Hata Mpoto anapomhimiza waibe kwa sababu ya hali ngumu ya maisha, Dunia anakataa. Anasema;

> "Aaa sahibu yangu, wanuia tuibe! Kutenda hivyo si ungwana hata kidogo. Magereza yamewekwa kutubadili tabia punde tutakapo vifungoni. Hapana bwana turejee nyumbani." (Uk 177)

Baada ya haya yote, Dunia anaamua kurudi kwao Kibaoni ili awaombe msamaha wazazi wake kwa kuwa mkaidi.

### 3.4 Hitimisho

Sura hii imeshughulikia kwa kina changamoto wanazopitia vijana baleghe katika jamii na suluhu kwa changamoto hizo kwa kutumia riwaya ya *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Waandishi wa riwaya teule wameonyesha changamoto halisi zinazowakumba vijana baleghe katika jamii ya kisasa. Visa halisi vinavyotendeka miongoni mwa vijana vimetajwa na waandishi. Mihimili ya nadharia ya Uhalisia imemsaidia mtafiti kutambua ya kwamba changamoto hizi zipo katika jamii na huwakumba vijana wa kawaida.

Wahusika kama Mliwa, Dunia, Pazia, Mpoto na Yasibu ni wahusika ambao wanaishi katika jamii. Aidha, vijana wa kike wanakumbwa na changamoto kama mimba za ujanani, kubaguliwa kiuana na kutawishwa ambazo wenzao wa kiume hawakumbani nazo. Vijana wa kike huathirika zaidi wanapopata ujauzito kwa mfano masomo yao hukatizwa ilhali wenzao huendelea na masomo. Utafiti huu umebaini kuwa, changamoto zinazowakumba vijana hutokana na jamii au vijana wenyewe. Aidha, jamii imechangia pakubwa katika changamoto hizo. Sura inayofuata inahusu mambo yanayochangia maendeleo ya vijana.

# SURA YA NNE

## MAMBO YANAYOCHANGIA MAENDELEO YA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA *CHOZI LANGU* (2014) NA *DUNIA MASHAKA MAKUU* (2015)

### 4.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, mtafiti amechunguza changamoto wanazopitia vijana katika jamii na suluhu kwa changamoto hizo. Sura hii imeangazia mambo mbalimbali yanayochangia maendeleo ya vijana katika jamii kwa kuzingatia *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Mambo haya ni pamoja na elimu, dini, sheria, ushauri nasaha, malezi, vyombo vya habari, jitihada, ufadhili kwa vijana na ukuzaji vipawa.

Kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii mtafiti amechunguza mambo ambayo huleta maendeleo miongoni mwa vijana. Kijana anapotangamana na jamii, huweza kujifunza mambo mengi ambayo humkuza. Maendeleo ni hali ya kufanikiwa aidha kiuchumi au kijamii. (TUKI, 2004). Maendeleo hutokana na juhudi afanyayo kijana maishani na huchangia mabadiliko miongoni mwa vijana. Ili kijana aendelee, ni muhimu kuzingatia mambo yafuatayo ambayo ni  msingi bora, msingi thabiti ambao hutatetereka.

### 4.1 Elimu

Elimu ni mafunzo yoyote yatolewayo na jamii kwa watu wake. ( TUKI, 2004). Inaweza kuwa elimu ya darasani au apatayo mwanajamii katika utangamano wake na jamii. Kijana anaweza kupata mafunzo kutoka kwa wazazi, wazee wa kijiji,

vijana wenzake au kutoka kwa walimu yaani shuleni. Mfumo wowote wa elimu ni muhimu sana katika kumpa kijana maarifa na maadili yafaayo katika jamii. Kwa mujibu wa Walibora (2012) elimu huwasaidia vijana kujielewa hao ni nani na hujenga utu miongoni mwao. Wahusika vijana ambao wameelimika katika *Chozi Langu (2015)* ni Mliwa, Chandeka na Chande. Mwandishi anasema kuwa, baada ya kuhitimu, Mliwa alipata kazi ya utangazaji katika kituo maarufu cha Redio Kisu. Licha ya hayo, Chanda dadake Mliwa, ni muuguzi katika hospitali kuu ya Nyikani, naye Chandeka dadake mdogo ni mwalimu katika shule ya upili huko Bondeni. Mwandishi anasema kuwa;

> Mliwa alikuwa keshafuta chozi lake na masaibu kayazika katika kaburi la sahau. Alikwishahitimu uanahabari katika chuo kikuu. Tangu kuhitimu kwake, ameshapata sifa kochokocho kwa utangazaji wake kwenye kituo maarufu cha Redio Kisu. (Uk 234)

Kupitia elimu, wahusika Mliwa, Chanda na Chandeka wameweza kujinyakulia nafasi za kazi. Mliwa ameweza kubadilisha hali ya mamake ambaye alikuwa akifanya biashara ndogondogo, sasa ana duka la jumla. Vilevile, mabadiliko yametokea kwa tabia ya Mliwa. Mliwa ambaye daima alikuwa amehuzunika kutokana na mateso aliyokuwa anayapitia sasa amefuta chozi lake.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), babake Dunia na Yasibu aliamini kuwa elimu ni nguzo ambayo kila mtu sharti azingatie. Anaona kuwa kupitia elimu watoto wanaweza kujiendeleza.

Anamwambia bintiye Yasibu kuwa;

> "Hebu yazingatie maendeleo yaliyoletwa na elimu. Huoni ajabu mwanangu namna runinga zinavyoyaonyesha matukio ya ulimwengu nzima kana kwamba ndiyo unayoshuhudia yakitendeka hapa." (Uk 30)

Kauli hii inaonyesha kwamba Bwana Mashaka ameona umuhimu wa elimu kuwa ni chanzo cha maendeleo hasa ya kiteknolojia. Hivyo basi, anajaribu kumfungua bintiye Yasibu macho ili asiyapuuze masomo. Hata hivyo, Dunia na dadake Yasibu wanakataa kuendelea na masomo. Dunia anatoroka kwao hata baada ya kupita mtihani wa darasa la nane, Yasibu naye anapata ujauzito, hivyo anaacha shule. Bwana Mashaka anahisi uchungu mwingi sana moyoni baada ya wanawe kukataa kuendelea na masomo. Anasema;

> "Huwezi mke wangu kukadiria hasara watakayoipata watoto hawa kwa kuikataa elimu? Ah! Ni hasara kubwa mno." (Uk 98)

Dunia anateseka sana baada ya kuacha masomo na kutorokea mjini. Anafungwa jela kwa kushukiwa kuwa mwizi. Baada ya kifungo anakosa makazi, chakula na mavazi. Anaamua kurudi kwao Kibaoni kumwomba babake msamaha. Mwandishi anasema;

> "Maisha yalikwisha kumhukumu Dunia, akateseka hadi ya kuteseka. Aliteleza akaanguka pindupindu. Malimwengu yalimng'ang'ania kumwadhibu kwa kila njia nafuu asiipate asilani." (Uk  212)

Vilevile, Yasibu alitorokea mjini baada ya kujifungua mwanawe Yadhuru. Alipata shida nyingi mno kama vile kukosa chakula na makazi. Akaamua kujiingiza kwa

mapenzi na Mzee Fadhili ambaye alimwambukiza ugonjwa wa Ukimwi na mwishowe akamwacha Yasibu. Imebainika kuwa elimu ndiyo nguzo kamili kwa maisha ya vijana kwani ndio suluhisho kwa baadhi ya matatizo yanayowakumba kama vile umaskini.

## 4.2 Jitihada

Mtafiti amebaini kwamba Mliwa, katika *Chozi Langu* (2014), amesawiriwa kama kijana ambaye anatia bidii sana masomoni ili aweze kujiendeleza kiuchumi. Ufanisi wa Mliwa katika masomo ulitokana na jitihada zake. Mliwa anasema;

> "Nitajitahidi zaidi. Falsafa yangu mpya sasa ni kufika kiwango cha juu zaidi cha ufanisi katika yote nitendayo." (Uk 193)

Mliwa alijua lengo lake la kuwa shuleni. Hii ndiyo sababu iliyomfanya kutia bidii masomoni. Akawa anasifika shuleni kutokana na ufanisi wake. Mwandishi anasema kuwa, ingawa Mliwa alikuwa na changamoto za kifamilia, hilo halikuwa pingamizi kwake. Alifanya kazi za ziada alizopewa na walimu wake shuleni. Anazifanya kazi hizo hata wikendi. Anamwambia Chifu kuwa:

> "Nimetoka shuleni kwa masomo ya ziada ingawa ni wikendi. Kuna kazi tuliopewa na mwalimu ambayo nilitaka kuimalizia kabla ya kwenda nyumbani. Tunajitayarisha kwa mtihani wa mwigo." (Uk 123)

Ni dhahiri kuwa kipawa chake Mliwa cha uandishi kiliendelea kunawiri. Mtafiti amebaini kuwa, kipawa hakiwezi kunawiri bila kupaliliwa. Mwandishi anasema kuwa Mliwa alifanya mazoezi kila wakati. Walimu wake walimpa motisha kila wakati. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii

unaoeleza kuwa, katika hatua ya kujitambulisha, kijana hutaka kujitambulisha na kukuza nafsi yake. Wale wanaopewa motisha huwa na ujasiri wa kujitegemea. Mliwa alipata ujasiri na kujiamini baada ya kupewa motisha kutoka kwa walimu na wenzake. Juhudi za Mliwa zilimsaidia kuwa mshindi katika shindano la utangazaji. Kutokana na hilo, Mliwa akajua fika kuwa ana kipawa cha utangazaji. Huo haukuwa mwisho kwani alitia bidii masomoni hadi alipohitimu Uanahabari katika chuo kikuu.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Dunia anajitahidi kufanya kazi ili abadilishe hali yake ya umaskini. Baada ya kifungo, Dunia pamoja na rafiki yake Mpoto wanafanikiwa kupata kazi za vibarua. Dunia aliendelea kujikaza kwa kazi hiyo hadi alipoweza kupata nyumba angaa ya maana na kupata chakula cha kutosha. Mwandishi anasema;

> Sasa walirauka kila siku wakaingia bandarini na madukani kufanya uhamali wa kila aina. Hawakulala njaa tena. Ugumu wa maisha ulianza kupungua polepole. Vijana waliokosa mustakabali mzuri wa maisha sasa walijaa fahari na matumaini. (Uk 178)

Taarifa hii inaonyesha matokeo ya juhudi miongoni mwa vijana. Vijana wana uwezo wa kuyabadilisha maisha yao iwapo watatia bidii kwa lolote wafanyalo.

### 4.3 Ushauri Nasaha

Mtafiti amebaini kuwa, ushauri nasaha ni jambo linaloweza kumjasirisha kijana. Walimu wanapowapa ushauri na motisha wanafunzi, wao hutilia mkazo zaidi katika kazi zao. Kwa mujibu wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii unaoeleza kuwa, vijana wanaopewa motisha kwa yale wanayofanya huwa na ujasiri

na kujitegemea. Zaidi ya masomo wanayowapa wanafunzi darasani, wanawahimiza wajitahidi zaidi iwapo wanataka kufaulu. Bi. Fasaha mwalimu wa Mliwa anamwambia kuwa;

> "Elimu ndiyo nuru ya maisha. Ukiongeza vipawa ulivyonavyo, utakuwa mtu wa kutajika katika jamii." (Uk 104)

Licha ya kumfunza Kiswahili, alikuwa anampa ushauri na kumtia motisha wakati Mliwa alipokuwa na wasiwasi. Kutokana na ushauri nasaha, Mliwa anaendelea kujiamini kila uchao. Imebainika kuwa, ushauri nasaha humpa kijana matumaini. Mliwa anapewa matumaini na Bi. Fasaha wakati anahisi kuwa hakufanya vyema katika mashindano ya utangazaji na kuwa hakuwa na matumaini kuwa angeshinda. Bi. Fasaha anasema;

> "Pole. Maji yakishamwagika hayazoleki. Huenda hii haikuwa nafasi yako. Utajaribu tena kwani bado u kijana na vipawa unavyo." (Uk 82)

Kulingana na kauli hii, Mliwa anapata matumaini kuwa bado anayo nafasi nyingine kwa hivyo wasiwasi wake unamwondokea.

Mamake Trufena anampa Mliwa ushauri nasaha wakati alipobakwa na Chifu Moegi. Unyama huu aliotendewa Mliwa ulimwathiri sana kiakili, kiafya na hata kimasomo. Aliacha kwenda shuleni na kuanza kuzurura mitaani huku akijiongelesha pekee yake. Kulingana na mamake Trufena, Mliwa alikuwa katika hali ya msongo wa mawazo. Hii hali ni hatari sana miongoni mwa vijana baleghe na wasiposhughulikiwa huenda wakajitia kitanzi au kurukwa na akili.

Anasema kuwa:

> "Huzuni, majonzi na mfadhaiko huwa ni ishara muhimi ya kuzingatia katika hali kama hii. Tena, waathiriwa wengi huwa hawana hamu ya chakula kando na kukosa usingizi na kuwa na majinamizi. Mliwa alikuwa na ishara kama hizo hapo mwanzoni kabla ya kumshughulikia." ( Uk 220)

Taarifa hii imetuonyesha ya kwamba hali ya afya ya Mliwa ilikuwa imebadilika baada ya kubakwa. Lakini baada ya ushauri nasaha aliopewa na Mamake Trufena, akawa mzima kiafya na akaendelea na masomo yake.

Mtafiti amebaini kuwa, vijana wenyewe kwa wenyewe wanaweza kuwabadilisha wenzao na kuwaendeleza kupitia kwa ushauri nasaha. Kupitia kwa barua, Trufena anamshauri Mliwa asipoteze matumaini maishani kutokana na unyama aliofanyiwa. Anamshauri aendelee kujikaza kimasomo na asikubali kandili yake ya maisha kuzimwa. Ushauri huu ulimpa ari tena Mliwa na akaanza kujizatiti masomoni kama ilivyokuwa awali.

Walimu, wazazi na wenzake wanapotambua kuwa Mliwa ana kipawa cha uandishi wa mashairi wanaendelea kumhamasisha aendelee na kipawa kile. Mwandishi anasema kuwa;

> Walimu walimshauri kuendelea na kukuza kipawa chake cha uandishi. Kila ijumaa alipenda kuandika shairi na kulitundika kwenye ukuta wa darasa lao ili wanafunzi wake wasome. (Uk 65)

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Dunia abadilisha tabia yake ya uasi na kuamua kurudi nyumbani kuomba msamaha baada ya kupitia mateso. Ingawaje

mwanzoni alikataa kufuata mashauri ya wazee wake, aligundua baadaye kuwa mambo waliyomwelezea yalikuwa muhimu katika maendeleo yake.

Wazazi na walimu wa Dunia wanampa ushauri aendelee na masomo yake. Dunia alipoanza kushirikiana na Pazia, alianza kutumia vileo na pia kuanza kuwa mtoro. Babake alipogundua hili alimshauri Dunia aachane na Pazia ambaye anamhadaa tu. Dunia anarudi shuleni na kuacha kushirikiana na Pazia. Mwalimu mkuu anampa ushauri unaomfaa sana Dunia ambaye anabadilika sana kitabia na anafaulu katika mtihani wake. Mwandishi anasema;

> Mja ni mwepesi wa kubadilika tabia, na ndivyo ilivyotokea kwa Dunia. Ghafla alibadilisha tabia yake ya awali ya utundu na kiburi, akawa mpole, mnyenyekevu na mwenye haya. Alijawa na roho ya imani. Chochote alichopata, si tunda, si chakula alikuwa na mwenziwe.(Uk 48)

Kauli hii inadhihirisha kuwa, Dunia alikuwa amebadilika tabia kutokana na ushauri aliopewa na walimu na wazazi wake.

Wazee katika jamii walimpa mawaidha ya kumwendeleza na kumbadilisha Dunia tabia ya ukaidi wake. Hata kama alikataa kabisa lakini walifanya jukumu lao la kumwelekeza Dunia. Bwana Mafusho anamwambia kuwa;

> "Chijana Dunia, akuambiaye, akutaka. Angalia namna tunavyokupenda. Sote tumeng'ang'na kukonya ndia, hata kutishwa upijwe ili angalau usihi rohoyo ukuishie ukaidi. Aa! Kweli sikio la kufa halina dawa." (Uk 139)

Ni dhihirisho kuwa jamii nzima ilitaka Dunia abadilishe msimamo wake. Aache ukaidi wake ili aendelee na masomo yake. Licha ya mawaidha yote Dunia alikataa kubadilisha msimamo wake.

Alipokuwa anasafiri kwenda Mwambao baada ya kutoroka nyumbani kwao, Mzee Mjumbe anamshauri Dunia kuwa elimu ni muhimu sana kwa maisha ya kijana na alifanya vibaya sana kukataa kusoma. Anamwambia;

> "N'hawafu chijana wee. Ulipewa elimu ukaikataa. Ulimwengu humuno, n'tu asiye na elimu ni kama n'tu bila mato- chipofu. Uliyasusia masomo hawafu nkubwa!" (Uk 148)

Dunia anabadilisha tabia yake na kuacha uasi baada ya kupitia mateso mengi jijini mwambao. Anagundua kuwa ushauri nasaha aliyopewa na wazazi na walimu wake ulikuwa muhimu sana maishani mwake. Kwa hivyo, anajuta na kuamua kurudi nyumbani kuomba msamaha.

Yasibu anajuta kwa kupuuza ushauri wa mamake kuhusu utu. Hii ni baada ya kutambua kuwa Bwana Fadhili aliyekuwa mumewe alikufa kutokana na ugonjwa wa Ukimwi. Yasibu anajuta kwa sababu alimtoroka Fakiri kijana aliyemsaidia wakati alikuwa na shida na kumkimbilia tajiri Fadhili ambaye baadaye alimfukuza. Anakumbuka ushauri wa mamake na hapo ndipo alipobadilisha mtazamo wake kwa Fakiri. Aliamua kurudi kwa Fakiri kumwomba msamaha. Anasema;

> "Kwa nini sikuzingatia wasia wa mama pale nilipoamua kumtoroka Fakiri? Kwa hakika nilifanya kosa kwa kutotathimini utu!" (Uk 186)

Mapenzi miongoni mwa vijana ni suala ambalo linafaa kushugulikiwa mno. Kulingana na Cherry (2017) ni wakati ambapo vijana hujaribisha kila kitu. Hivyo basi wanafaa kupewa ushauri mwafaka. Kwa mujibu wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii, kijana hutaka kujitambulisha na kukuza nafsi yake, wale

wanaopewa motisha huwa na ujasiri na hujitegemea na wale ambao hawapewi mwongozo unaofaa huchanganyikiwa na hukosa mwelekeo maishani. Yasibu anakosa ushauri nasaha kutoka kwa wazazi wake. Anakosa ushauri wa wazazi wake na mwishowe anapata mimba na kuacha masomo.

### 4.4 Ufadhili kwa Vijana

Ingawa vijana wengi hasa wanaotoka katika familia maskini hutaka kubadilisha hali yao kupitia elimu, ukosefu wa fedha huzima ndoto yao. Mtafiti amebaini kuwa ndoto yao inaweza kutimia iwapo katika jamii kutakuwa na watu watakaowasadia katika utekelezaji wa malengo yao ya maisha. Kupitia kwa Mliwa, mwandishi wa *Chozi Langu* (2014) ameonyesha umuhimu wa wahisani hawa katika jamii. Mwandishi anasema;

> St. Stephen's ilikuwa shule iliyowasaidia wanafunzi wengi kutoka mitaa duni ukiwemo mtaa wa Mwembe kupata angaa kisomo siku hizo na kujidai kuwa waliwahi kuziona kuta za shule ya upili. Ikawa shule iliyomvaa na kumfaa Mliwa pia. (Uk 144)

Taarifa hii inadhihirisha umuhimu wa msaada kwa wanafunzi wasio na karo. Mliwa anafadhiliwa katika masomo na shule ambako alisoma kwa bidii hadi chuo kikuu. Mwandishi anasema;

> Babake Trufena alikuwa tajiri mtajika. Pamoja na utajiri wake alikuwa na utu busara na hekima (Uk 119)

Baba Trufena aliwafadhili vijana wengi kutoka jamaa maskini. Licha ya hayo, aliwavisha na kuwalisha.

Mliwa vilevile anapata ufadhili kutoka kwa shirika la utangazaji. Baada ya Mliwa kuibuka mshindi katika shindano la utangazaji anaahaidiwa kwamba atalipiwa karo ya shule ya upili na pia apelekwe kwenye mafunzo ya uanahabari. Mkurugenzi anasema;

> Kwa kuwa Mliwa ndiye mwanafunzi pekee kati ya wale waliofuzu, tumeamua kumlipia karo. Pia tutampeleka kwenye mafunzo ya Uanahabari ili ajiunge mara moja na kampuni yetu baada ya mafunzo. (Uk 103)

Imebainika kwamba, kanisa alilohudhuria Mliwa na Mamake Bonuke, lilimfadhili Mliwa kwa masomo yake ya shule ya upili. Kutokana na juhudi alizokuwa nazo Mliwa, aliweza kuendelea na masomo yake na kufaulu mtihani. Mwandishi anasema;

> Kundi la wazungu kutoka Marekani lilitembelea kanisa alilohudhuria Bonuke na wanawe. Bonuke alielezwa kuwa ujumbe kama huo ulitembelea kanisani ili kila mwaka kutathimini njia za kuwasaidia waumini wahitaji. (Uk 63)

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), mwalimu mkuu anajitolea kumlipia Dunia karo ya shule baada ya babake Dunia kukataa kuchukua jukumu hilo kama mzazi. Hii ni baada ya kugundua kuwa Dunia amekataa kwenda shule. Licha ya Dunia kumwomba babake msamaha na kurudi shule, babake anakataa kabisa kujihusisha naye. Mwalimu mkuu alipoona hivyo, akaamua kumlipia Dunia karo ya shule hadi alipohitimu darasa la nane na kufaulu katika mtihani. Mwandishi anasema;

> Dunia aliishi kwa rehema za Mwenyezi Mungu, akapata riziki kwa kudoea kwa marafiki na wafadhili. Huko kupata elimu kulikuwa kwa bahati nasibu tu. Hangeendelea kusoma shule thama na imani ya Mwalimu Mkuu Bwana Busara. (Uk 102)

Taarifa hii inaonyesha kuwa katika jamii kuna watu wanaojitolea kuwafadhili vijana ili wawasaidie vijana kujiendeleza kimaisha.

**4. 5 Dini**

Dini ni imani inayohusiana na kuwepo kwa Mungu au miungu. Waumini huwa na imani inayodhibiti maisha yao. Waumini katika dini hizi wanatarajiwa kufuata kanuni za dini zao. Asasi ya dini ina jukumu la kuwaendeleza vijana kwa njia mbalimbali na pia kuwabadilisha kitabia kulingana na mafunzo yao kwa jamii. Kama anavyosema Kiprugut (2011), dini ni asasi muhimu sana katika kufunza maadili kwa wanajamii kwani vipengele vyote vya maisha vimeingiliana na dini.

Mtafiti amebaini kwamba, mwandishi wa *Chozi Langu* (2014) anatuangazia nafasi ya dini kama mojawapo ya mambo yanayowaendeleza vijana. Kwa kutumia wahusika kama vile Mliwa, Trufena na vijana wa shule ameonyesha jinsi imani yao kwa Mungu iliwapa matumaini. Mtafiti amebaini kuwa, dini huathiri familia na pia kuleta mabadiliko katika jamii. Kila wakati Mliwa alipokumbana na tatizo, alimlilia Mungu amsaidie.

Anasema kuwa;

> "Makosa haya yameniharibia nafasi ya kushinda, Mungu wangu nipe ushindi nikutumikie katika utangazaji." ( Uk 79)

Kutokana na kauli hii, ni dhahiri kuwa Mliwa aliamini Mungu kuwa ni yeye pekee atakayempa ushindi katika utangazaji. Mliwa anapopata ushindi, anaona si bidii yake tu bali ni mkono wa Mungu. Anamshukuru Mungu kwa kuweza kuibuka mshindi.

Imebainika kuwa Mliwa alikuwa na subira na uvumilivu kwa sababu alimwamini Mungu kuwa ataibadilisha hali yake. Alichukiwa na wakoi wake wakati alikuwa akiishi na hale wake. Licha ya matatizo aliyoyapitia, Mliwa hakufa moyo ila aliendelea kuomba Mungu ampe subira ili avumilie hayo yote. Anasema ya kuwa;

> "Ewe Mola nipe subira ya kuyavumilia haya yote mazito na mepesi, meupe na meusi. Mwenye kunitakia shari iwe shari kwake, mahasidi waguse nyoyo zao…" (Uk 95)

Trufena rafikiye Mliwa anaamini pia Mungu ni mlinzi wao. Mliwa anapobakwa na kuacha kwenda shule, wanafunzi wanajawa na wasiwasi nyingi mno. Trufena anawaongoza katika maombi. Maombi haya yanawapa tumaini kuwa Mliwa atarudi.

Aidha, kwa sababu ya dini Mliwa anaweza kuendelea na masomo yake. Mliwa anafadhiliwa na Wazungu kutoka Marekani ambao huja katika kanisa lao kila mwaka. Wafadhili hawa walipoona kipawa cha Mliwa katika utunzi na uimbaji wa

mashairi, walimfadhili katika masomo yake ya shule ya upili. Mliwa anapata nafasi nzuri ya kujiendeleza na kubadilisha hali yake. Mwandishi anasema;

> Kundi la Wazungu kutoka Marekani lilitembelea kanisa alilohudhuria Bonuke na wanawe. Bonuke alielezwa kuwa ujumbe kama huo ulitembelea kanisani ili kila mwaka kutathimini njia za kuwasaidia waumini wahitaji. (Uk 63)

Utafiti huu unabaini kuwa, mamake Trufena aliyemsaidia Mliwa baada ya kubakwa anamwamini Mungu. Baada ya kubakwa, Mliwa alikosa tena matumaini ya kuendelea na shule. Akawa na msongo wa mawazo hadi kiwango cha kurukwa na akili. Mama Trufena alimchukua Mliwa na kumpeleka hospitalini atibiwe. Anaamini kuwa Mungu hukubali matukio haya yatendeke ili aadilishe binadamu. Baada ya kumpa ushauri, Mliwa alirudi kuwa katika hali yake ya kawaida na kurudi shuleni ambako alifaulu mtihani.  Hivyo basi, Mliwa anabadilika tabia na kujiendeleza kimasomo kwa sababu amempata muumini aliyejitwika jukumu hilo.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), walimu na wanafunzi wanamwamini Mungu kuwa yeye ni mweza yote. Mwalimu mkuu anasema;

> "Hizi ni Baraka zake Mwenyezi Mungu, tuwa tumeweza kusoma kwa salama salmini siku ya leo. Tumshukuruni Mwenyezi Mungu." (Uk 83)

Ni wazi kuwa, maisha ya wanafunzi na walimu hawa yako mikononi mwa Mungu, kwani yeye ndiye huwawezesha kuendelea kimasomo. Aidha, Dunia anaamini kuwa ni Mungu tu anayeweza kubadilisha hali yake. Imani na matumaini kuwa kesho itakuwa sawa katika maisha ya vijana, ni mambo muhimu sana. Dunia

aliendelea kujikaza tu katika kazi alizofanya hadi alipoweza kupata nyumba angaa ya maana. Anamwambia rafikiye Mpoto kuwa;

> "Siku yatakapokuja mabadiliko, tutapata vitanda. Mabadiliko yatakuja kwa kudura za Mwenyezi Mungu, machungu yatuhame, tuishi kwa wema."(Uk 175)

Matatizo mengi nchini Kenya yameikumba jamii ya vijana, hivyo basi, dini ina jukumu kubwa sana la kuwapa vijana mafunzo yanayofaa ili wawe waadilifu. Makanisa kwa mfano yana nafasi kubwa sana katika uelimishaji wa vijana katika jamii. Vijana wanapopotoka kimaadili, huwa tunaitazamia kanisa kutoa mwelekeo unaofaa.

### 4.6 Malezi

Kwa mujibu wa Naliaka (2012) malezi huhusisha makuzi, mafundisho na uangalizi anaopewa mtoto. Malezi bora huchangia katika tabia nzuri kwa kijana. Wazazi waliowajibika huona umuhimu wa elimu. Huwapa motisha watoto wao wasome kwa kuwalipia karo na kuhakikisha wamepata mahitaji ya kuboresha masomo. Mtafiti amegundua kuwa malezi huhusisha wazazi wote wawili ambao wanafaa kuwajibika. Mzazi mmoja asipowajibika basi watoto huathirika. Katika *Chozi Langu* (2014), Mliwa analelewa na baba asiyewajibika. Kajogoo anakosa kumlipia Mliwa karo ya shule. Aidha, anamtesa mamake kila wakati anapotoka ulevini. Mliwa anakosa matumaini mpaka anatamani kifo kimchukue.

Mtafiti amebaini kuwa ingawa mamake Mliwa aliachana na Kajogoo, hiyo haikuwa suluhu kwake Mliwa kwani matatizo yalizidi. Hii ni kwa sababu wenzake shuleni

walikuwa wakimtusi kuwa yeye hana asili wala fasili. Walimtusi kuwa yeye ni 'mathee' kutokana na umri wake mkubwa. Mliwa alijawa na huzuni. Mwandishi anasema;

> Suala la kufukuzwa na babake ni jambo lililomsumbua moyoni Mliwa na kumkosesha amani na usingizi. Alikumbuka jinsi mamake alivyoteseka wakiishi na babake mjini bapa. Alikumbuka wakati mmoja wakilala matumbo yakiwanguruma. (Uk 111)

Kauli hii inaonyesha ya kwamba Mliwa aliathiriwa kiakili kwa sababu ya hali hiyo. Hata hivyo mwandishi anasema kuwa, mawazo haya yalimjenga upya na kumpa mwelekeo na mwamko mpya. Hivyo, akabadilisha hii tabia ya kuhuzunika kila wakati. Akawa na falsafa mpya ya kujiunga na chuo kikuu.

Mliwa anatia bidii masomoni ili abadilishe hali yake. Mtafiti amebaini kuwa mamake Mliwa anamlea kwa mapenzi na busara. Anampa ushauri unaomwongoza maishani. Anahakikisha kuwa Mliwa amepata elimu nzuri. Anasema kuwa;

> "Mimi ni mzazi na haja yangu ni kumsaidia binti yangu Mliwa. Ningependa arudi shuleni na aendelee na masomo. Elimu ndio urithi mkubwa mzazi anaweza kuwapa wanawe bila kubagua jinsia." ( Uk 175)

Utafiti huu umetuonyesha ya kwamba, Bonuke alimlea Mliwa bila usaidizi wa mumewe. Hata hivyo, Mliwa anafaulu maishani kutokana na bidii na mashauri aliyopewa na mamake. Kama wanavyosema Dacey na John (2009), si kila kijana anayelelewa na wazazi waliotalikiana huwa na athari mbaya kwao, baadhi yao hufanya vyema.

Hata hivyo, mtafiti aling'amua kuwa, Yasibu katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) anadekezwa sana mwanzoni na babake. Babake hataki mwanawe hata atumwe maji ya kunywa. Yasibu hafurahishwi na jinsi anavyodekezwa na wazazi wake katika umri wake wa miaka 12. Anaona anafaa ajitegemee kufanya mambo, sio kufanyiwa kila kitu. Anataka pia apate uhuru wa kutembea kama wenzake. Maelezo haya ya mwandishi yanaingiliana sana ya mawazo ya Kroger (2004) ambaye anasema kuwa katika umri huu wa kubaleghe vijana hutaka kujitambulisha kwa kutangamana na jamii. Yasibu anamwomba babake ruhusa ya kutoka ili atangamane na wenzake. Anasema;

> "Ba! Nataka n'cheze kama wenzangu. Nataka nende kuni na maji. Nataka nijifulie nguo. Nataka baba nitoke nyumbani na kurudi pasi na kuulizwa."  (Uk 23)

Baada ya kupewa uhuru wa kutembea, Yasibu akaanza kuonyesha ukaidi kwa wazazi wake akakosa tena kuwaheshimu. Ni bayana kuwa, Bwana Mashaka alishindwa kumwelekeza bintiye kwa njia inayofaa. Ule utundu wake unatokana na uhuru alioupata na kuanza kutangamana marafiki ambao walimpotosha. Bwana Mashaka alimpa Yasibu uhuru bila hata kushughulika kujua uhuru huo unatumiwa vipi. Matokeo yakawa kupata ujauzito.

Mtafiti alibaini kuwa, uhuru kupita kiasi kwa vijana baleghe ni mojawapo ya mambo yanayowapotosha vijana. Wazazi wanapowapa vijana uhuru wawape pia na masharti na wafaa wajue wanao wanahusiana na nani. Na pia wazazi hawafai kulegeza kamba kwa masharti yanayowapa vijana. Yasibu alipewa uhuru kupita kiasi ikawa ni chanzo cha ukaidi wake. Vilevile imebainishwa kuwa si vyema

kuwadekeza sana vijana. Wanafaa kupewa majukumu na kupitia kwayo watapata changamoto. Hizi changamoto zikikabiliwa kwa njia inayofaa wataweza kukua ipasavyo. Jeffrey na Brown ( 2003) wanasema kuwa kazi ya wazazi ni kuangalia mambo ya nje yanayohusiana na kijana kwa mfano, sehemu za burudani, shule na marafiki wanaotembea nao. Bwana Mafusho anamuuliza Bwana Mashaka chanzo cha ukaidi wa Yasibu. Anasema;

> "Tulimlea kama desturi ya malezi. Tulimzuia asitoke nje ya nyumba alipotoka shuleni ili apate kudurusu masomo yake. Tuliamuru watumishi wamkimu kwa kila jambo, mradi apate wasaa wa kudurusu." (Uk 43)

Bwana Mafusho anasema kuwa chanzo cha ukaidi wa Yasibu ni kutopewa nafasi ya kutangamana na wenzake. Anasema kuwa mtoto anafaa kupewa nafasi ya kucheza baada ya kusoma na pia kusaidia watumishi katika baadhi ya kazi. Kulingana na Bwana Mafusho, wazazi wengi huteleza katika kulea wanapozuia watoto kutangamana na wenzao. Yasibu alipata mimba kwa sababu ya malezi mabaya. Hakupewa maelekezo yanayofaa katika umri wake wa kubaleghe na kutoka na udhaifu wa nafsi yake akashindwa kuhimili mihemko ya hisia.

Mtafiti amegundua kuwa Dunia anashindwa kuendelea na masomo yake kwa sababu ya malezi mabaya. Baada ya babake kukataa kuhusiana na Dunia kwa lolote, Dunia alikimbilia rafikiye Pazia ambaye anamshauri kuanza kutumia vileo. Licha ya Dunia kufaulu vizuri katika mtihani wa darasa la nane, anaamua kutoendelea na masomo na kutoroka nyumbani. Huu ni ushauri kutoka kwa Pazia rafikiye. Pazia anamshauri Dunia aache kusoma kwa sababu hapo awali babake hakumthamini. Anamwambia;

> "Dunia, usiyaridhi maneno ya Bwana Mashaka. Noma sana mzee yule. Amekupuuza wakati huo wote leo tu ndio ati ajifanya mwema. Leo ndio anatambua kuwa wewe ndio mtoto wake hata anaandaa karamu ya kufaulu kwako?" ( Uk 129)

Maneno haya yanadhihirisha wazi kuwa, Dunia alikosa mapenzi ya babake. Hivyo, basi malezi mazuri yanapokosa nyumbani vijana huweza kuyatafuta kwingineko na huko wanaweza kuhadaiwa. Malezi si ya mzazi tu, hiyo ndio sababu mwalimu mkuu akajitwika jukumu la kulipia Dunia karo aendelee na masomo yake. Licha ya Dunia kumwomba msamaha, Bwana Mashaka hakulegeza kamba. Kwa mujibu wa Jeffrey na Brown (2003), wazazi wanafaa kuongea wazi na wanao, wawe na uhusiano mwema ili wasiwaone kama maadui bali marafiki.

Kulingana na Dacey na John (2009), ukosefu wa mzazi mmoja hasa baba hufanya watoto wakose mahitaji muhimu. Wanasema kuwa, kuadhibu vijana kunaweza kubadilisha tabia ya vijana, yaani hukomaa haraka na kutoka katika ulinzi wa familia. Hata hivyo, adhabu haifai kuvuka mpaka. Ukaidi wa Dunia unatokana na babake kumnyima nafasi nyingine ya kuwa karibu naye. Kulingana na Jeffrey na Brown (2003), baba ni kielelezo kwa kijana wa kiume. Mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameonyesha bayana malezi kama chanzo cha mabadiliko hasi ya tabia ya Dunia. Hasa babake Dunia ambaye alikosa kumpenda na kumwelekeza Dunia kwa njia inayofaa. Chuki kwake Dunia ikawa chanzo cha kujiingiza katika matumizi ya mihadarati. Malezi ni mojawapo ya masuala muhimu yanayoathiri maendeleo ya vijana. Vijana hudhihirisha mabadiliko chanya au hasi kutokana na malezi wanayopewa. Dunia na Yasibu ni vijana waliokosa malezi na

maelekezo mazuri wakiwa katika umri wa kujitambulisha. Kwa mujibu wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na kijamii, katika hatua hii ya kujitambulisha kijana hutaka kujitegemea na kukuza nafsi yake. Erickson na Erickson (1998) wanasema kuwa, wale wanaopewa motisha huwa na ujasiri na kujitegemea ilhali wale ambao hawapewi mwongozo unaofaa huchanganyikiwa. Kutokana na maelezo haya, ni wazi kuwa Dunia na Yasibu walikosa mwelekeo maishani kwa sababu wazazi hawakuwapa mwongozo unaofaa.

## 4.7 Vyombo vya Habari

Mwandishi wa *Chozi Langu* (2014) amesawiri vyombo vya habari kama taasisi inayowaendeleza na kuwabadilisha vijana tabia kwa njia ya elimu. Aidha, vyombo vya habari husaidia jamii katika kupambana na uovu dhidi ya wanajamii. Pia huweza kuwahamasisha wanajamii kupigana dhidi ya unyama ambao hutendewa vijana kwa kuchapisha kwa magazeti masuala hayo au kupitia redioni.

Shirika la Utangazaji, linajitolea kumlipia Mliwa karo ya shule. Baada ya kushinda shindano la utangazaji anahaidiwa kulipiwa karo ya shule ya upili. Licha ya hayo, Mkurugenzi wa Shirika hilo anampa ahadi Mliwa kuwa atapelekwa katika chuo kwa mafunzo ya uanahabari. Mkurugenzi anasema;

> "Kwa kuwa Mliwa ndiye mwanafunzi pekee kati ya wale waliofuzu, tumeamua kumlipia karo. Pia, tutampeleka kwenye mafunzo ya uanahabari ili ajiunge mara moja na kampuni yetu baada ya mafunzo." (Uk 103)

Taarifa hii inatuonyesha kuwa, Mliwa alisaidiwa kimasomo na shirika la utangazaji. Isitoshe, alihaidiwa kazi baada ya kusoma. Mliwa naye baada ya

kuhitimu uanahabari katika chuo kikuu, anapata kazi ya utangazi kwenye kituo maarufu cha Redio Kisu. Moriki anasema;

> "Kazi ya Uanahabari ni muhimu sana katika jamii zinazoinuka kama yetu. Lazima tuchape kazi kwa jino na ukucha kumulika changamoto zinazoikumba jamii ili tuweze kubaini jinsi ya kuboresha jamii yetu." (Uk 234)

Mtafiti ameng'amua ya kwamba, licha ya kuajiri vijana, vyombo vya habari huwafunza maadili katika jamii. Pia huwapa ujuzi vijana kukumbana na matatizo yanayoikumba jamii. Moriki anakataa kuhongwa na Chifu Moegi ili afiche unyama alioutenda. Anadai kuwa hiyo itakuwa kinyume cha maadili ya kazi waliofunzwa shuleni. Anasema kuwa;

"Sisi wanahabari kazi yetu ni kuwatetea wanyonge" (Uk 160)

Anayapuuza maneno ya Mbunge na kuchapisha ripoti hiyo kwa gazeti la Jicho la Leo. Taarifa hiyo inawazindua wanajamii na serikali. Kutokana na taarifa hii, viongozi wa elimu na wa kiserikali wanaanza kuchunguza kisa hicho na walipopata ukweli Chifu Moegi akafungwa kifungo cha maisha. Mliwa naye akarudi shuleni kuendeleza masomo yake na hali yake pia kubadilika.

Mwandishi amesawiri vyombo vya habari kama asasi inayowasaidia vijana kujiendeleza kwa kukuza vipawa vyao mbalimbali. Kipawa cha Mliwa cha utangazaji kinapaliliwa na shirika la utangazaji. Shirika hili liliwapa nafasi vijana chipukizi wenye vipawa vya utangazaji kwenye redio katika lugha ya Kiswahili. Mliwa alifahamu kuwa ana kipawa hicho kwa hivyo akaona ni nafasi nzuri ya kukuza kipawa chake. Mwandishi anasema;

> Tangazo hilo lilieleza kuwa walihitajika vijana chipukizi wenye kipawa cha utangazaji kwenye redio lugha ya Kiswahili. Mliwa alifahamu bayana kuwa alikuwa na uwezo wa kupata nafasi hiyo ili kukuza kipawa chake. Kwa kujiamini aliamua kushiriki kwa kutuma maombi. (Uk 72)

Hali ya Mliwa inabadilika baada ya kuibuka mshindi katika shindano la utangazaji. Akawa na matumaini makubwa zaidi ya kuwa mtangazaji. Akatia bidii masomoni mpaka akahitimu kuwa mtangazaji wa Redio kisu. Ni bayana kuwa, vyombo vya habari vimechangia sana katika maendeleo na mabadiliko ya vijana katika jamii.

### 4.8 Ukuzaji Vipawa

Imebainika kuwa ukuzaji vipawa kwa vijana ni moja kati ya mambo yanayochangia maendeleo ya vijana. Kila kijana katika jamii ana kipawa ambacho anapokitumia vizuri kinaweza kumwendeleza. Katika *Chozi Langu* (2014), Mliwa anatambua kuwa ana kipawa cha utunzi wa mashairi, utangazaji na uandishi. Mara ya kwanza kufahamu hili ilikuwa wakati wageni walikuja kwa kanisa lao. Mliwa aliwaburudisha wageni kwa kukariri shairi kwa ustadi mukubwa. Mwandishi anasema;

> Shairi hili liligusa nafsi za wengi. Wageni walilifurahia kwa mdundo wake ingawa hawakuelewa ujumbe. Mdundo wa kimuziki na madoido aliyoyaongeaz Mliwa kwenye shairi yalichangia mvuto wa aina yake. ( Uk 64)

Kwa mujibu wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii, katika hatua ya kujitambulisha kijana hutaka kuijtegemea na kukuza nafsi yake. Wale wanaopewa motisha huwa na ujasiri na kujitegemea ilhali wale vijana ambao hawapewi mwongozo unaofaa huchanganyikiwa. Mtafiti amebaini kuwa hongera alizopewa

Mliwa baada ya kukariri shairi hili lilimpa motisha ya kusoma zaidi ili afaulu katika kila jambo afanyalo. Mliwa alipenda sana kuandika makala mengi kuhusu mambo tofauti katika lugha ya Kiswahili na kuandika shairi kila Ijumaa na kulitundika kwenye ukuta wa darasa lao. Walimu walimshauri Mliwa aendelee kukuza kipawa chake cha uandishi. Wanafunzi wenzake wakampa lakabu mbalimbali kwa mfano, 'Jicho la shule' na 'Mdadisi. Tangazo kuhusu mashindano ya watangazaji chipukizi yaliyotayarishwa na Redio Kisu yalipotangazwa mwalimu wa Chama cha Kiswahili alimhimiza Mliwa kujaribu.

Imebainika kuwa Mliwa alipata ujasiri kutokana na motisha aliyopewa na walimu. Pia alijiamini kuwa ataweza. Licha ya hayo, alifanya mazoezi kila siku. Tunambiwa kuwa;

> Trufena alimsikiza Mliwa akifanya mazoezi ya kujibu maswali na kutosheka. (Uk 71).

Mtafiti amebaini kuwa, Mliwa alitumia kipawa chake kujiendeleza kimaisha na kubadilisha hali yake ya maisha. Baada ya kuhitimu katika chuo kikuu, anapata kazi ya Utangazaji katika kituo maarufu cha Redio Kisu. Mliwa aliyemchukia babake sasa anataka kumtafuta ili kumsamehe.

### 4.9 Sheria

Katika riwaya ya *Chozi Langu* (2014) mwandishi anaisawiri sheria kama asasi ya kuwabadilisha na kuwaendeleza vijana. Sheria imetumika kuwalinda vijana dhidi ya dhuluma za kijamii. Mliwa ni kijana ambaye sheria inamsaidia kuendeleza

masomo yake. Kupitia sheria, Mliwa anapewa haki yake baada ya kubakwa na Chifu Moegi. Sheria ilimchukulia Chifu Moegi hatua. Alifungwa jela ambako alihukumiwa kifungo cha maisha kwa kumtendea Mliwa unyama. Hakimu anasema;

> "Ukosefu wa maadili wa aina hii unafaa kuadhibiwa kwa adhabu kali. Katiba yetu inatetea haki za kimsingi za kila mmoja wetu awe mtoto au mtu mzima, wa kike au wa kiume." (Uk 236)

Hii inaonyesha nafasi ya sheria katika kuwaendeleza vijana katika jamii. Naibu wa chifu Bi. Zawadi ambaye pia ana nasaba na Chifu Moegi, anajitolea kumsaidia Mliwa ili arudie hali yake ya awali.

Mashirika ya kupigania haki za kibinadamu walijitolea kupigania haki za vijana. Wanafunzi wa St. Stephen's pia wanaandamana ili hatua ichukuliwe dhidi ya Chifu Moegi. Aidha sheria iliwachukulia hatua vijana wawili waliomshambulia na kumjeruhi Moriki kijana ambaye alikuwa anampigania Mliwa. Vijana hao wanafungwa miaka saba. Hii ilikuwa ripoti kutoka kwa redio. Ilisema;

> "Nazo habari kutoka mahakamani zaeleza kuwa vijana wawili wamefungwa miaka saba kila mmoja kwa kumshambulia na kumjeruhi mwanahabari, Moriki Mwandiki. Korti iliwapata vijana hao na hatia ya kutekeleza kosa hilo katika mtaa wa Konambaya mjini Nyikani." (uk 215)

Aidha, katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha umuhimu wa sheria katika jamii. Mtafiti alinga'mua kuwa sheria ni mojawapo ya mambo yanaliyobadilisha tabia ya Dunia na hivyo kumwendeleza kimaisha. Kwa mujibu

wa Stringer (2017) lengo la vijana baleghe kuzuiliwa gerezani ni kuwabadilisha tabia ili wawe waadilifu baadaye. Dunia aliposhikwa na kuzuiliwa gerezani, aliweza kugundua kuwa alifanya makosa kuacha masomo na kutoroka kwao. Dunia anasema;

> "Sikiza Mpoto, sisi sote ni wahalifu. Tumo humu kwa sababu ya kuvunja sheria kwa njia moja au nyingine. Mimi nimepatikana nusu uchi na nimekuwa nikijuta tangu kuingia gerezani humu. Dhamira hasa ya vifungo hivi ni kutubadili tabia katika maisha". (Uk 173)

Hakimu anamhukumu Dunia na kumfunga kwa miezi sita. Baada ya hiyo anamshauri Dunia arudi Kibaoni ili aendelee na masomo yake. Dunia anabadilika na kuwa kijana mnyenyekevu, mwadilifu na mwenye bidii katika kazi zake baada ya kufungwa gerezani. Anafanya kazi kwa bidii ili abadilishe maisha yake ya kimaskini.

### 4.10 Hitimisho

Sura hii imetoa maelezo ya jumla kuhusu mambo yanayochangia maendeleo ya vijana baleghe katika riwaya za *Dunia Mashaka Makuu* (2015) na *Chozi Langu* (2014). Mtafiti amebaini kuwa malezi, dini, ukuzaji vipawa, ufadhili kwa vijana, sheria, vyombo vya habari, jitihada, elimu na ushauri nasaha ni baadhi ya mambo yanayochangia mabadiliko na maendeleo ya vijana. Aidha, elimu, malezi na ushauri nasaha yalichukua nafasi muhimu sana katika kuleta mabadiliko na maendeleo ya vijana. Mtafiti alibaini kuwa malezi huwa na athari kubwa sana katika kuwaendeleza vijana. Maswala haya yamejadiliwa kwa mujibu wa Nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ambayo mihimili yake imetumika. Kwa

mfano, kwa mujibu wa mihimili ya nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii mwandishi amesawiri vijana wasiopata malezi mazuri kama waliochanganyikiwa na waliokosa mwelekeo maishani. Kwa upande mwingine, wale wanaopewa motisha na mwongozo unaofaa hufanikiwa maishani. Katika sura ya tano, muhtasari, matokeo na mapendekezo ya utafiti yameshughulikiwa.

# SURA YA TANO

## MUHTASARI, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

### 5.0 Utangulizi

Katika sura iliyotangulia, mambo yanayochangia maendeleo ya vijana yalichunguzwa. Sura hii imeshugulikia muhtasari wa utafiti na matokeo ya utafiti ambayo yalitokana na uchanganuzi wa data iliyokusanywa na matokeo kuwasilishwa kwa mujibu wa malengo ya utafiti huu. Pia, changamoto za utafiti, mchango wa utafiti na mapendekezo yametolewa katika sura hii. Matokeo ya utafiti yametolewa kwa kuongozwa na malengo ya utafiti na mihimili ya nadharia. Mihimili ya nadharia ya Uhalisia imetumika kuonyesha uhalisia wa changamoto zinazowakumba vijana katika jamii. Pia, nadharia ya uhalisia imetumika kuonyesha uhalisia wa wahusika vijana na jinsi wanavyoendeleza maudhui ya mabadiliko na ukuaji. Vilevile, nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii ya Erickson imetumika katika kubainisha maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana na kuchunguza mambo yanayochangia mabadiliko na maendeleo ya vijana.

### 5.1 Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulichunguza maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika Riwaya za *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015) na umeongozwa na malengo matatu. Kwanza, utafiti huu ulilenga kubainisha maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume, kutambua changamoto wanazopitia vijana wa kike na wa kiume katika jamii na suluhu zake na ulitathmini mambo yanayochangia maendeleo ya wahusika vijana. Riwaya zilizoteuliwa ni faafu sana

kwa sababu zimesheheni changamoto wanazopitia wahusika vijana na jinsi wanavyozisuluhisha, mambo yanayochangia maendeleo ya vijana na jinsi wahusika vijana walivyodhihirisha mabadiliko na ukuaji.

Katika sura ya kwanza, masuala ya kimsingi katika utafiti huu yameshughulikiwa. Sura hii iliangazia usuli wa utafiti ambao uliuwekea msingi utafiti huu kwa kuonyesha nafasi ya fasihi katika kuleta mabadiliko na ukuaji wa vijana katika jamii. Sura hii vilevile ilijadili suala la utafiti, maswali ya utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada na upeo na mipaka. Isitoshe, yaliyoandikwa kuhusu mada yamejadiliwa ili kubainisha mchango wa kazi ambazo zimetajwa katika utafiti huu.

Sura ya kwanza vilevile imejadili misingi ya nadharia ambazo zilitumiwa kuongoza utafiti huu. Nadharia hizo ni Uhalisia na Nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii. Hali kadhalika, sura hii imejadili mbinu za utafiti ambazo zilijumuisha usomaji maktabani. Sampuli lengwa, ukusanyaji wa data na uchanganuzi wa data pia zimejadiliwa. Mbinu-kusudio ilitumika kuteua riwaya teule. Ziliteuliwa kwa misingi kwamba wahusika wakuu ni vijana ambao wanapatikana katika umri lengwa. Data ya kimsingi ilikuwa aina ya mabadiliko na ukuaji wa vijana, changamoto zinazowakumba vijana katika jamii na suluhu zake, mwishowe mambo yanayochangia maendeleo ya vijana. Data ilichanganuliwa kwa kuzingatia malengo ya utafiti. Kwa mfano, lengo la kwanza lilimwezesha mtafiti kubainisha maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume. Lengo la pili lilimsaidia mtafiti kuchunguza changamoto wanazopitia vijana wa kike na wa kiume katika

jamii na suluhu zake. Hatimaye lengo la tatu lilimsaidia mtafiti kutathmini mambo yanayochangia maendeleo ya vijana.

Sura ya pili imeshughulikia muhtasari wa riwaya teule, maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume katika jamii kwa kuzingatia riwaya za *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Wahusika vijana, wa kike na wa kiume wametumiwa kuendeleza maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana. Aidha, sura hii imeonyesha kuwa mabadiliko huweza kuwa ya tabia, hali ya maisha, hisia na afya. Nao ukuaji huweza kuwa wa kiakili, kijamii, kimaadili na kihisia. Mabadiliko na ukuaji hutokana na malezi, ushauri nasaha, sheria, ukuzaji wa vipawa, matumizi ya mihadarati na mengineyo. Mihimili miwili ya nadharia ya uhalisia imetumika kubainisha maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana wa kike na wa kiume na pia kuonyesha uhalisia wa wahusika vijana na jinsi wanavyotumika kuendeleza maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana. Pia mhimili wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii umetumika kuchunguza chanzo cha mabadiliko na ukuaji wa vijana.

Sura ya tatu imeshughulikia changamoto wanazopitia vijana katika jamii na suluhu zake katika riwaya teule. Changamoto huwa zinatokana na jamii au kwa vijana wenyewe. Changamoto hizi ni pamoja na umaskini, ukosefu wa malezi bora, dhuluma, uhusiano wa kimapenzi na nyinginezo. Suluhu kwa kila changamoto zimeshughulikiwa. Changamoto hizi zimejadiliwa kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya Uhalisia unaoeleza kuwa fasihi husawiri uhalisia wa maisha.

Sura ya nne imeshughulikia mambo yanayochangia maendeleo ya wahusika vijana katika riwaya za *Chozi Langu* (2014) na *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Kwa kuzingatia mhimili wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii, mambo kama vile; elimu, malezi, ushauri nasaha, jitihada, dini, vyombo vya habari na mengineyo yamejadiliwa. Masuala kama malezi na elimu kwa mfano yameelezwa kama masuala muhimu sana katika maendeleo na mabadiliko ya vijana.

Sura ya tano na ya mwisho imeshughulikia muhtasari, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, mapendekezo na changamoto za utafiti.

### 5.2 Matokeo ya Utafiti

Riwaya za vijana zina umuhimu katika fasihi na pia katika jamii. Licha ya kuburudisha, riwaya hizi zimetumika kama kioo cha jamii katika kuzindua wazazi, vijana na jamii kwa ujumla kuhusu mabadiliko na ukuaji wa vijana.

Ni bayana kuwa vijana wa kiume na wa kike wanadhihirisha mabadiliko na ukuaji kila wanapotangamana na jamii. Mabadiliko ya tabia yanayodhihirishwa ni hasi au chanya. Mabadiliko chanya yanatokana na ushauri nasaha, bidii na jitihada ya vijana na elimu ya darasani na maisha. Kwa mfano, katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Dunia anaonyesha mabadiliko chanya ya kitabia na mabadiliko ya hali ya maisha kupitia ushauri anaopewa na mwalimu mkuu, wazazi na wazee wa kijijini. Aidha, sheria inakuwa msingi wa kubadilisha tabia yake na hisia kuhusu maisha. Anakuwa mwadilifu na mnyenyekevu baada ya kumaliza kifungo chake.

Vilevile, Mliwa katika riwaya ya *Chozi Langu* (2014) anaonyesha mabadiliko chanya alipokubali kurudi shuleni na kuendelea na maisha kama kawaida baada ya

kupewa ushauri nasaha kutoka kwa mama Trufena na rafikiye Mawazo. Hata hivyo, imebainika kwamba, vijana wa kike huonyesha mabadiliko hasi kutokana na dhuluma za kimapenzi, kubaguliwa kiuana na kutawishwa. Mliwa anabadilika kitabia baada ya kubakwa na Chifu Moegi. Anakuwa mnyonge na anaacha kuendelea na masomo. Kulingana na Jerop (2009), wasichana hubakwa na wenzao au watu wazima. Utafiti umebainisha kuwa ubakaji ni suala ambalo huwabadilisha vijana wa kike kitabia na kiafya. Haya ni mambo ambayo yanashuhudiwa nchini Kenya. Kwa mujibu wa mhimili ya nadharia ya Uhalisia unaoeleza kuwa maudhui na matukio yalingane na yale yanayorejelewa katika jamii, maudhui ya mabadiliko na ukuaji yanashuhudiwa miongoni mwa vijana katika jamii. Mliwa anaathirika kisaikolojia baada ya kubakwa. Aidha, katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) afya ya Yasibu inadhoofika baada ya kupata mimba na kuambukizwa virusi vya ukimwi. Vilevile anaonyesha mabadiliko hasi ya tabia baada ya kupitia matatizo mengi mjini. Yasibu anajiingiza katika ukahaba ili kukidhi mahitaji yake ya kila siku.

Isitoshe, vijana hasa wa kiume huweza kubadilika kitabia na hali ya afya kwa sababu ya utumiaji wa vileo na kutelekezwa hasa na wazazi wao. Kwa mujibu wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii, mahitaji ya kibinafsi hukinzana na ya kijamii kwa hivyo huibua mgogoro kwani vijana huona kuwa wanatawaliwa na wazazi. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Dunia ameonyesha mabadiliko hasi baada ya babake kumtelekeza. Babake anapogundua kuwa Dunia anasusia kwenda shule, kunakuwa na mgogoro baina yao. Dunia anajirekebisha na kurudi shuleni lakini babake anakataa kumsamehea kabisa. Babake anakataa kumlipia karo ya shule. Hii inakuwa chanzo cha mabadiliko hasi ya tabia. Dunia anaanza kutumia vileo.

Mabadiliko haya yanatokana na shinikizo analopata kwa rafiki yake Pazia ya kutumia dawa za kulevya. Dunia anakuwa mkaidi na mtundu kwa sababu ya kuvuta bangi. Anapata ujasiri wa kukataa kuendelea na masomo mbele ya hadhira. Malezi yasiyofaa huchangia pia mabadiliko ya tabia, hisia na afya ya vijana. Dunia anapougua homa kali, babake hamjali. Suala hili linamfanya Dunia kuathirika kisaikolojia. Haelewi ni kwa nini babake anakataa kumsamehe. Kwa sababu hii, Dunia naye anabadilika hisia kwa baba yake. Anakuwa na mtazamo hasi kumhusu baba yake ambaye anamtelekeza na kumchukia.

Imebainika kwamba, wasichana wanapotawishwa na kubaguliwa kiuana huweza kuathiri ukuaji na maendeleo yao. Vijana hutaka uhuru wa kutangamana na wenzao huku wazazi wanafikiri kuwa uhuru kwa vijana haufai. Hii inakuwa chanzo cha mabadiliko ya tabia yao au hali. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha umuhimu wa vijana wa kike kuwa huru. Hata hivyo, wanafaa kuwa waangalifu na uhuru huo usivuke mipaka kwani unaweza kuwatia katika hali tatanishi. Yasibu anapopewa uhuru wa kutoka, anajiingiza katika mapenzi ya kiholela ambayo matokeo ni kupata ujauzito. Wazazi wanafaa kuweka sheria licha ya kuwapa vijana uhuru. Hivyo basi, ni dhahiri kuwa malezi mema huweza kuwabadilisha vijana wawe wazuri kitabia. Malezi mabaya huwapotosha vijana na huweza kuchanganyikiwa.

Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), mwandishi ameonyesha kuwa sheria huchangia ukuaji wa vijana wa kiume kimaadili, kijamii, kihisia na kiakili. Dunia anapomaliza kifungo, anaonyesha ukuaji wa kiakili na kimaadili kutokana na

matendo anayoyafanya. Kwa mfano, anatambua umuhimu wa elimu na anajuta kwa kuacha kuendelea na masomo. Pia, anaamua kurudi kwao ili awaombe wazazi wake msamaha na aanze maisha upya.

Aidha, ukuaji miongoni mwa vijana hasa wa kike hutokana na ushauri nasaha. Mliwa katika *Chozi Langu* (2014) anajitambua kuwa anafaa kuacha kusononekea hali yake na kutia bidii masomoni. Mliwa alikuwa na tabia ya kulia kila wakati anapotusiwa kuhusu babake mzazi. Kupitia ushauri nasaha kutoka kwa Mawazo, hali ya Mliwa inabadilika. Maneno kuhusu babake hayakumpiga tena mshipa. Anaonyesha ukuaji wa kiakili na kijamii anapotambua kiini chake cha kuwa hapo shuleni. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) Yasibu naye anabadilisha tabia yake na kuwa kahaba baada ya kuachwa na mumewe. Anaonyesha ukuaji wa kijamii na kiakili anapotambua kuwa alifanya makosa kutoroka kwao nyumbani. Kama Dunia, Yasibu anaamua kurudi nyumbani.

Zaidi ya yote, imebainika kuwa, ukuaji wa vijana hutokana na imani za kidini walizo nazo. Katika *Dunia Mashaka Makuu (*2015), dini inampa Dunia matumaini kuwa siku moja mambo yatabadilika. Anaonyesha ukuaji wa kimaadili anapomweleza Mpoto kuwa kuchukua mali ambayo si halali yako ni makosa mbele ya Muumba wa nchi na Dunia. Dini inawakuza na kuwalea vijana kwa kutoa mafunzo mwafaka. (Kibutu, 2013). Dini inamfanya Dunia kupata malipo kwa jasho lake. Aidha, mateso na hali ngumu ya maisha huwakuza vijana kihisia. Dunia anajifunza kudhibiti hasira yake anapokutana na Pazia anayemkejeli kuwa yeye Dunia aliacha masomo. Dunia anahisi uchungu moyoni ikizingatiwa kuwa Pazia ndiye aliyemhadaa aache masomo.

Anajizuia kumpiga Pazia anapokumbuka mateso aliyoyapitia. Kwa kuzingatia nadharia ya Uhalisia, wahusika katika kazi ya fasihi huwa vielelezo halisi vya binadamu wa kawaida. Imebainika kuwa wahusika kama Dunia, Yasibu na Mliwa ni vielelezo halisi vya vijana katika jamii. Wahusika hawa wametumiwa kuendeleza maudhui ya mabadiliko na ukuaji. Wameonyesha matukio halisi ambayo huwa chanzo cha mabadiliko na ukuaji wa vijana.

Vijana baleghe hukumbwa na changamoto nyingi sana ambazo angalabu huweza kuathiri maendeleo na ukuaji wao. Hata hivyo, kuna suluhu kwa baadhi ya changamoto zinazowakumba. Mwandishi wa *Chozi Langu* (2014) ameonyesha kuwa umaskini huathiri masomo ya vijana kwani wengi wao hukosa karo ya shule. Umaskini huchangia ukosefu wa elimu bora. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha kuwa baadhi ya vijana hutaka kujiweka katika hali ya umaskini kwa kupuuza mashauri wanayopewa na wazazi au kwa kuacha kusoma. Kwa mfano, Dunia anajipata katika hali ya umaskini kwa sababu ya ukosefu wa elimu bora. Yasibu naye anashiriki katika mapenzi ya kiholela na kupata ujauzito. Masomo yake yanakatizwa na anapoenda mjini, anaishi katika hali ya umaskini na baadaye anakufa kutokana na ugonjwa wa Ukimwi. Hata hivyo, kupitia bidii na jitihada, kijana huweza kufanikiwa maishani. Kwa mfano, licha ya Mliwa katika *Chozi Langu* (2014) kukumbwa na umaskini aliweza kutia bidii masomoni na mwishowe akafaulu. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015), Dunia na Mpoto wanafanya kazi kwa bidii ili waweze kubadilisha hali ya umaskini.

Hali kadhalika, ukosefu wa usalama ni changamoto inayokumba vijana wa kike na wa kiume na serikali imechangia zaidi katika kusababisha changamoto hii. Kwa mfano, katika *Chozi Langu* (2014) mwandishi ameonyesha kuwa vijana wa kike hawana usalama hasa wale wanaoishi katika maeneo duni. Kwa maoni ya Stringer (2017), serikali inafaa kuhakikisha kuwa mahali ambapo vijana wanaishi pana usalama wa kutosha. Mliwa anabakwa kwa sababu ya ukosefu wa usalama. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi naye ameonyesha wazi kuwa vijana wa kiume wanashukiwa kuwa wezi hasa wanapopatikana katika mazingira tatanishi. Hawapewi nafasi ya kujitetea. Dunia anafungwa mara mbili bila kufanyiwa uchunguzi wa kina. Pia, anaibiwa kila kitu alipokuwa hotelini na kubaki bila nguo. Badala ya kusaidiwa na polisi, wanamkamata na kumtia ndani kwa kumshuku kuwa ni jambazi anapopatikana nusu uchi bustanini. Stringer (2017) anasema kuwa, ni vizuri vijana wasikizwe kabla ya kufungwa, kwani kuna baadhi ya vijana ambao hawastahili kifungo bali kupewa tu mawaidha.

Kwa kiwango kikubwa, matokeo ya utafiti yanaonyesha kuwa, ukosefu wa malezi bora huathiri ukuaji wa vijana baleghe. Imebainika kwamba, wazazi wamechangia malezi mabaya kwa vijana. Kwa maoni ya Dacey na John (2009), familia zinazohangaika kwa kukosa malezi bora watoto pia wanakosa vielelezo bora na hata wanakosa elimu ya kimsingi. Hili linajitokeza katika *Chozi Langu* (2014) ambapo Mliwa anakosa chakula na amani kwa sababu ya mzozo uliokuwepo kati ya wazazi. Mliwa anapata mawaidha kutoka kwa rafiki yake Mawazo. Mawaidha haya yanamsaidia na hivyo anakuwa na mbinu ya kukabiliana na changamoto hii kwa kujibidiisha kwa masomo na kupuuza yale masimango kutoka kwa wenzake. Katika

*Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha wazi kuwa malezi mabaya yanajitokeza kuwa na athari hasi ya kutowajibika kwa Yasibu na Dunia. Wazazi wao wanashindwa kuwaelekeza ipasavyo. Vijana hawa wanapoteleza, baba yao anawachukia zaidi na kukosa kuwasamehe licha ya wao kujuta na kuomba msamaha mara nyingi. Vijana hawa wanatorekea mjini hadi dunia inapowafunza kuwa elimu ni muhimu katika maisha yao. Kwa mujibu wa Jeffrey na Brown (2003), vijana katika umri wa kubaleghe wanafaa kuelekezwa ipasavyo. Wazazi wanafaa kujua watu wanaotangamana nao na vijana wanatumia muda vipi.

Vilevile, msongo wa mawazo hutokana na matatizo yanayowakumba vijana baleghe katika jamii. Vijana wa kike wanaobaleghe huathirika zaidi Kisaikolojia na masomo yao hukatizwa wanapokumbwa na changamoto kama vile mimba za ujanani, mapenzi ya kiholela, dhuluma ya kimapenzi na kubaguliwa kiuana. Kwa mfano, Mliwa katika *Chozi Langu* (2014) ananyimwa nafasi ya kusoma kwa sababu ni mtoto wa kike. Kwa mujibu wa Kimani (2003) na Momanyi (1998), dhuluma hizi zinawakabili vijana wa kike kwa sababu ya maumbile yao na wanaume wanawachukulia kama viumbe duni. Katika hali hii wasichana wanajihisi wapweke, kukataliwa na huweza kujitia kitanzi. Mwandishi wa *Chozi Langu* (2014) ameonyesha kuwa Mliwa anazongwa na mawazo anapobakwa na kuhusu suala la mamake kufukuzwa na babake. Kama wanavyosema Jeffrey na Brown (2003), wazazi wanapozozana vijana huathiriwa zaidi kisaikolojia. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha athari ya mapenzi ya kiholela na mimba za ujana. Yasibu anashindwa kustamihili mihemko ya mapenzi akiwa na umri wa miaka kumi na mitano na hivyo anapata mimba na kuacha masomo ilhali Pazia aliyehusika

anaendelea na masomo. Yasibu anakumbwa na msongo wa mawazo. Kwa mujibu wa waandishi wa riwaya teule, vijana wanafaa kupewa ushauri mwafaka. Wazazi wanafaa kuwa waangalifu sana vijana wanapotaka uhuru. Wanafaa kujua vijana hawa wanatembea na nani au wanafanya nini.

Matumizi ya mihadarati ni changamoto kubwa zaidi miongoni mwa vijana hasa wa kiume. Vijana wanapotumia dawa za kulevya, hubadili tabia zao na kuwa watundu. Tatizo la matumizi ya dawa za kulevya limekithiri katika jamii. Dunia katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) alikosa mapenzi kwao nyumbani na hivyo akashirikiana na rafikiye Pazia ambaye alimfunza matumizi ya dawa za kulevya. Shinikizo la marika lina athari kubwa sana kwa vijana na hivyo basi wazazi wanafaa kuwa waangalifu sana ili kujua marafiki wa wanao.

Imebainika kuwa dhuluma na vifungo vya jela ni changamoto inayowakumba hasa vijana wa kiume. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha kuwa, vitisho na kutukanwa kwa vijana si njia mwafaka ya kuwarekebisha. Dunia anadhulumiwa na baba yake kwa kutukanwa kila mara. Kwa mujibu wa Jeffrey na Brown (2003), wazazi wanafaa kuwasikiza vijana na kuwa karibu nao ili waweze kuwaelewa vijana. Pia, Dunia anadhulumiwa akiwa gerezani kwa kupewa chakula kidogo na kazi ngumu. Dunia anapokuwa mgonjwa akiwa gerezani, hapewi matibabu. Anaambiwa kutoa hongo ndipo apewe dawa. Kwa mujibu wa Stringer (2017), lengo la kifungo kwa vijana baleghe ni kuwafunza maadili na mafunzo mengine yatakayowasaidia wanapotoka kifungoni lakini si kuwapa adhabu kama ya watu wazima.

Waandishi wa riwaya teule wameangazia changamoto zinazowakumba vijana wa kike na kiume katika jamii na suluhu zake. Changamoto zinazoangaziwa hapa ni zile ambazo zinapatikana katika jamii ya sasa. Kwa mujibu wa nadharia ya Uhalisia, fasihi husawiri uhalisia wa maisha katika ngazi zote kama vile siasa, uchumi, utamaduni na jamii. Mambo yanayowaathiri wahusika vijana kama Mliwa, Dunia na Yasibu ni yale ambayo yanawaathiri vijana wa kawaida.

Utafiti huu umeonyesha kuwa maendeleo miongoni mwa vijana hutokana na mambo mbalimbali. Imebainika kwamba elimu na jitihada ni muhimu sana katika kuleta mabadiliko na maendeleo yao. Elimu huwapa vijana uwezo wa kupambana na mila na tamaduni zisizofaa. (Kibet, 2016). Katika *Chozi Langu (2014)* mwandishi ameonyesha umuhimu wa elimu katika kubadilisha hali ya maisha ya Mliwa. Kupitia juhudi za Mliwa shuleni anapata ufadhili kutoka kwa shule yao na pia kutoka kwa shirika la utangazaji. Anafuzu na kuwa mtangazaji maarufu. Hata hivyo, mwandishi wa *Dunia Mashaka Makuu* (2015) ameonyesha kuwa bila elimu, vijana hukosa mwelekeo maishani. Dunia na Yasibu waliokataa kusoma na kutorokea mjini, wanapata mateso mengi sana.

Ushauri nasaha kutoka kwa walimu, wazazi, vijana, wazee wa dini na wataalamu wa masuala mbalimbali ni njia mwafaka ya kuwabadilisha na kuwaendeleza vijana. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) babake Dunia na mwalimu mkuu wanapomshauri Dunia kuhusu umuhimu wa elimu, Dunia anazinduka na kurudi shuleni. Vilevile, katika *Chozi Langu* (2014) mwandishi ameonyesha umuhimu wa ushauri nasaha miongoni mwa vijana. Vijana wanafaa kukumbushwa kila mara kuwa

licha ya changamoto wanazopitia ni muhimu wawe na matumaini. Kwa mujibu wa mhimili wa nadharia ya Ukuaji wa Kisaikolojia na Kijamii, katika hatua ya kujitambulisha, vijana hutaka kujitegemea na kukuza nafsi zao, wale wanaopewa motisha huwa na ujasiri wa kujitegemea ilhali wale wasiopewa mwongozo unaofaa huchanganyikiwa. Mliwa anapitia changamoto nyingi sana lakini hafi moyo. Anaendelea kutia bidii kutokana na ushauri anaopewa kila mara na mamake mzazi, walimu wake na wenzake na mwishowe akafaulu.

Aidha sheria, dini, vyombo vya habari na ukuzaji vipawa yamesawiriwa kama mojawapo ya mambo yanayowaendeleza vijana. Katika *Dunia Mashaka Makuu* (2015) mwandishi ameonyesha jinsi Dunia anavyobadilika na kuwa mwadilifu kutokana na kifungo alichopata baada ya kushukiwa kuwa ni mwizi. Isitoshe, sheria imetumika kuwalinda vijana dhidi ya dhuluma za kijamii kwa mfano ubakaji. Mliwa katika *Chozi Langu* (2014) anapewa haki yake baada ya kubakwa ambapo Chifu Moegi anafungwa kifungo cha maisha.

Vyombo vya habari ni asasi ya kuwasaidia vijana katika masuala ya elimu, kukuza vipawa vyao na kupambana dhidi ya maovu. Kupita magazetini na redioni, vijana wanahamasishwa kupigana dhidi ya uovu ambao wanatendewa. Katika *Chozi Langu* (2014), shirika la utangazaji linajitolea kumlipia Mliwa karo ya shule baada ya kushinda shindano la utangazaji. Zaidi ya hayo, Mliwa anaahidiwa kupewa mafunzo ya Uanahabari. Baada ya kuhitimu katika chuo kikuu Mliwa anapata kazi ya utangazaji katika kituo maarufu cha Redio Kisu. Dini inawasaidia vijana kuwa na matumaini na pia kuwafadhili. Mliwa anapata ufadhili kutoka kwa kanisa lao.

Malezi anayopewa kijana hujenga tabia yake ya usoni. Kijana anapolelewa kwa njia inayofaa, anaweza kujiendeleza na kubadilisha hali yake ya maisha. Katika *Chozi Langu* (2014) Mliwa analelewa na mama pekee. Hata hivyo, anamlea kwa mapenzi na busara. Mliwa anafanikiwa maishani. Imebainika kuwa, mtoto akilelewa na wazazi wasiowajibika au wanaokosa kumpa mwongozo unaofaa, huchanganyikiwa katika majukumu yake ya usoni na hukosa mwelekeo maishani. Haya yanaonekana wazi hasa pale ambapo Dunia na Yasibu katika riwaya ya *Dunia Mashaka Makuu* (2015) walilelewa kwa chuki na uhasama.

## 5.3 Changamoto za Utafiti

Utafiti huu ulikumbwa na changamoto ya ukosefu wa vitabu vya Kiswahili. Ili kuweza kupata dhana mbalimbali na maelezo zaidi hasa ya kinadharia, mtafiti alilazimika kusoma vitabu vilivyoandikwa katika lugha ya Kiingereza na kutafsiri kwa Kiswahili. Halikuwa jambo rahisi kutafsiri ikizingatiwa ya kwamba, kuna msamiati wa Kiingereza ambao haupatikani katika lugha ya Kiswahili. Pia, baadhi ya maneno yalikosa visawe vyake na mtafiti alilazimika kutumia baadhi ya istilahi za Kiingereza ili kufanikisha utafiti huu. Vilevile, taarifa zilizotolewa mtandaoni zilikuwa zimeandikwa kwa Kiingereza kwa hivyo zilihitaji kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili jambo ambalo halikuwa rahisi.

## 5.4 Mchango wa Utafiti

Utafiti huu umenuia kuwafaidi watafiti wa fasihi ya Kiswahili kuhusu maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe na jinsi wahusika huchangia katika

kuendeleza maudhui katika kazi ya fasihi. Watafiti wa kazi ya fasihi watatumia mchango wa utafiti huu kwa kazi zao ili kuupa utafiti wao msingi.

Utafiti huu utawafaa wasomi na wahakiki wa fasihi ya Kiswahili kwa kuchangia hazina ya usomi wa fasihi. Hii ni kwa sababu tasnifu hii itakuwa kazi ya marejeleo kwa wasomi na wahakiki wa fasihi. Vilevile, wakuza mitalaa ya fasihi na Saikolojia watafaidika kwa sababu utafiti huu umeshughulikia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana ambayo ni masuala ya kisaikolojia na ya kijamii.

Matokeo ya utafiti huu utawafaidi wachanganuzi wa masuala ya kijamii, kisiasa na kiuchumi kwa kuwafafanulia chanzo cha mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe. Wanajamii wanapoelewa mambo hayo, watakuwa makini sana katika kuwalea vijana kwa njia inayofaa. Na kama kutakuwa na mabadiliko yawe chanya. Iwapo ni hasi, wanajamii watapata njia mwafaka ya kurekebisha mambo kwani wataweza kujua kiini chake. Vilevile, utafiti umeonyesha kuwa baadhi ya changamoto wanazopitia vijana huwatia ari katika masomo yao. Kiini ni kwamba wanataka kubadilisha hali yao kwa kujiendeleza kiuchumi. Hivyo basi, utafiti huu utawapa vijana motisha hasa wale wanaopitia changamoto kama hizo matumaini katika maisha.

## 5.5 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Utafiti huu umeangazia maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana katika riwaya za *Chozi Langu (2014)* na *Dunia Mashaka Makuu* (2015). Mtafiti alieleza jinsi waandishi wa riwaya teule wameainisha aina ya mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe. Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi ili kubainisha mabadiliko na ukuaji katika tanzu nyingine kama vile ushairi na hadithi fupi.

Utafiti huu ulichunguza maudhui ya mabadiliko na ukuaji wa vijana baleghe. Ni muhimu kutafiti kuhusu mabadiliko na ukuaji katika kiwango tofauti kwa mfano vijana wa kati ya umri wa miaka ishirini hadi thelathini na mitano ili kufafanua ikiwa vijana katika umri huu huonyesha mabadiliko na ukuaji kutokana na changamoto zinazowakumba.

## MAREJELEO


Adhiambo, M. (2018, November 3). Teenage Pregnancy Becoming a National Threat. *Standard Media Group*. Retrieved from http://www.standardmedia.coke. On 10/9/2019

Akoth, S. (2018, November 8). Teen Pregnancy crisis Requires a New Approach. *People Daily*. P.11

Awiti, A. and Scott, B. ( 2016). The Kenya Youth Survey Report. *East Africa Institute.* Retrieved from https://www.ecommons.aku.edu/eastafrica_eai/17. On 18/1 2016

Cherry, K. (2017*).* Erick Erickson Stages of Psychosocial Development. Retrieved from *http://www.verywell.com. On 20/9/2018*

Chesang, K. (2013*).* Drug Abuse Among the Youth in Kenya. *International Journal of Scientific Research*, 2 (6). Retrieved from *http://www.ijistr.org*. On 16/10/2020

Committee of Experts on Constitution Review. (2010*) Harmonized Draft Constitution of Kenya.* Nairobi: Government Printers.

Cosby, B., Rick, L., Charlie, W., Clement, S. & Barbara, V. (2000). *Lions Quest, Skills For Adolescents: Changes and Challenges 4th* Asian Edition. India: Lions Club International.

Crowe, C. (1998). What is Young Adult Literature. *The English Journal*, 88 . National Council of Teachers of English.

Dacey, J. and John, F. (2009). *Human Development Across the Lifespan*. New York: McGraw-Hill International.

Erickson, E. and Erickson, J. (1998). *The Life Cycle Completed*: *Extended Version*. New York: W.W.Norton.

Jeffrey, B. and Brown, P. (2003). *A Guide to Parenting*. England: The Stanborough Press.

Kamote, I. (2016). Ufahamu Kuhusu Saikolojia. *Makala ya Dira ya Elimu*. Retrieved from *https://diraElimu.blogspot.com. On 12/9/2018*

Kaui, T. (2008). Usawiri wa Vijana Katika Tamthilia Teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili ya Chuo Kikuu cha Kenyatta. ( Haijajapishwa).

Kezilahabi, E. (2005). *Rosa Mistika*. Dar-es-Salaam: Kenya Literature Bureau.

Kibet, E. (2016). Usawiri wa Vijana Katika Tamthilia ya *Mbaya Wetu*. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. ( Haijajapishwa)

Kibutu, S. (2013). Maudhui na Mitindo ya Lugha inayotumiwa kuwasilisha Mafunzo ya Kukuza Vijana Katika Misingi ya Kiuana; Dhehebu la P.C.E.A Kikuyu. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijajapishwa).

Kihara, S. (2016). Nafasi ya Vijana katika Riwaya za *Pendo La Karaha* na *Kovu Moyoni*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. ( Haijajapishwa).

Kimani, C. (2003). Suala la Dhuluma Dhidi ya Wanawake Katika Fasihi ya Kiswahili. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijajapishwa).

King'ei, K. na Kisovi, C. (2010). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Kiprugut, D. (2011) Dini kama Chombo cha Kuwadhulumu Waumini: Mifano Kutoka Fasihi Katika Kiswahili. Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu Cha Kenyatta. (Haijajapishwa).

Kroger, J. (2004). *Identity in Adolescence: The Balance Between Self and Other. 3rd Edition*. New York London: Routledge.

Jerop, R. (2009). Sexual Abuse of School Age Children: Evidence in Kenya. CICE Hiroshima University, *Journal of International Cooperation in Education.* 12 (1), 177-192.

McLeod, S. (2013). *Kohlberg's Stages of Moral Development*. Retrieved from https://www.simplypsychology.org. On 20/11/2018

McNeely, C. and Blanchard, J. (2009). *The Teen Years Explained; A Guide to Healthy Adolescent Development*. U.S.A: Center for Adolescent Health at Johns Hopkins Bloomberg School of Public Health.

Mogambi, H. (2014). *Chozi Langu*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Momanyi, C. (1998). Usawiri wa Mwanamke Muislamu Katika Jamii ya Waswahili Kama ilivyobainika Katika Ushairi wa Kiswahili. Tasnifu ya Ph.D. Chuo Kikuu cha Kenyatta. (Haijajapishwa)

Mumbi, M. (2017). Teen boy kills a 16 year old girl in Mirera, Naivasha. *Pulse Live Kenya.* Retrieved from http://www.pulselive.co.ke.

Mutembei, K. (2013). Hali ya Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili KatikaTanzania. Retrieved from http://www.coursehero.com. *On 27/9/2018*

Mureithi, F. (2016). Changamoto Zinazowakumba Vijana katika Riwaya za *Upotevu* na *Dunia Uwanja wa Fujo*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijajapishwa).

Naliaka, R. (2012). Hali ya Vijana Katika Riwaya ya *Vipanya vya Maabara*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. ( Haijajapishwa).

Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari.* Nairobi: Phoenix Publishers Limited.

Njogu, K. na Chimera, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Ntaragwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Kiswahili*. Augustana College: Rock Island.

Nyamai F. (2017, March 28) Child Abuse in Nairobi. *Daily Nation*.

Nyamemba, R. (2012). Uchanganuzi Linganishi wa Maswala ya Vijana na Jinsi yanavyoshughulikiwa na Waandishi Katika Diwani ya *Tunu ya Ushairi*. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Nairobi. (Haijajapishwa).

Odaga, A. (1985). *Literature for the Children and the Young People in Kenya.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Okun, M. (2018, January 3). Give our Girls a future by preventing Teen Pregnancy. *Daily Nation*.

Omar, L. ( 2015). *Dunia Mashaka Makuu*. Nairobi: City Book Publishers.

Onyango, P. and Tostensen, A. (2015). The Situation of Youth and Children of Kibera. Retrieved from *http://www.cmi.ne /publications/file/5527.On 20/9/2018*

Plotnik, R. (1996*). Introduction to Psychology* (4th ed.) U.S.A: Brooks/Cole Publishing Company.

Siddarth, C. (2018). Teenage Pregnancy in Kenya: Acrisis of Health, Education and Opportunity. *Thomson Reuters Foundation.* Retrieved from *https://www.ipsnews.net/2018/11/teenage-pregnancy-kenya-crisis-health-education-opportuniy/*

Stringer, H. (2017). Justice for Teens. *American Psychological Association.* 8 (9), 44.

TUKI. (2004). Kamusi ya Kiswahili Sanifu. Nairobi: Oxford University Press.

Wafula, R. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia, Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wafula, R. na Njogu, C. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publications.

Wamitila, K.W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publication Limited.

Wood, S. (2011). *The World of Psychology*. U.S.A: Pearson Allyn and Bacon.

Young Adult Library Service Association, ( 2011). Young Adult Fiction. Retrieved from www./en.wikipedia.org/wiki/young-adult-fiction. On 18/9/2017